**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua Pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. FA.27/249/01/2013/2014/42/01 Tarehe 26 Machi 2015

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
1 Barabara ya Barack Obama,
**11400 DAR ES SALAAM.**

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), nawasilisha kwako ripoti ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoelezewa katika Sehemu ya 3 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii, inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2013, 31 Disemba, 2013 na tarehe 30 Juni, 2014. Nawasilisha kwako ripoti hii kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

**Prof. Mussa Juma Assad**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

***(Imeanzishwa kwa Mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)***

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeainishwa katika Ibara 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muunganowa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 (iliyorekebishwa) iliyofafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

**Dira ya Ofisi**
Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

**Lengo la Ofisi**
Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya misingi vifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **Kutopendelea** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki bila upendeleo. |
| **Ubora** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalam inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma vya Kimataifa. |
| **Uadilifu** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi ya kiwango cha juu na kuheshimu sheria. |
| **Kujali Watu** | Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na kuongeza tija. |
| **Ubunifu** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi. |
| **Matumizi bora ya Rasilimali za Umma** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake. |

# YALIYOMO

**Ukurasa**

Orodha ya Majedwali ........ vi
Orodha ya Vielelezo ........ vii
Shukrani ........ viii
Dibaji ........ x
Muhtasari ........ xii
**Sura ya Kwanza** ........ 1
Utangulizi na Taarifa za Jumla ........ 1
**Sura ya Pili** ........ 8
Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa ........ 8
**Sura ya Tatu** ........ 14
Muhtasari wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita ........ 14
**Sura ya Nne** ........ 27
Masuala Muhimu ambayo hayakutolewa Taarifa katika Ripoti ya Mwaka Uliopita ........ 27
**Sura ya Tano** ........ 39
Usimamizi wa Sheria ya Ununuzi na Mikataba ........ 39
**Sura ya Sita** ........ 60
Usimamizi wa Mali za Umma ........ 60
**Sura ya Saba** ........ 69
Usimamizi wa Rasilimali Watu ........ 69
**Sura ya Nane** ........ 79
Utawala Bora ........ 79
**Sura ya Tisa** ........ 93
Hali ya Madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ........ 93
**Sura ya Kumi** ........ 98
Matokeo ya Kaguzi Maalumu ........ 98
**Sura ya Kumi na Moja** ........ 107
Hitimisho na Mapendekezo ........ 107

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Ukurasa**

Jedwali 1:Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa ........ 10
Jedwali 2:Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti ya mwaka 2012/2013 ........ 15
Jedwali 3:Orodha ya kutosuluhishwa kwa tofauti zilizojitokeza ........ 30
Jedwali 4:Akaunti za Benki Zilizoonyesha Deni ........ 31
Jedwali 5:Wadai wa muda mrefu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ........ 32
Jedwali 6:Hali ya Uhai wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ........ 34
Jedwali 7:Stakabadhi zilitolewa kabla ya malipo ya ada ya leseni ........ 37
Jedwali 8:Zabuni zilizotekelezwa zaidi ya ukomo uliowekwa kisheria ........ 45
Jedwali 9:Zabuni zilizotekelezwa kinyume na matakwa ya sharia ya Ununuzi wa Umma ........ 46
Jedwali 10:Mikataba ambayo haionyeshi ukomo ........ 55
Jedwali 11:Makato ya kisheria yaliyolipwa zaidi NSSF na Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam ........ 76
Jedwali 12:Kiasi cha PAYE na SDL kilicholipwa zaidi (Bandari Makao Makuu, Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Kyela) ........ 76
Jedwali 13:Kiasi cha SDL Kilicholipwa Kinyume na Utaratibu – Bandari ya Dar es Salaam ........ 77
Jedwali 14:Deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kufikia Tarehe 30 Juni, 2014 ........ 95
Jedwali 15:Deni la Serikali kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii hadi tarehe 30 Septemba, 2014 ........ 96

## ORODHA YA VIELELEZO

**Kielelezo namba 1:** Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2013/2014................................. 6

**Kielelezo namba 2:** Mgawanyo wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.......................... 10

**Kielelezo namba 3:** Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi........................................................ 11

## SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia mkazo masuala mbalimbali yanayoandikwa kwenye ripoti zangu.

Shukrani pia, ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Wabunge wote kwa kujitoa kwa dhati kujadili na kutoa maelekezo ya mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya utekelezaji.

Napenda kumshukuru kiongozi aliyenitangulia aliyestaafu kwa mujibu wa sheria, Bwana Ludovick S.L. Utouh kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kujenga mifumo mizuri ya kiutendaji katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo imeniwezesha mimi kutoa ripoti ya mwaka ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa wakati.

Napenda pia kutoa shukrani kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilizokaguliwa, kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani kwa Mpiga Chapa kwa kukamilisha uchapaji wa ripoti hii na hivyo kuifanya itoke na kuweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge kwa muda uliowekwa kisheria.

Zaidi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabia wa maendeleo ambao wamekuwa wakitoa msaada kwa Ofisi yangu, hususani Mpango wa Maboresho wa Menejimenti ya Fedha za Umma (PFMRP) chini ya usimamizi wa Benki ya Dunia, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden (SIDA), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB), Wakala wa Maendeleo wa Kimataifa wa Canada (CIDA), Umoja wa Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Kiafrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya India (SAI India), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya China (SAI China), Serikali ya watu wa Marekani kupitia Shirika lao la Maendeleo (USAID), Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika lake la Maendeleo (GIZ) na wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa kwa kufadhili mafunzo ya wafanyakazi na kutupatia vifaa mbalimbali zikiwemo kompyuta na magari.

Aidha, napenda kuyashukuru makampuni binafsi ya ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya ukaguzi wa hasabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba yangu.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kujitolea kwao na jitihada walizoonyesha katika kukamilisha ripoti hii. Kujitolea kwao kumekuwa kwa manufaa na faraja sana kwangu. Nawasihi waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na umoja kwa siku zijazo ili kuendelea kudumisha heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za umma.

## DIBAJI

Ninayo furaha na heshima kuwasilisha ripoti hii ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2013/2014. Ripoti hii ni mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma inayoainisha masuala husika yaliyozorotesha ufanisi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza na kufikia malengo waliyojiwekea.

Ripoti hii, inalenga kuwataarifu wadau kama vile Serikali, Bunge, Mahakama, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kijamii na Umma wa Watanzania kwa ujumla, muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2013/2014.

Katika kipindi hiki ambacho kumekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, uwazi na utawala bora ni jambo muhimu kwa watendaji kusimamia kwa makini mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma na kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha. Napenda kueleza kuwa ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka, 2008.

Ili kuhakikisha kuwa kazi yangu inachangia katika maendeleo ya Taifa, ofisi yangu imekuwa ikipitia na kuboresha mbinu za ukaguzi mara kwa mara ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau wangu. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele ili kuhakikisha wanapata uelewa wa sheria, miongozo, kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za taaluma ya uhasibu na ukaguzi za kimataifa kama vile “IFAC”, “INTOSAI” na nyinginezo ambazo ofisi yangu ni mwanachama.

Katika kudumisha weledi, Wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wamekuwa wakifanyiwa Mafunzo, ili kuongeza ubora na ufanisi katika kufanya kazi. Kwa mtizamo huo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina mpango wa kujenga Kituo cha Mafunzo ya Ukaguzi katika eneo la Gezaulole lililoko Kigamboni-Dar es Salaam. Ninayo imani kubwa na Serikali kuwa itaendelea kusaidia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika nyanja zote, ili kukamilisha mradi huo, kwani imeona na kutambua umuhimu wa kutoa mafunzo kwa Wakaguzi.

Ni vyema ikafahamika kwamba, vyombo vyenye dhamana ya uangalizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zinafuatwa ndani ya Taasisi, Bodi za Wakurugenzi na Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho

Kikwete na Serikali yake kwa ujumla, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge kwa ujumla, Wadau wa Maendeleo na Benki ya Dunia kwa michango yao katika kufanikisha kuongeza kasi ya uwajibikaji katika nchi yetu.



**Prof. Mussa Juma Assad**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

26 Machi, 2015

# MUHTASARI

## Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii na zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa Mashirika na Tasisi Nyinginezo za Umma.

Ripoti hii inajumuisha hoja mbalimbali zilizotolewa katika ripoti za ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinazoonyesha kuwepo kwa mapungufu yanayokwamisha utendaji ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi. Hoja hizo kwa kifupi ni kama ifuatavyo:-

## i. Hali ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokaguliwa

Hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2015 nimekamilisha kaguzi 125 kati ya kaguzi 180 zilizotakiwa kufanyika kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Katika Kaguzi zilizokamilika, ripoti za mashirika 109 ziliridhiwa na Bodi za Wakurugenzi na kuzitolea hati za ukaguzi, wakati Mashirika 16 yalikuwa hayana Bodi za Wakurugenzi hivyo kushindwa kuridhiwa kwa hesabu zake. Kaguzi 52 zilizobakia zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, Mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za Wakurugenzi kuridhia hesabu na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati, hali iliyosababisha zoezi la ukaguzi kutokamilika kwa wakati. Mashirika matatu (3) hayakuwasilisha hesabu zake kwa ajili ya kukaguliwa yakiwemo Shirika la Reli Tanzania (TRL), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Kampuni ya Huduma za Majini (Marine Services Company).

Kati ya kaguzi za mashirika 109 zilizokamilika na kutolewa hati za ukaguzi, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma 105 (96%) yalipata hati zinazoridhisha wakati Mashirika 4 (4%) yalipata hati zenye shaka. Mwaka huu hati isiyoridhisha au mbaya hazikutolewa kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Hata hivyo, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zipatazo 39 kati ya 105 zilizopata hati zinazoridhisha na mbili (2) ambazo zilipata hati zenye shaka, zilikuwa na masuala yenye msisitizo.

Vile vile napenda kubainisha kwamba, baadhi ya Mashirika ya Umma yamekumbana na kupungua kwa mtaji na hivyo kusababisha uzorotaji wa hali ya kifedha kutokana na hasara mfululizo kwa zaidi ya miaka miwili. Hii imesababisha matatizo ya kifedha kwenye mashirika hayo hali iliyoyafanya yashindwe kulipa madeni ya muda mfupi. Pia, ninatoa angalizo au msisitizo kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yaliyokuwa

yanakabiliwa na madeni tarajiwa (contingent liabilities) yenye jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 52.36 na Dola za Kimarekani milioni 258.761 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatisho cha IV. Madeni tarajiwa (contingent liabilities) yalitokana na uwepo wa mashauri yaliyokuwa yakiendelea katika mahakama mbali mbaaali ambayo matokeo yake bado hayajajulikana.

**ii. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita**

Katika ripoti zangu za kila mwaka huwa ninatoa mapendekezo kwa Serikali pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuchukua hatua stahiki kutatua kasoro ambazo zimejitokeza wakati wa ukaguzi. Katika ripoti ya mwaka 2012/2013 kulikuwa na mapendekezo 31.

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, ufuatiliaji wa mapendekezo ya miaka ya nyuma umebaini kuwa mapendekezo mawili (2) (6%) yametekelezwa, mapendekezo kumi na mbili (39%) hayajatekelezwa na mapendekezo kumi na sita (52%) yanaendelea kutekelezwa huku moja (3%) likiwa limepitwa na wakati. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo imejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu ya ripoti hii. Baadhi ya mapendekezo hayo hayajafanyiwa kazi na Watendaji Wakuu na Bodi za Mashirika husika kwa zaidi ya miaka mitano. Hii inamaanisha kuwa watendaji husika hawatekelezi majukumu yao ipasavyo. Mapendekezo ya muda mrefu ambayo hayajatekelezwa yamekuwa yakijirudia rudia kama mapungufu katika ripoti zangu za kila mwaka. Hali hii inapunguza juhudi za ofisi yangu katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma.

Napenda kutambua jitihada za Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu mapendekezo yaliyojitokeza katika ripoti yangu ya mwaka 2012/2013. Kwa ujumla utekelezaji wa mapendekezo niliyotoa hauridhishi kwani mapendekezo mengi yapo katika hatua za utekelezaji na mengine bado hayajatekelezwa kabisa.

**iii. Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka 2012/2013**

Masuala muhimu ya hoja zilizotolewa taarifa katika ripoti za kaguzi moja moja za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma lakini hazikuripotiwa katika ripoti ya jumla ya mwaka 2012/2013 ni kama zinavyoonyeshwa hapa chini kwa muhtasari:

Nilibaini kuwepo kwa madeni ya muda mrefu katika Shirika la Posta Tanzania (TPC) yenye kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 2.695, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) Shilingi za Kitanzania milioni 215.66 na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Shilingi za Kitanzania bilioni 3.289. Shirika la Posta Tanzania (TPC) lilikuwa na tofauti ya Shilingi za Kitanzania milioni 436.2 ikiwa ni tofauti kati ya taarifa za benki na zile za Shirika ambazo

mpaka wakati wa ukaguzi zilikuwa hazijasuluhishwa. Pia, kulikuwa na ucheleweshwaji katika kuwasilisha makato ya kisheria uliobainika katika Shirika la Posta Tanzania (TPC) inayojumuisha PAYE Shilingi za Kitanzania bilioni 4.019, VAT Shilingi za Kitanzania bilioni 2.063 na SDL Shilingi za Kitanzania bilioni 2.679. Pia, katika Shirika hilo ilibainika kuchelewa kulipwa michango ya wafanyakazi kwenda kwenye mfuko wa PPF kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 2.6.

Wadai wa muda mrefu walibainika katika Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 236.833 na milioni 100.22 sawia. Chuo Kikuu cha Dodoma kilichelewa kukusanya kodi ya pango kutoka kwa Kampuni ya Taji Ltd kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 84.50. Pia, ilibainika katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya daftari la kumbukumbu la mali halijahuishwa hali iliyopelekea kutosuluhishwa kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 3.89. Vile vile, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Shirika la Utafiti na Maedeleo ya Viwanda Tanzania, kulikuwa na mali katika maghala ambazo zilikuwa hazijahakikiwa zenye thamani ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 129.95 na Shilingi za Kitanzania milioni 6.51 sawia.

Ukaguzi ubaini viashiria vya matatizo ya kujiendesha katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) kama ilivyofafanuliwa katika sura ya nne ya ripoti hii. Mamlaka ya Kanda ya Uwekezaji Tanzania (EPZA) ililimbikiza riba ya Shilingi za Kitanzania bilioni 3.297 kutokana na kuchelewa kulipa fidia kwa wamiliki wa ardhi.

Pia, nilibaini kutoandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Shirika, na kutokuonyeshwa kwa akaunti ya Dhamana ya Utendaji katika Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania. Pia, vibali vya ghala na stakabadhi ya dhamana vyenye thamani ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 260 vilitolewa kabla ya waombaji wa leseni za maghala kufanya malipo.

### iv. Ununuzi na Usimamizi wa Mikataba

Shughuli za ununuzi zimeendelea kuchukua nafasi kubwa katika bajeti ya matumizi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Kwa ajili hiyo suala la uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo katika Ununuzi ya Umma ni la msingi katika kupunguza gharama za ununuzi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia sheria mbili za Ununuzi wa Umma, yaani Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446) zilizoanza kutumika katikati ya mwaka wa fedha 2013/2014 na Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97 na 98) ambazo zilitumika hadi

katikati ya mwaka 2013/2014 na ambazo zimetenguliwa, kama inavyoelezewa kwa kina katika sura ya tano ya ripoti hii.

Baadhi ya mambo yaliyoripotiwa katika ukaguzi wa mwaka huu ni pamoja n:- Muundo usioridhisha wa Bodi za Zabuni katika Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Kitengo cha Ununuzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kutokutimiza wajibu wake, hivyo kupelekea mamlaka kuingia mkataba wenye utata wa Shilingi za Kitanzania bilioni 2.443 wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya ofisi ya Mamlaka hiyo na utoaji wa zabuni zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 4.412 bila kuthibitisha kama mzabuni anacho cheti cha mlipa kodi kinachotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kinyume na Kanuni ya 14 (1)(d) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97).

Pia, nilibaini ununuzi mkubwa uliofanywa nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka kama ifuatavyo:- Shilingi za Kitanzania 151,738,945 katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza, Shilingi za Kitanzania bilioni 12.4 katika Benki Kuu ya Tanzania na Shilingi za Kitanzania bilioni 45.7 katika Kampuni ya Simu Tanzania. Kutohakiki ubora wa bidhaa kabla ya kupokelewa na kuingizwa kwenye matumizi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kulikopelekea ununuzi ya gari lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania milioni 53.9 bila kuzingatia vigezo vilivyowekwa kinyume na Kanuni ya 244 na 245 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013. Kadhalika nilibaini muundo usio sahihi wa Kitengo cha Ununuzi katika Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania, suala lililopelekea Shirika kufanya ununuzi ya Shilingi za Kitanzania Milioni 971.152 bila ushirikishwaji wa Kitengo cha Ununuzi. Mfululizo wa kuidhinisha ununuzi kwa njia ya Zabuni Zuifu (Restricted Tendering) bila Bodi ya Zabuni kukutana, ulibainika wakati wa ukaguzi wa hesabu za Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.277 zilitumika kununulia bidhaa na huduma bila kupitia kwenye vikao vya kawaida vya Bodi ya Zabuni.

Pia, nilibaini ununuzi usio na ushindani wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 219.87 katika Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC) na Shilingi za Kitanzania Milioni 335.9 katika Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara Moshi kinyume na Kanuni ya 159 ya Sheria za Ununuzi ya Umma ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446). Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania nilibaini zabuni 8 zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 9.279 na EURO Milioni 5.879 ambazo hazikuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma na Kanuni zake.

Kwa upande wa usimamizi wa mikataba, nilibaini kasoro kadhaa ambapo katika Chuo Kikuu Mzumbe tawi la Mbeya, mkataba wenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.944 haukusimamiwa vizuri. Tatizo la

kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa mujibu wa mkataba lilijitokeza katika Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania ambapo mikataba yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 34.848 haikuweza kukamilika kwa wakati na hivyo kupelekea Shirika kulipa fidia ya Dola za Kimarekani milioni 2.106 na EURO 981,831. Pia, katika ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Kansa ya Ocean Road ilibainika kuwa ujenzi wa jengo la tiba lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.333 haujakamilika kwa wakati kwa mujibu wa mkataba.

**v. Usimamizi wa Mali**

Ucheleweshwaji katika kukamilisha miradi (Work In Progress) ulibainika katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yenye thamani ya zaidi ya Shilingi za Kitanzania bilioni 3.0. Ucheleweshwaji huo, ulionekana katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC), Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Arusha. Pia, mapungufu yalibainika katika usimamizi wa mafuta ambapo vitabu vya kusimamia matumizi ya magari (Log Books) vilikuwa aidha havijazwi kwa wakati ama havipo kabisa kama ilivyoelezewa kwa kina katika sura ya sita ya ripoti hii.

Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC) kililipa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 157.5 kwa Kampuni ya M/s Scan Tanzania kwa ajili ya vipuli vya matrekta kutoka mwezi Mei, 2012 ambapo vipuli vya kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 142.94 havijapokelewa mpaka tarehe ya ukaguzi. Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, na hasa Chuo Kikuu cha Dodoma hakikujumuisha mali zake katika vitabu vya hesabu. Chuo hicho hakikujumuisha kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 452.1 katika hesabu zake. Pia, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji ilinunua magari kupitia Wizara ya Miundo Mbinu toka mwaka 2010. Hata hivyo gari moja lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 106.7 halijapokelewa na Mamlaka hiyo mpaka wakati wa ukaguzi.

Shirika la Hifadhi za Taifa limeendelea kupata changamoto za kufa kwa wanyama kutokana na ajali za magari ambapo kulingana na ripoti ya usimamizi wa viumbe hai, jumla ya wanyama 107 walikufa kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha Julai 2013 na Machi 2014. Pia, tofauti kubwa ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.137 ilibainika baina ya taarifa za Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar na Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

**vi. Usimamizi wa Rasilimali Watu**

Mabadiliko makubwa yamefanyika kutokana na ripoti ya mwaka jana kuhusu usimamizi wa rasilimali watu, ingawa kuna maeneo ambayo bado yanahitaji maboresho. Ukaguzi umebaini ucheleweshwaji wa makato ya kisheria kwa

Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO) ambapo kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 10 ikiwa ni PAYE, SDL na michango ya Mifuko ya Pensheni zilikua hazijalipwa na Shirika hilo. Pia, ilibainika kuwa nafasi za Wakuu wa Idara katika Benki ya Wanawake hazikuwa zimepitishwa na Benki Kuu ya Tanzania. Hali kadhalika, mikataba ya wafanyakazi wa muda katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilikuwa imeisha muda wake wakati Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Katani Tanzania alikuwa akifanya kazi bila ya kuwa na mkataba wa kazi.

TANAPA ililipa mara mbili gharama za bima (Group Endowment Assurance Scheme) kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 957.807 kwa wakala aitwaye Inter Trade Express Ltd. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) ilipitisha muundo wa mshahara bila kupata kibali kutoka kwa Msajili wa Hazina wakati Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilionekana linakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Tanga haina mpango wa namna ya kurithishana madaraka.

**vii. Utawala Bora**

Kanuni za utawala bora huhakikisha kufikiwa kwa uwajibikaji, usawa na uwazi katika uendeshaji wa Taasisi. Utawala bora hutoa muundo wa uongozi ambao hufanya kazi kwa faida ya wote kwa kuzingatia kanuni za utawala bora na sheria zinazotawala Taasisi husika. Utawala bora pia, huhakikisha kuwa kazi na mahusiano baina ya Menejimenti ya Shirika, Bodi za Wakurugenzi, Kamati za Bodi za Wakurugenzi, Wanahisa na Wadau wengine yanafuatwa ipasavyo.

Ili Kamati za Ukaguzi ziweze kufanya kazi zake za usimamizi na kuwa na uhuru wa kiwango kikubwa katika kutoa maamuzi, baadhi ya wajumbe wake wanapaswa kuwa na taaluma ya uhasibu na mambo ya fedha. Hata hivyo, tulibaini kuwa baadhi ya Kamati za Ukaguzi hazikuwa na mjumbe mwenye taaluma ya Uhasibu au fedha. Taasisi hizi ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii (SSRA) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF).

Pia, nilibaini kuwa, kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Masoko Kariakoo kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yake, shughuli za Shirika hilo ziliwekwa chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, Halmashauri hiyo iliteua baraza la ushauri kuwa kama chombo cha usimamizi wa Shirika hilo kinyume na matakwa ya vifungu namba 5(2) na 5(3) vya Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo. Sheria inatamka kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye

atakayemteua Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wengine kuteuliwa na Waziri husika.

Nilibaini pia kuwa, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Bima (TIRA) yalianzisha kamati za ukaguzi za bodi kwa kufuata Sheria ya Fedha ya Umma wakati Mashirika mengine ya Umma yalitumia kanuni za utawala bora na hivyo kusababisha kuwepo kwa tofauti wa Kamati hizo ya kutokuwa na kiwango kimoja cha kutathmini Mashirika hayo. Kwa hoja hii, Msajili wa Hazina anapaswa kutoa mwongozo kwa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo juu ya njia nzuri ya uanzishaji wa Kamati za Ukaguzi ili kuondoa mkanganyiko wa aina hii. Ni muhimu kutambua kuwa katika taratibu za utawala bora, Kamati za Ukaguzi zinapaswa kuundwa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na wajumbe kutokaaa nje yaa Shirika ambao siyo watendaji wa kila siku wa Shirika.

Pia nilibaini kuwepo kwa wadhibiti wawili katika sekta ya hifadhi ya jamii kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya Udhibiti wa Mifuko ya Jamii ya mwaka 2008 ambapo pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pia ilipewa nguvu kuhusiana na udhibiti na usimamizi wa masuala ya fedha ya mifuko hii ikiwemo kudhibiti hifadhi ya fedha, kusimamia uwekezaji na maamuzi ya kiuwekezaji ambayo ndiyo majukumu makuu katika sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mikataba ya utendaji kazi kati ya Bodi za Wakurugenzi na Msajili wa Hazina ni muhimu katika kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa Bodi za Wakurugenzi. Nimebaini kuwa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Shirika la Tija la Taifa (NIP) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) hayakusaini mikataba hiyo kama ilivyotakiwa na waraka wa Msajili wa Hazina.

Pia, kama ilivyo katika ripoti zangu za nyuma, nimekuwa nikitoa taarifa kuhusu umuhimu wa kuteuliwa kwa wakati Bodi za Wakurugenzi mara baada ya Bodi zilizotangulia kuisha muda wake. Hata hivyo, katika kipindi hiki hakukuwa na mwitikio wa kutosha na kumekuwepo na kuchelewa kuteuliwa kwa Bodi zinapokwisha muda wake kama ilivyoonekana katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) na Kituo cha Elimu Kibaha (KEC). Hali hii, ina athari katika utendaji wa Mashirika haya katika kuyapa miongozo, utoaji wa maamuzi muhimu na ukamilishaji wa kaguzi za Shirika husika.

**viii. Hali ya Madeni ya Serikali Kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

Madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yameendelea kukua na kufikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.876 hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2014. Madeni haya yanajumuisha mikopo iliyokopeshwa Serikali

moja kwa moja, ile iliyotolewa kwa Mashirika ya Umma/Taasisi za Serikali kwa dhamana ya Serikali na michango ya wanachama ambayo haijawasilishwa kwenye mifuko husika. Kiasi hiki hakijumuishi Shilingi za Kitanzania Trilioni 7.1 ambazo Serikali inadaiwa na PSPF tangu mwaka 1999 kwa kuwalipa mafao wastaafu ambao hawakuwa wakichangia lakini kwa mujibu wa Sheria walitakiwa kulipwa mafao ya kustaafu.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya madeni haya hayalipwi kabisa na mengine yanalipwa kwa kasi ndogo sana. Pia, ilibainika kuwa baadhi ya madeni haya hayana mikataba ya mikopo wala dhamana ya Serikali.

Kutokulipwa kwa madeni haya kunaweza kuwa na madhara makubwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii kumudu kulipa madeni ya muda mfupi na mrefu ikiwemo uwezekano wa kushindwa kulipa mafao kwa wastaafu. Kwa upande mwingine, mzigo wa madeni haya kwa Serikali unaongezeka kwa kuwa madeni haya yana riba na adhabu za ucheleweshaji malipo, mzigo ambao Serikali isingekua nao kama madeni haya yangelipwa kwa wakati uliokubaliwa.

**ix. Matokeo ya Kaguzi Maalum**

Katika mwaka huu wa ukaguzi, kaguzi maalum tatu zilifanyika katika Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA) na Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL).

Ukaguzi maalum wa Bodi ya Pamba Tanzania ulibaini kuwa Bodi hiyo ilipata hasara ya Shilingi za Kitanzania Milioni 166.446 ikiwa ni kiasi kilicholipwa zaidi ya kiasi kilichokuwa kinastahili kulipwa kwa kampuni zinazonunua pamba. Ruzuku ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 68.731 hakikulipwa kwa wakulima wa pamba na kampuni ya S & G wakati fedha hizo zilikuwa zimekwisha kulipwa kwa kampuni hiyo na Bodi ya Pamba. Kampuni za Badugu Ginning Company Ltd na Vearrian (T) zilifunga na kusitisha biashara ya ununuzi wa pamba kabla ya kuwalipa wakulima wa pamba stahili zao za ruzuku ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania 105,823,760. Ilibainiki pia kuwa, kiasi cha ruzuku ya Shilingi za Kitanzania 104,680,350 hakikulipwa kwa wakulima wa pamba kutokana na kupoteza stakabadhi za mauzo ya pamba na kukosa vielelezo vya kulipwa ruzuku hiyo. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha bado hakijareshwa Hazina na Bodi ya Pamba Tanzania.

Katika ukaguzi maalumu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA), nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 554.6 kilitumika kununua mita za maji lakini haikujulikana idadi ya mita zilizonunuliwa kwa fedha hizo. Mamlaka bado haijaweza kuwafungia mita za maji wateja 2399 wanaopata huduma ya maji kutoka kwa Mamlaka hiyo. Pia, Mamlaka ilitumia kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 724. 1 bila kuzingatia

Kanuni za Fedha za Mamlaka. Kwa upande mwingine watumishi 30 waliajiriwa na Mamlaka hiyo bila ya kutangaza nafasi hizo kinyume na utaratibu wa ajira wa Mamlaka; ilibainika pia kuwa, watumishi watano walioajiriwa na Mamlaka walipewa mishahara mikubwa ambayo haikuendena na nafasi zao kinyume na ikama ya Mamlaka.

Ukaguzi maalumu wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), ulibaini kuwa Menejimenti ya kampuni iligundua vihatarishi (risks) lakini haikuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kukabiliana na vihatarishi hivyo. Nilibaini pia kuwepo kwa uangalizi mbovu kutoka kwa Menejimenti ya kampuni kwenye maandalizi ya mishahara ambapo mtumishi mmoja aliweza kuiba kwa kujizidishia mshahara wake kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 71.77. Kiasi hicho kiliingia kwenye akaunti yake ya benki zaidi ya mshahara wake wa kawaida. Sheria ya Ununuzi wa Umma haikuzingatiwa vyema katika ununuzi wa Bajaji 30 zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 156 na ununuzi wa magari 10 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.254. Kampuni ya simu Tanzania (TTCL) haikuweza kudhibiti vizuri matumizi ya mafuta ya magari hali iliyopelekea kampuni hiyo kupata hasara ya Shilingi za Kitanzania Milioni 73.97.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

## 1.0 Uanzishwaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ofisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama inavyorekebishwa mara kwa mara). Ukaguzi wa Umma Tanzania umeelezewa zaidi kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 pamoja na kifungu cha 44 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na baadae kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011.

Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma angalau mara moja kwa mwaka. Vilevile, kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mtu yeyote ama afisa yeyote kukagua kwa niaba yake vitabu vya hesabu za Mashirika na Taasisi yoyote ya Umma ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anapaswa kukagua kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, jukumu la kutoa hati ya ukaguzi linabaki kuwa la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nchini zinafanya kazi kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

## 1.1 Ukaguzi na Mamlaka ya Kuripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

### 1.1.1 Mamlaka ya Ukaguzi

Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma umeelezewa katika Ibara ya 143(2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya ibara hii ya Katiba yameelezewa zaidi katika Kifungu Na. 34 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambayo inasema “baada ya kupokea mahesabu kwa ajili ya ukaguzi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ndiye atakayehakikisha kuwa ukaguzi unafanyika na ndani ya kipindi cha miezi tisa baada ya mwaka

wa fedha kuisha inabidi atoe taarifa kuhusiana na hesabu pamoja na matokeo ya ukaguzi".

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyinginezo katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:-

- Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija;
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Umma;
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu na rushwa katika rasilimali za Umma;
- Kuongeza manufaa, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

### 1.1.2 Mamlaka ya Kuripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo tamkwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo au kabla ya tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawaelekeza wahusika kuwasilisha ripoti hizo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge ambacho kitafanyika baada ya Rais kupokea ripoti hiyo (zo). Ripoti hizo zinatakiwa ziwasilishwe Bungeni ndani ya siku saba tangu kuanza kwa kikao hicho cha Bunge.

Kama Rais hatachukuwa hatua zozote za kuwasilisha ripoti hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti hizo kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma itajadiliwa kwanza na Kamati za Bunge za Hesabu (PAC) kwa niaba ya Bunge na kuandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

## 1.2 Wigo na Matumizi ya Viwango vya Ukaguzi

### 1.2.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihasibu na udhibiti wa ndani katika shughuli za taasisi husika, ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji na mbinu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi huu unafanyika kwa kuzingatia viashiria hatarishi na umuhimu wa miamala katika maamuzi "risk and materiality". Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatokana na kiwango cha kumbukumbu, nyaraka na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na kuwasilishwa kwangu.

Nia na madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutimiza jukumu la kutoa hati ya ukaguzi iliyo huru kwenye hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2013/2014 kama zimeandaliwa kutokana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zinazokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Septemba, 2013, tarehe 31 Disemba, 2013 na tarehe 30 Juni, 2014. Pia, ripoti hii inajumuisha mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti za ukaguzi za miaka iliyopita ambayo hayajatekelezwa na mambo muhimu yaliyokuwa kwenye ripoti za Mashirika husika ambayo kwa sababu mbalimbali hayakuandikwa kwenye ripoti ya mwaka uliopita.

### 1.2.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za nchi za Afrika (AFROSAI) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa nchi za Afrika zinazoongea lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo, ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAIs) vinavyotolewa na "INTOSAI" na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu Duniani (IFAC).

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina majukumu ya kipekee ya kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi, uwajibikaji na uwazi katika nchi. Pia, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania ina jukumu la kutoa ripoti iliyo bora na kwa wakati unaofaa inayoelezea namna rasilimali za Taifa zilivyokusanywa na kutumika.

## 1.3 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinalo jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha:-

- Kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa ikiwa ni pamoja na kuweka, kutekeleza na kudumisha mifumo ya udhibiti wa ndani itakayowezesha kuandaa hesabu zilizo huru na yasizo na makosa au mapungufu yatokanayo na udanganyifu;
- Kuchagua na kutumia sera sahihi za uandaaji wa mahesabu na
- Kufanya makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi.

Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi husika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu (IAS 1) na Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS 1) vinaainisha aina za taarifa za hesabu zinazotakiwa kuandaliwa. Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma Tanzania zinatakiwa kuandaa hesabu kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSASs) kutokana na aina/asili ya shughuli na madhumuni ya Mashirika na Taasisi husika. Hii inatokana na maamuzi yaliyochukuliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) yaliyopitishwa na Serikali ya kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma Tanzania zinatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu na ukaguzi na utafanyika kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na itaongozwa na viwango na miongozo inayotolewa mara kwa mara na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).

Ripoti ya mwaka ya Mashirika Taasisi Nyinginezo za Umma inatoa taarifa ambazo zinasaidia Umma kutathmini ustawi wa mashirika na uwajibikaji wa Watendaji Wakuu katika kutumia rasilimali za Taifa. Kwa hali hiyo, kupata taarifa kwa wakati muafaka kisheria ni kitu muhimu. Hii ndiyo dhima nzima ya uwazi na uwajibikaji katika kutumia rasilimali za Umma.

## 1.4 Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Udhibiti wa ndani ni utaratibu unaowekwa na uongozi wa Taasisi husika kwa lengo la kuhakikisha kuwa utendaji unafikia malengo yafuatayo:

- Ufanisi katika matumizi ya rasilimali za shirika,
- Ubora wa taarifa za kifedha,
- Utii wa sheria na miongozo mbalimbali inayohusika.

Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kuhakikisha kuwa ufanisi katika uendeshaji na kudhibiti, ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za Umma zinazoshikika na zisizoshikika. Kwa taasisi yoyote lengo la mfumo wa udhibiti wa ndani ni kuhakikisha shughuli za taasisi husika zinafanywa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Tukiongelea malipo na ununuzi, udhibiti wa ndani una maana ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia malengo mbalimbali yaliyowekwa, mfano; namna ya kuhakikisha kuwa malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma na mali za shirika ni halali.

## 1.5 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Kifungu Na. 8 na 11 cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Sura ya 370 iliyorekebishwa mwaka 2002) na sehemu ya tano ya Sheria ya Mashirika ya Umma (Sura ya 257 iliyorekebishwa mwaka 2002) kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.2 ya 2010 , zinahusiana na majukumu ya Msajili wa Hazina katika Mashirika ya Umma. Sheria hizo zinaelezea kuwa, Msajili wa Hazina ana kazi na jukumu la kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika. Vyombo hivi viwili vinafanya hivyo kwa ukaribu katika kusimamia na kuongoza Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ufanisi kwa kutoa maelekezo na kuyasimamia.

## 1.6 Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu Na. 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, kinayataka Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ndani ya miezi mitatu baada ya kuisha mwaka wa fedha unaohusu hesabu hizo.

## 1.7 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa kazi ya Ukaguzi

Ili ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, ninatumia mamlaka yangu ya kikatiba kuteua makampuni binafsi ya ukaguzi kukagua Mashirika

Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba yangu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, ambacho kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumteua mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya mwaka 1972 (iliyorekebishwa mwaka 1995) kufanya ukaguzi kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba yake.

Wakaguzi nitakaowateuwa watafuata sheria kama inavyotakiwa na kuwaa hawana mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza wajibu wao na pia hawatatoa siri za Mashirika wanayoyakagua. Wajibu wa kutoa hati za ukaguzi ni wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi zitakazofanywa na Makampuni binafsi zitahakikiwa ubora wa kazi zake na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014; kati ya Mashirika 180, Mashirika 6 (3%) yalikaguliwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, na Mashirika 37 (21%) yalikaguliwa na wakaguzi wa ofisi yangu kwa kushirikiana na wakaguzi wa makampuni binafsi na Mashirika 137 (76%) yalikaguliwa na makampuni binafsi peke yao kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.1.

**Kielelezo namba 1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka 2013/2014**



Idadi ndogo ya Mashirika ya Umma ya asilimia 3% yanayokaguliwa na ofisi yangu ni ishara ya upungufu wa wafanyakazi katika ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ofisi yangu inahitaji wafanyakazi wa kutosha na wenye ujuzi ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali ninazokumbana nazo katika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Katika mwaka wa fedha 2013/2014 ofisi yangu imetoa zabuni kwa Makampuni binafsi ya Ukaguzi 56. Majina ya makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyofanya kazi ya ukaguzi kwa niaba ya ofisi yangu yameorodheshwa kwenye kiambatisho cha I cha ripoti hii.

# SURA YA PILI

# AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

## 2.0 Utangulizi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Na.200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Taasisi na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika, na kumfanya mtumiaji kupata uhakika ya kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na anaweza kuzitumia kwa maamuzi mbalimbali.

Ripoti hii ya mwaka inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zipatazo 180 ambazo mwaka wake wa fedha uliishia tarehe 30 Septemba 2013, 31 Disemba 2013 na 30 Juni 2014. Kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 hesabu za Mashirika 177 kati ya 180 ziliwasilishwa kwenye ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa. Mashirika matatu (3) ambayo ni Shirika la Reli Tanzania (TRL), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Kampuni ya Huduma za Majini (Marine Services Company) hayakuwasilisha hesabu zake.

Katika hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, kaguzi 125 zilihitimishwa na ripoti zake kutolewa kwa mashirika husika hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2015. Kati ya kaguzi zilizohitimishwa, ripoti za kaguzi za Mashirika 109 ziliridhiwa na Bodi za Wakurugenzi na hati za ukaguzi kutolewa, wakati mashirika 16 hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi kuidhinisha hesabu hizo. Kaguzi 52 zilizobaki zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, Mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za Wakurugenzi kwa wakati na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati. Hali halisi ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hadi kufikia tarehe 17 Machi, 2015 ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. II cha ripoti hii.

## 2.1 Aina za Hati za Kaguzi zilizotolewa

### 2.1.1 Hati Inayoridhisha (Unqualified Opinion)

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika. Kwa mwaka huu ninaoripoti, kaguzi 105 za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilipata hati inayoridhisha.

### 2.1.2 Hati Yenye Shaka (Qualified Opinion)

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na Menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla wake zimeandaliwa vizuri isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa. Kwa mwaka huu ninaoripoti, kaguzi nne (4) za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilipata hati yenye shaka.

### 2.1.3 Hati Mbaya (Disclaimer of Opinion)

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa hati ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo. Hata hivyo, kwa mwaka huu hakuna hati mbaya iliyotolewa kwa shirika lolote.

### 2.1.4 Hati Isiyoridhisha (Adverse Opinion)

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa taarifa za fedha za Shirika au Taasisi Nyinginezo za Umma kwa kiasi kikubwa zimeandaliwa bila kufuata miongozo inayotolewa na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, sheria na kanununi husika. Kimsingi hati hii hueleza kwamba, taarifa zilizomo katika hesabu za Shirika au Taasisi kwa kiasi kikubwa si sahihi wala za kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya Shirika au Taasisi husika. Hakuna hati isiyoridhisha iliyotolewa kwa shirika lolote kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Uchanganuzi wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka 2013/2014 unapatikana kwenye kiambatisho cha III na mgawanyo wake umeainishwa kwenye kielelezo Na.2.

**Kielelezo namba 2: Kinaonyesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014**




**Kumbuka**: Kwa mwaka wa huu wa mapitio hati mbaya na hati isiyoridhisha hazikutolewa

Mchanganuo wa Hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo kutoka mwaka 2009/2010 hadi 2013/2014 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali 1: Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa**

| Mwaka | Aina ya Hati | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Hati zinazoridhisha | Hati zenye Shaka | Hati Mbaya | Hati Zisizoridhisha | Jumla |
| 2013/2014 | 105 | 4 | 0 | 0 | **109** |
| % | 96 | 4 | 0 | 0 | **100** |
| 2012/2013 | 92 | 1 | 0 | 0 | **93** |
| % | 99 | 1 | 0 | 0 | **100** |
| 2011/2012 | 85 | 9 | 1 | 0 | **95** |
| % | 90 | 9 | 1 | 0 | **100** |
| 2011/2010 | 96 | 11 | 0 | 0 | **107** |
| % | 90 | 10 | 0 | 0 | **100** |
| 2009/2010 | 104 | 17 | 1 | 0 | **122** |
| % | 85 | 14 | 1 | 0 | **100** |

Kwa ufafanuzi zaidi, mwelekeo wa hati za ukaguzi umefafanuliwa katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo namba 3:Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi**




Mwelekeo wa hati za ukaguzi katika suala la idadi na aina zinazotolewa zimekuwa zikibadilika kutoka kipindi kimoja hadi kingine kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la 1. Hali hii inaashiria kuwa, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yameshindwa kuwa na mwenendo thabiti katika kuzingatia mifumo ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu na uwepo wa dosari na makosa katika taarifa hizo za fedha.

## 2.2 Misingi ya Hati Zilizotolewa

### 2.2.1 Ripoti Zenye Hati Inayoridhisha

Kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 1, hati 105 zinazoridhisha zilitolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kati ya hati hizo, hati 39 zilitolewa zikiwa na aya zenye masuala ya msisitizo kwenye ripoti ya ukaguzi. Aya hizi zilitolewa ili kuweka msisitizo juu ya masuala fulani yaliyoonekana ili kuwawezesha watumiaji wa taarifa za fedha kuyapa uzito wakati wa kufanya maamuzi. Hali hii itasaidia Menejimenti husika za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kuchukua hatua madhubuti pindi shughuli na huduma za Taasisi hizo zinapoweza kuwa mashakani.

Hali ya kuwa mashakani kihuduma kulifanywa sambamba na kufanya tathmini ya matukio yoyote au vitu ambavyo vinaweza kuleta shaka ama wasiwasi juu ya kuweza kuendelea na shughuli zake kwa Mashirika na Taasisi Nyiginezo za Umma. Tulibaini kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuwa na mwenendo usioridhisha wa hali ya kifedha kutokana na hasara zilizojitokeza kwa

miaka zaidi ya miwili mfululizo. Hali hii ilipelekea Mashirika haya yashindwe kulipa madeni yake ya muda mfupi. Hali hii imesababisha kuwa na uwiano wa mali na madeni ambao si mzuri ikilinganishwa na ule unaokubalika wa uwiano wa kihasibu wa 2:1 yaani uwezo wa kifedhaa uzidi madeni kwa mara mbili.

Msisitizo au umakini pia umetolewa kwenye Mashirika ya Umma ambayo yalikuwa na madeni tarajiwa (contingent liabilities) kutokana na uwepo wa mashauri mbalimbali katika hatua mbalimbali za maamuzi ambayo matokeo yake hayajajulikani yatakuwaje na hakuna kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kukabiliana na madeni hayo kwenye taarifa za fedha. Aya yenye Suala la Msisitizo ilijumuishwa kwenye ripoti ya Mkaguzi ili kusisitiza juu ya viashiria hivyo kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili waweze kufanya maamuzi sahihi ya kiuchumi huku wakiwa na taarifa za awali kuhusiana na madeni tarajiwa. Kiasi cha fedha ambacho kinahusishwa na madeni tarajiwa ni Shilingi za Kitanzania bilioni 52.36 na Dola za Kimarekani milioni 258.761 kama ilivyoainishwa kwenye kiambatisho cha IV.

Mashirika ya Umma ambayo yamekuwa na mwenendo usio mzuri wa hali ya kifedha uliochangiwa na hasara mfululizo na matatizo ya ukwasi ambayo Serikali inahitaji kuingilia kati yamekuwa hayana unafuu wowote wa mabadiliko kama nilivyoyatolea taarifa kwenye ripoti yangu iliyopita. Mchanganuo unaoonyesha hasara, upungufu na matatizo ya kifedha umeonyeshwa kwenye kiambatisho cha IV.

### 2.2.2 Hesabu zenye Hati yenye Mashaka

Kwa kipindi hiki cha mwaka ninaoripoti nimetoa hati zenye mashaka kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zipatazo nne (4) ambazo ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Chalinze. Hati yenye mashaka ilitolewa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa misingi kwamba kulikuwa na majengo yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 452.1 ambazo hazikujumuishwa kwenye taarifa za fedha za Chuo hicho.

Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu vinataka mali kutambuliwa kutokana na namna inavyonufaisha Taasisi husika kuliko umiliki wake kisheria. Chuo kikuu cha Dodoma kinagharamia utunzaji na ukarabati na pia kinanufaika na faida zote zitokanazo na majengo hayo ikiwa ni pamoja na mapato hali inayopelekea kuwa na sifa za kujumuishwa kwenye taarifa za fedha za Chuo hicho. Kwa hali hiyo Chuo Kikuu cha Dodoma hakikufuata Viwango vya Kimataifa vya

Uandaaji wa Hesabu Na. 16 aya ya 7 ambayo inasema kuwa gharama za Majengo, Mitambo na vifaa vitajumuishwa kama mali za Taasisi endapo itathibitika kwamba kuna uhakika wa faida zinazohusiana na mali hizo kuinufaisha taasisi husika.

Hati nyingine yenye shaka ilitolewa kwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same kutokana na idadi kubwa ya wateja wa maji ambao hawakupelekewa ankara. Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia stakabadhi 6,189 za malipo kwa wastani wa wateja 516 waliopewa ankara za maji kila mwezi umeonyesha kuwa mamlaka ilikusanya Shilingi za Kitanzania Milioni 164. 1 kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014. Hata hivyo, idadi ya wateja waliothibitishwa na mamlaka kuwepo ni wateja 1,200 hali iliyopelekea tofauti ya wateja 684 kutopewa ankara za kulipia maji. Wateja ambao hawakupewa ankara za maji wanakadiriwa kuiingizia Mamlaka hasara ya Shilingi za Kitanzania milioni 217 kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2014.

Zaidi ya hayo, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania ulipata hati yenye shaka kutokana na Majengo, Mitambo na Vifaa vilivyoripotiwa vya kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.385 bila ya kufanyiwa tathmini kwa zaidi ya miaka mitano ikiwa ni kinyume na matakwa ya aya Na.31 na 34 za Kiwango Na.16 cha Kimataifa cha Uandaaji wa Hesabu. Vile vile, taarifa za fedha za Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Chalinze zilipata hati yenye shaka kutokana na kutotenganisha thamani ya Ardhi na Majengo kama inavyotakiwa na aya Na. 58 ya kiwango Na. 16 cha Kimataifa cha uaandaaji wa hesabu, na hivyo Ardhi na Majengo viliripotiwa kwa pamoja kwa thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 8.68.

# SURA YA TATU

## MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inaonyesha kwa muhtasari mapendekezo ya ukaguzi wa ripoti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa miaka iliyopita, ambayo bado hayajatekelezwa. Mapendekezo hayo yapo aidha kwenye hatua za utekelezaji au hayakutekelezwa kabisa hadi ilipofikia wakati wa kuandaa ripoti hii. Malengo ya mapendekezo ya ukaguzi ni kuimarisha uwajibikaji na utawala bora. Iwapo hapatakuwa na jitihada binafsi kutoka kwenye Shirika la Umma husika kutekeleza mapendekezo ambayo hayajatekelezwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na utawala bora halitafanikiwa.

### 3.1 Majibu ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita (2012/2013)

Nimepokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita kupitia barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu Na. C/DE.85/229/01/72 ya tarehe 30 Agosti, 2014. Napenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa majibu aliyotoa kuhusu mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Pamoja na juhudi hizo, mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa. Kwa hali hiyo, malengo na madhumuni ambayo Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamejiwekea hayatafikiwa kama hatua za ziada hazitachukuliwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyokwishatolewa.

Ninapenda kuifahamisha Serikali kwamba, mapendekezo ninayoyatoa mara kwa mara yana lengo la kuhakikisha kunakuwa na hatua madhubuti na umakini katika kuimarisha ukusanyaji na utumiaji wa mapato na rasilimali za Taifa. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakikisha matumizi ya fedha za Umma yanaidhinishwa na wenye mamlaka na fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa hali hiyo, kwa kuzingatia sheria na kanuni katika kutumia rasilimali za Taifa; thamani ya fedha, tija na ufanisi vyaweza kufikiwa.

Kwa misingi hiyo ninaona ni vyema kuyarudia tena mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma. Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti ya mwaka jana yanaonekana kwenye Jedwali Na. 2.

**Jedwali 2: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti ya mwaka 2012/2013**

| Hali ya Utekelizaji | Idadi ya Mapendekezo | | | | | | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | Jumla | |
| Yametekelezwa | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 6 |
| Utekelezaji Unaendelea | 4 | 2 | 1 | 5 | 4 | 16 | 52 |
| Hayajatekelezwa | 0 | 0 | 1 | 3 | 8 | 12 | 39 |
| Yamepitwa na Wakati | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 |
| **Jumla** | **4** | **2** | **3** | **8** | **14** | **31** | **100** |

## 3.2 Mapendekezo ya Mwaka 2008/2009 Ambayo Bado Hayajatekelezwa

### 3.2.1 Mikataba ya Uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi

Serikali inapaswa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ili kuwekeana malengo wanayotakiwa kufikia kwa kipindi chao cha kazi na yawekwe wazi.

Ingawa Mlipaji Mkuu wa Serikali ametoa majibu, lakini mpango wa Serikali wa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ishirini (20) haitoshelezi. Serikali inashauriwa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zote zilizobaki ili kuwe na usawa.

### 3.2.2 Haja ya Kuanzishwa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji

Ni dhahiri kwamba Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa ni ukosefu wa mitaji ya kutosha ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mashirika hayo. Serikali inapaswa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi. Nasisitiza Serikali iongeze juhudi katika uanzishwaji wa Mfuko huu wa Umma wa Uwekezaji kulingana na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

### 3.2.3 Kutokuwepo kwa Usawa Katika Marupurupu Yatolewayo na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Kuna umuhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa kuna uwiano katika marupurupu wanayopata Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi za

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, kutokana na ukweli kwamba rasilimali wanazotumia (kama posho za vikao, ada za Bodi za Wakurugenzi n.k.) ni rasilimali za Umma. Hii itasaidia kuondoa tofauti zilizopo, sasa kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali tumeyatambua juu ya uanzishwaji wa Bodi ya Uwiano wa Mishahara na Marupurupu.

### 3.2.4 Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 54.6 kwa Bodi ya Mikopo na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1

Mikopo ambayo Taasisi za Serikali zimekopa kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo imedhaminiwa na Serikali inachukua muda mrefu kulipwa huku Serikali ikiwa imekaa kimya. Pamoja na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, hadi kukamilika kwa uandikaji wa ripoti hii, mkopo wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu bado haujarejeshwa. Ningependa kusisitiza kuwa Serikali ichukue hatua kuhakikisha kwamba bakaa la deni lote la mkopo (ikiwa ni kiasi cha mkopo na riba) linarejeshwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mkopo huo.

Kuhusu kutotorejeshwa kwa mkopo uliokopwa na wanafunzi wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 51.1, Bodi ya Mikopo inashauriwa kuchukua hatua za kisheria kwa waajiri na wakopaji binafsi ambao hawatoi ushirikiano kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Na. 9 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004.

## 3.3 Mapendekezo ya Mwaka 2009/2010 ambayo Hayajatekelezwa

### 3.3.1 Mgongano wa Kimaslahi kwa Wabunge Kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Bunge ndicho chombo cha juu kinachowakilisha wananchi na chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi wa Serikali ikiwa ni pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kupitia Kamati za Kudumu za Bunge. Ili kuepuka mgongano wa kimaslahi, nasisitizia mapendekezo yangu kuwa, Wabunge hawastahili kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwani wana jukumu la kusimamia Mashirika hayo.

### 3.3.2 Kuongezewa Mtaji kwa Mashirika ya Umma yenye Mtaji Mdogo

Msajili wa Hazina (Mmiliki) anashauriwa kuhakikisha kuwa Mashirika ya Umma yenye mchango mkubwa kiuchumi ambayo hayana mitaji ya kutosha, yanapatiwa fedha za mtaji kwa ajili ya kujiendesha. Suala hili linaweza kufanyika kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato

vitakavyoyawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa Umma. Kama alivyojibu Mlipaji Mkuu, nasisitiza kuwa Serikali ianzishe mchakato wa uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma bila kukawia.

## 3.4 Mapendekezo ya Mwaka 2010/2011 ambayo Hayajatekelezwa

### 3.4.1 Usimamizi wa Rasilimali

Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) yalitumia jumla ya Shilingi bilioni 415.4 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, endesha na kisha hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya mifuko ya hifadhi ya jamii. Japokuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali amejibu kuwa majengo haya yataingizwa kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma mwaka wa fedha wa 2013/2014, bado Chuo kimeendelea kupata hati yenye Mashaka kutokana na kutokuwepo kwa majengo hayo kwenye vitabu vyake.

### 3.4.2 Uhakika wa Vyanzo vya Fedha za Uwekezaji

Nasisitizia mapendekezo yangu ya kwenye ripoti zilizopita kuwa kuna haja ya Serikali kupitisha sheria ya kuyataka Mashirika muhimu kiuchumi kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es Salaam. Mfano wa Mashirika hayo ni Kampuni za Madini, Kampuni za Simu, Kampuni za Saruji na Kampuni za Vinywaji.

## 3.5 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2011/2012

### 3.5.1 Ununuzi ya Dharura Ambayo Hayakupata Kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali

Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ilifanya ununuzi ya dharura yenye thamani ya Dola za Kimarekani 810,000 na Euro milioni 13.915 bila idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hali kadhalika ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Mzumbe kilifanya ununuzi ya dharura yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.987 kwenye ujenzi wa jengo la ghorofa tano katika kampasi ya Dar es Salaam bila idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Suala la Chuo Kikuu cha Mzumbe linachunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Sina taarifa ya hatua zilizochukuliwa kuhusiana na suala la Mamlaka ya Bandari Tanzania.

### 3.5.2 Matatizo ya Kifedha Katika Shirika la Utangazaji la Tanzania

Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) limeripotiwa kuwa na hasara kwa miaka mingi mfululizo. Shirika hili lina matatizo ya ukwasi na linaitegemea Serikali kwa kiasi kikubwa katika mahitaji yake ili kujiendesha na kulipia madeni mbalimbali. Hali hii inaleta mashaka na endapo itaendelea kwa kipindi kirefu shirika linaweza kushindwa kujiendesha. Nashauri Serikali iongeze mchango wa kibajeti kwa Shirika hili wakati mpango mkakati wa miaka mitano unaanza kutekelezwa kama ilivoelezwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

### 3.5.3 Kuongezeka Matukio ya Uwindaji Haramu Katika Hifadhi za Taifa Tanzania

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uwindaji haramu katika hifadhi ambazo zipo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa hususani mauaji ya Tembo. Napenda kutambua mikakati inayotekelezwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuzuia na kupambana na shughuli za uwindaji haramu kama kuongezwa kwa askari wa wanyama pori, kushirikisha vikosi vya askari polisi, kuimarisha idara ya upelelezi ya wanyamapori, kuboresha zana za vitendea kazi na hatua nyinginezo. Kwa sasa ujangili ni janga la kitaifa na kimataifa ambapo kama lisipodhibitiwa kwa miaka ya hivi karibuni litahatarisha uhai wa wanyamapori Tanzania. Nashauri nguvu kubwa iongezwe kwenye utoaji wa elimu kwa jamii ili wanajamii wanaozunguka hifadhi hizi watambue umuhimu wa uhifadhi.

### 3.5.4 Kontena Mbili za Vitabu vya Maktaba Kutoka Shirika la Kimataifa la Kufadhili Watoto Hazijatolewa Bandari ya Dar es Salaam Tangu Mwaka 2009

Katika ripoti yangu ya mwaka jana nilitoa taarifa kuwa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imeshindwa kutoa mzigo wa vitabu katika Bandari ya Dar es Salaam tangu mwaka 2009. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2013/2014 vitabu hivyo vilikuwa bado havijatolewa bandarini vikisubiri malipo ya kodi na gharama za kuhifadhi mizigo ambayo imefikia kiasi cha shilingi milioni 147. Nashauri Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania iishirikishe Serikali katika kutatua suala hili mapema ili vitabu hivi visipitwe zaidi na wakati au kuharibika.

### 3.5.5 Malipo ya Leseni ya Biashara Yaliyolipwa na TBC kwa TCRA Kwa Niaba ya Star Media

Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lililipa kiasi cha shilingi milioni 618.3 kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa niaba ya Kampuni ya Star Media (T) Limited (Star Times) katika mwaka 2009/2010 kwa ajili ya leseni ya biashara. Hata hivyo, Star Media (T)

Limited ina mkataba wa utendaji uliosainiwa na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) ambapo Star Media (T) Limited imepewa msamaha wa kulipa ada ya leseni ya biashara kwa kipindi cha miaka kumi (10), hivyo kusababisha malipo ya awali ya leseni ya biashara yaliyolipwa na TBC kwa TCRA kutotambuliwa kama mtaji wa hisa za TBC katika Kampuni ya Star Media (T). Mpaka wakati wa kuandika ripoti hii bado suala la fedha zilizolipwa na Shirika la Utangazaji Tanzania kwa niaba ya Star Media (T) Limited halikuwa limepata ufumbuzi. Nashauri Shirika la Utangazaji Tanzania likishirikiana na Taasisi nyingine za Serikali watatue mgogoro huu.

### 3.5.6 Majengo ya NDC Kwenye Kitalu Na.2338 yaliyopo Mbezi Beach, Barabara ya Bagamoyo Hayana Mkataba wa Pango

Nilibaini kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa halina mkataba wa pango na mpangaji wa sasa wa jengo hilo, Messrs Vignan Education Foundation (IMTU) baada ya mkataba na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) kuisha mwezi Agosti, 2011. Vignan Education Foundation amekataa kukubali masharti ya mkataba ulioandaliwa na NDC ambao pamoja na mambo mengine una kodi ya mwezi ya shilingi milioni 60, ambayo ilikadiriwa na mthamini (valuer). Kwa mujibu wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, Shirika la Maendeleo la Taifa limefungua kesi mahakamani. Nashauri NDC iendelee kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa kesi hii.

### 3.5.7 Nyumba ya Bodi ya Sukari Tanzania Anayoishi Waziri wa Zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika

Nilibaini kuwa Bodi ya Sukari Tanzania ina nyumba kwenye kiwanja Na. 482 iliyopo katika barabara ya Bray Masaki. Kwa muda mrefu nyumba hiyo amekuwa akiishi Waziri wa zamani wa Kilimo, Hifadhi ya Chakula na Ushirika. Kama alivyojibu Mlipaji Mkuu wa Serikali, ninashauri Serikali ifanye jitihada za kutatua suala hili kwa wakati.

### 3.5.8 Usafiri Dar es Salaam (UDA)

#### a) Uuzwaji wa Hisa za UDA

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) iliuza hisa za Shirika hilo bila kupata kibali cha Serikali. Hisa za Shirika la UDA zilithaminishwa kwa bei ya shilingi za Kitanzania 744.79 kwa kila hisa mwezi Oktoba, 2009 na mwezi Novemba, 2010 thamani ya kila hisa ikawa Shilingi za Kitanzania 656.15. Hata hivyo, katika uuzaji huo, Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ilitoa punguzo la asilimia 60 kwa kila hisa kwa mwekezaji huyo (kwa tathimini ya bei ya hisa ya mwezi Oktoba, 2009), bila kuwepo na sababu za kufanya hivyo. Kwa mujibu wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, Serikali haitambui uuzwaji wa hisa hizo. Zaidi, Serikali inaandaa mapendekezo ya kuuza asilimia 49

ya hisa za UDA na kufikishwa mbele ya Baraza la Mawaziri. Majibu haya hayasemi chochote kuhusu mustakabali wa hisa ambazo zilishauzwa na hatua zilizochukuliwa dhidi ya Bodi ya Wakurugenzi wa UDA.

**b) Kuthibitishwa Kiasi Kilicholipwa na Mnunuzi**

Mkataba wa kuwasilisha hisa wa tarehe 11 Februari, 2011 unaeleza kwamba mnunuzi (mwekezaji) atalipa jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.143 kama bei ya ununuzi ya hisa zote ambazo hazijagawiwa na UDA ingawa mkataba haukuonyesha akaunti ya benki ambayo malipo yangefanyika. Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 285 katika akaunti namba 0J1021393700 ya benki ya CRDB inayomilikiwa na UDA. Kulikuwa hakuna malipo mengine ya ziada yaliyofanywa na mwekezaji kuhusiana na ununuzi wa hisa za UDA. Malipo haya ni sawa na asilimia 24.9 ya bei ya kuuza iliyokubaliwa. Mwekezaji alidai kumlipa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya UDA kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 320 na kuziingiza kama ada ya kukubali kununua UDA mwaka 2009. Mwenyekiti wa Bodi alikubali kupokea kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 320 katika akaunti yake binafsi kutoka kwa Mwekezaji ikiwa kama ada ya ushauri alioutoa kwa Mwekezaji, hali inayopelekea kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi. Ninashauri Serikali ichukue hatua za kisheria dhidi ya Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya UDA. Kwa kuwa Serikali haitambui uuzwaji wa hisa za UDA, ninashauri Shirika la UDA lirudishwe chini ya usimamizi wa Serikali.

## 3.6 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2012/2013

### 3.6.1 Msaada wa Dola za Kimarekani 300,000 Kutoka Jamhuri ya watu wa China Haukuwa Kwenye Vitabu vya Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ilipokea msaada wa fedha wa Dola za Kimarekani 300,000 tarehe 24 Septemba, 2012. Msaada huu ulijumuisha vitabu 1000, kompyuta na samani 20. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikuonyeshwa kwenye vitabu vya hesabu za Maktaba hivyo kushusha kiasi cha rasilimali kwenye vitabu vya Maktaba kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 300,000. Nashauri Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ijumuishe msaada huu kwenye vitabu vyao.

### 3.6.2 Mita za Kupima Mafuta Zilizotelekezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua mita nane kwa ajili ya kudhibiti upimaji wa shehena za mafuta yanayoingia nchini. Mita hizo ziliwekwa

tayari kwa matumizi kwenye bandari za Tanga na Dar es Salaam kwa ajili ya kusaidia kudhibiti mapato yanayopotea kutokana na kutokuwa na vifaa vizuri vya kupimia shehena za mafuta zinazoingia nchini. Vifaa hivyo vilinunuliwa na kuwekwa kwenye bandari hizo baada ya serikali kuagiza ununuzi wake kwa ajili ya kupata vipimo sahihi na hatimaye kutoza viwango sahihi vya kodi. Hata hivyo, mita hizo zimetelekezwa kwa miaka kadhaa sasa. Sababu iliyotolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa vipimo ni kwamba vifaa hivyo havikidhi viwango vinavyotakiwa. Baada ya matatizo hayo kushindikana, Mamlaka ikaamua kuendelea kutumia njia zisizo za kielektroniki ("deep stick"- fimbo ya kutumbukiza kwenye matangi ya mafuta) kwenye kupima shehena za mafuta yanayoingia nchini.

Kitendo hicho kina athari kwa mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania katika uhakiki wa usahihi wa kiasi cha kodi kinacholipwa kutokana na upimaji wa shehena hizo za mafuta bila ya kutumia vifaa stahiki na athari katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka ya Bandari Tanzania.

### 3.6.3 Kutokuwepo kwa Mkataba wa Kugharamia Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Afya

Ukaguzi ulibaini kuwa, katika ujenzi wa kituo cha afya unaondelea Chuo Kikuu cha Dodoma, hakuna mkataba halali kwa fedha zilizotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kutokuwepo kwa mkataba kumesababisha kukosekana kwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali kama vile haki na wajibu wa kila upande katika mkataba huo, namna marejesho yatakavyokuwa yanafanyika na pia mfuko uko katika hatari ya kupoteza fedha nyingi iwapo litatokea tatizo la kisheria. Nashauri Serikali na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya waingie kwenye makubaliano rasmi yatakayoainisha haki na wajibu wa kila upande.

### 3.6.4 Kuvunjwa kwa Makubaliano ya Uwiano wa Umiliki wa Hisa

Kufuatia magawio mbalimbali ya hisa za ziada kwa Serikali ya Tanzania, Umiliki wa hisa wa benki ya posta kufikia tarehe 31 Disemba, 2012 ulikua ni uwiano wa 80.4:4.1:11.8:3.7 kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shirika la Posta Tanzania na Chama cha Kuweka na Kukopa cha TP&TC sawia. Hata hivyo, sheria ya Benki ya Posta Tanzania ya mwaka 1991 inaelekeza kuwa umiliki wa hisa uwe kwa uwiano wa 41:10:30:39 kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Benki ya Posta Tanzania na ushirika wa TP&TC sawia. Hali hii inaweza kuleta matatizo ya kisheria wakati wa ugawanywaji wa gawio la faida.

### 3.6.5 Kodi ya Upangaji ambayo Haijalipwa Kwa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

Kampuni ya Simu Tanzania ina majengo yake ambayo inayapangisha kwa Wizara, Taasisi za Serikali na makampuni mengine binafsi ambayo kwa mujibu wa mkataba yanatakiwa kulipa kodi kabla ya muda. Hata hivyo baadhi ya wapangaji hawajalipa kodi ya pango kwa muda mrefu. Makampuni yafuatayo hayajalipa madeni yao; Airtel (Shilingi za Kitanzania milioni 687.631), Wizara ya Afya (Shilingi za Kitanzania milioni 419.394), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Shilingi za Kitanzania milioni 267.187), Universal Communications (Shilingi za Kitanzania 216.967), Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi (Shilingi za Kitanzania milioni 213.125) na e-government (Shilingi za Kitanzania milioni 211.359).

Mlipaji Mkuu wa Serikali hajatoa majibu yoyote kuhusu suala hili ingawa wapangaji wengi wanaodaiwa ni Taasisi za Serikali. Kutokukusanywa kwa kodi hiyo kunasababisha Kampuni ya Simu kukosa fedha za kujiendesha na kuendeleza miradi ya maendeleo.

### 3.6.6 Ukosefu wa Mwongozo Unaoeleweka Kuhusu Michango Inayotolewa na TANAPA Kwa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma

Mamlaka ya Hifadhi Tanzania inakabiliwa na michango kadhaa ya kikanuni, michango na misaada kama inavyoelekezwa na Wizara mama kupitia nyaraka mbalimbali na sheria zilizoanzishwa na Bunge.

Baadhi ya Kanuni za sheria za Bunge za kuanzisha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zimetamka wazi kuwa moja ya vyanzo yake vya mapato itakuwa asilimia fulani ya makusanyo ghafi ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA). Kwa mfano Kanuni ya 3(a) ya Utalii (*Tourism Development Levy*) ya mwaka 2012 imetamka kuwa asilimia 3 itakusanywa kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa kwa ajili kuendeleza utalii na itawekwa chini ya Usimamizi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Mali Asili na Utalii.

Kuhusu fedha inayolipwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, utaratibu wa sasa ni kukubaliana na Msajili wa Hazina juu ya kiasi cha kulipa. Miongoni mwa Mashirika yaliyonufaika na michango kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ni Bodi ya Utalii. Kwa upande mwingine, lengo namba 4 la Shirika la Hifadhi za Taifa linahusu kuendeleza utalii katika nchi, kazi ambayo pia inafanywa na Bodi ya Utalii Tanzania. Hali hii inasbabisha kazi moja ya kuendeleza utalii kufanywa na Mashirika mawili tofauti. Kama hatua za makusudi hazitachukuliwa kulinda rasilimali fedha, Shirika la Hifadhi za Taifa linaweza

kushindwa kutekeleza mipango yake ya muda mrefu kwa kukosa fedha.

### 3.6.7 Kuongeza Tija na Ufanisi wa Mabaraza ya Watumiaji wa Huduma

Serikali imekuwa ikianzisha mabaraza mbalimbali ya kuwatetea watumiaji wa huduma (Consumer Consultative Councils – CCC) nchini kwa ajili ya kushughulikia haki za watumiaji wa huduma kwenye Taasisi zinazoshughulika na huduma. Mabaraza mbali mbali yaliyoanzishwa yana lengo moja la kumwakilisha mtumiaji wa huduma ambapo yanatumia gharama kubwa ambazo zingeweza kupunguzwa kama mabaraza haya yangeweza kufanya kazi kama chombo kimoja. Kwa sasa kuna mabaraza manne ya kuwatetea watumiaji wa huduma/walaji kama vile Baraza la kuwatetea watumiaji/walaji wa Nishati na Maji (EWURA CCC), Baraza la kuwatetea watumiaji wa huduma ya usafiri wa nchi kavu na majini (SUMATRA CCC), Baraza la kuwatetea wafugaji Ngorongoro (Ngorongoro CCC) na Baraza la kuwatetea watumiaji wa Mawasiliano (TCRA CCC).

Ninaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha mabaraza hayo ili yaweze kufanya kazi kama chombo kimoja hali itakayosaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuwa na Mkurugenzi Mtendaji mmoja akisaidiwa na Wakurugenzi watakaoongoza kurugenzi mbalimbali za sekta husika kwa vile wote wanahudhumia walaji wenye mahitaji yanayoendana ya kupata hudhuma.

### 3.6.8 Uteuzi wa Mfanyakazi wa Bandari katika Bodi ya Wakurugenzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 6(2) cha sheria ya Mamlaka ya Bandari Na.17 ya mwaka 2004, Waziri wa Uchukuzi anayo mamlaka ya kuteua wajumbe watano (5) ili kuungana na Mwenyekiti aliyeteuliwa na Rais kuunda Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania. Nilibaini mfanyakazi mmoja anayewakilisha wafanyakazi katika chama cha wafanyakazi wa Bandari (DOWUTA) ameteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Hii ni kinyume na kanuni na taratibu za utawala bora katika kuliongoza Shirika kwa kuzingatia kuwa Bodi inalo jukumu kubwa la kusimamia na kulielekeza Shirika katika utendaji wa shughuli zake. Hali hii inaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi na utendaji usioridhisha wa Bodi ya Wakurugenzi.

### 3.6.9 Maendeleo ya Soko la Mitaji

Ubinafsishaji na maendeleo ya masoko ya mitaji vinategemeana. Ubinafsishaji husaidia makampuni kufanya kazi kwa ufanisi na kwa faida na hivyo kuyafanya yaweze kuwa na sifa ya kuorodheshwa katika

soko la hisa. Soko la Hisa la Dar-es-Salaam lilianzishwa mwaka 1998 ili kusaidia mchakato wa urekebishaji wa sekta ya fedha, kuhamasisha umiliki wa hisa kwa watanzania na kusaidia mchakato wa ubinafsishaji.

Changamoto kubwa zilizoathiri maendeleo ya Soko la Hisa ni kuwa na kiwango kidogo cha mauzo na idadi ndogo za huduma zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa na Mitaji. Ukuzaji wa umiliki wa Mashirika ya Umma kwa watanzania ilikuwa ni moja ya malengo ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma Tanzania. Hata hivyo, Mashirika mengi makubwa yalibinafsishwa na kuuzwa kwa mataifa ya kigeni.

Ni muhimu kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam kutoa elimu kwa wananchi kuhusu manufaa ya kuwekeza kwenye masoko ya mitaji. Elimu hii itawezesha wananchi kutambua fursa za uwekezaji katika masoko ya mitaji na kuzitumia vizuri.

### 3.6.10 Benki ya Azania

Benki ya Azania (hapo mwanzo ikiitwa 1st Adili Bancorp Limited) ni benki binafsi iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) 34.8%, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) 30.1%, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) 17.2%, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF) 14.2%, Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) 2.3%, Wafanyakazi wa Benki ya Azania na wanahisa wengine (1.4%). Mifuko ya pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 96.3 ya hisa zote katika benki ya Azania. Hali hii inamaanisha kuwa mifuko hii ina uwezo wa kuisimamia benki hii kwa kutoa miongozo na maamuzi muhimu yanayohusu shughuli za uendeshaji. Kwa upande mwingine, Mifuko yote ya pensheni inamilikiwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina. Kwa kuzingatia uhusiano huu, ni wazi kuwa benki ya Azania inamilikiwa na Serikali kupitia Mifuko ya Pensheni.

Hata hivyo, Benki hii ilianzishwa kama benki binafsi iliyoandikishwa kwa kutumia Sheria ya Makampuni (Companies Act) na hivyo kutokuwa na sheria ya Bunge ya kuianzisha. Hii imesababisha benki hii kutokuwepo katika orodha ya Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina na hivyo halijawahi kuwasilisha hesabu kwenye Ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a) (iii) na (iv) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

### 3.6.11 PRIDE Tanzania Limited

Taasisi ya PRIDE Tanzania ilianzishwa mnamo tarehe 5 Mei, 1993 chini ya Sheria ya Makampuni (CAP 212) kwa dhamana (*limited by guarantee*). Dhumuni la kuanzishwa kwa chombo hiki ni kutoa mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali. Chanzo kikuu cha fedha za kuanzisha Taasisi hiyo kilitoka NORAD kwa makubaliano baina ya Serikali za Tanzania na Norway. Pia Serikali ya Sweden ilijiunga kukifadhili chombo hiki mwaka 2001. Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina ya uwekezaji wa Serikali katika makampuni kufikia tarehe 30 Juni, 2008, ilionyesha kuwa hisa zote za PRIDE zinamilikiwa na Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina inayoishia tarehe 30 Juni, 2013 nimebaini kuwa Shirika hili halipo tena kwenye orodha ya Mashirika ya Umma. Uhalali na sababu za kuondolewa kwa Shirika hili katika orodha ya Msajili wa Hazina hazikuweza kubainika.
Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, kila Shirika la Umma linatakiwa kuleta hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kukaguliwa katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Hata hivyo, hesabu za PRIDE Tanzania hazijawahi kuwasilishwa kwenye Ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa na Sheria.

### 3.6.12 Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma

Ukaguzi uliofanyika baada ya ubinafsishaji ulibaini masuala kadhaa ya ukiukwaji wa sheria. Napenda kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Msajili wa Hazina kuzingatia Sheria ya Mashirika ya Umma ili kuondokana na uwezekano wa mgongano wa kimaslahi baina ya Serikali na vyombo vingine vilivyopewa majukumu ya kusimamia kwa mujibu wa Sheria. Pia kuzingatia Sheria, katika kufuatilia na kudhibiti Mashirika yaliyobinafsishwa ili kuhakikisha kuwa yanafanya kazi sawa na mipango ya uwekezaji iliyowekwa kwa mujibu wa makubaliano katika mikataba ya mauzo.

Ninapenda pia kupendekeza kwa Msajili wa Hazina kuhakikisha anafanya kazi kwa bidii ili kutathmini utendaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa na kubaini kama yanafanya kazi kwa kuzingatia makubaliano ya mikataba ya mauzo. Pia kwa Mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kuuzwa, usimamizi kwa Bodi za Wakurugenzi uimarishwe ili kuhakikisha kuwa Mashirika hayo yanaendelea kufanya kazi kulingana na madhumuni ya uanzishwaji wake.

Msajili wa Hazina anashauriwa kuchukua hatua za haraka kuhusu masuala yaliyoainishwa katika taarifa iliyoandaliwa na Kampuni ya PKF Tanzania kabla ya Serikali kuitwaa "Kiwira Coal Mine". Mlipaji Mkuu wa Serikali hajatoa majibu kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye taarifa ya ukaguzi maalum wa "Kiwira Coal Mine".

### 3.6.13 Ubinafsishaji wa Southern Paper Mills (SPM)

Southern Paper Mills iliuzwa kwa Kampuni ya Rai Group ya Kenya kwa Dola za Kimarekani milioni 26 mnamo mwaka 2004. Mkataba wa mauziano ulitamka kwamba bei iliyokubaliwa ni Dola za Kimarekani milioni 26 itakayolipwa kama ifuatavyo; Dola za Marekani milioni 1 wakati wa kusaini mkataba, Dola za Marekani milioni 3 kuwekwa kwenye "escrow account" na Dola za Marekani milioni 22 kutumika na mnunuzi kwa (i) kuwekeza katika kampuni kwa kipindi cha miaka miwili ya kwanza (Dola za Marekani milioni 16.2) na (ii) Dola za Marekani milioni 5.8 katika mwaka wa tatu. Ilikubaliwa pia kwamba kiasi kilichowekwa kwenye "escrow account" kitolewe na mwekezaji baada ya kuweka uwekezaji wa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 22.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba Dola za Marekani milioni 3 zilizowekwa kwenye "escrow account" zitarejeshwa kwa mwekezaji na Dola za Marekani milioni 22 zitawekezwa kwenye SPM. Kiasi kinachobaki ni Dola za Marekani milioni moja (1) tu kuwa bei halisi ya kuuzia mali za SPM.

Kwa maoni yangu, hii ina maana kwamba kama bei ya kuuzia ni Dola za Marekani milioni 26 ina maana kwamba mali za SPM hazikuuzwa kwa mwekezaji lakini inamilikiwa na Serikali kwa kuwa malipo yaliyofanywa kwa mali za SPM hazikwenda kwa Serikali bali ziliwekezwa katika SPM. Kiasi cha Dola za Marekani milioni 22 zilizowekwa SPM kama sehemu ya bei ya kuuzia zilitakiwa kufanywa kama sehemu ya uwekezaji wa Serikali katika SPM.

Zaidi ya hayo, hakuna ushahidi kwamba Tume ya Urekebishaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa au Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilifanya usimamizi na tathmini ya ubinafsishaji na utekelezaji wa mkataba wa uuzaji.

Msajili wa Hazina anapaswa kufanya tathimini ya utekelezaji wa mkataba wa mauzo wa Shirika hili na usahihi wake kwani kwa hali halisi SPM bado ni mali ya Serikali.

# SURA YA NNE

## MASUALA MUHIMU AMBAYO HAYAKUTOLEWA TAARIFA KATIKA RIPOTI YA MWAKA ULIOPITA

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea masuala muhimu yanayohusiana na ripoti ya kaguzi zilizopita za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo matokeo ya kaguzi zao hazikuingia katika ripoti ya mwaka 2012/2013 kutokana na sababu mbalimbali zilizokuwa nje ya uwezo wangu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ni wajibu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kufunga mwaka husika wa fedha. Kwa vile kumekuwa na kiasi kikubwa cha kutokuzingatiwa kwa matakwa haya ya Sheria na baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, baadhi ya kaguzi hazikukamilika kwa wakati na hivyo kumfanya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ashindwe kuziandika katika taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2012/2013. Ni muhimu ikaeleweka kuwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo kaguzi zake zitashindwa kukamilika katika kipindi kinachotakiwa na hivyo kutoripotiwa katika ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zitaripotiwa katika ripoti ya mwaka unaofuata.

Hadi kufikia kipindi cha kuandaa taarifa jumla ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2012/2013 iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais mwishoni mwa mwezi Machi, 2014, ni kaguzi za Mashirika 93 tu zilikamilika kikamilifu, ambapo kaguzi 10 hazikuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa ajili ya kuridhia hesabu. Kaguzi za Mashirika 74 yaliyobaki zilikuwa kwenye hatua mbalimbali ya ukamilishaji ripoti kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuchelewa kuwasilishwa kwa hesabu, vikao vya Bodi ya Wakurugenzi vya kuridhia mahesabu kutokufanyika kwa wakati na Menejimenti za Mashirika husika kushindwa kujibu hoja za ukaguzi kwa wakati. Masuala muhimu ambayo hayakuandikwa kwenye ripoti yangu iliyopita ni pamoja na:

## 4.1 Utumiaji wa Njia ya Ununuzi usio wa Ushindani katika Shirika la Nyumba la Taifa Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.75 na Dola za Kimarekani Milioni 5.54

Kifungu Na. 58(2) cha Sheria Na. 21 ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 kinataka ununuzi wowote na uuzaji wa rasilimali za umma ufanyike kwa ushindani kwa manufaa ya kiuchumi, kuleta ufanisi, uwazi na thamani ya fedha. Kinyume na matakwa haya, nilibaini kwamba Shirika la Nyumba la Taifa lilitumia njia ya ununuzi ya chanzo kimoja ambapo mikataba mbalimbali iliyopitiwa ilibainika kutokuzingatia ushindani wenye lengo la kupata thamani ya fedha. ununuzi huo ulikuwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.75 na Dola za Kimarekani milioni 5.54.

Hali kadhalika, kanuni Na. 69(1) ya Kanuni za Ununuzi ya Umma, 2005 (Tangazo la Serikali Na. 97) inaruhusu njia ya ununuzi kutoka chanzo kimoja endapo bidhaa husika zinapatikana kwa mzabuni mmoja tu, kuna hali ya udharura, kuna hitaji la nyongeza ya bidhaa kutokana na mkataba wa awali au kama bidhaa zinahusiana na masuala yahusuyo Ulinzi na Usalama wa Taifa. Uanunuzi ambao ulifanyika kutumia chanzo kimoja na kutothibitishwa yameonyeshwa katika kiambatanisho V.

## 4.2 Usimamizi na Utekelezaji Mbovu wa Mikataba katika Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

Katika mapitio ya usimamizi wa mikataba nilibaini kwamba tarehe 7 Februari, 2007 Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) kiliingia mkataba na M/s Gross Investment Limited kwa ajili ya ukarabati wa maabara uliogharimu Shilingi za Kitanzania milioni 333.396. Mradi huu ulipangwa kukamilika ndani ya wiki sita kutoka tarehe ya kusaini mkataba. Hata hivyo, mradi huo ulikamilika tarehe 9 Agosti 2012 ikiwa ni miaka mitano (5) baadaye. Matokeo yake Kituo kililipa Shilingi za Kitanzania milioni 376.912 ambazo ni zaidi kwa Shilingi za Kitanzania milioni 43.516 ya bei ya mkataba. Kutokana na maelezo ya Menejimenti, hali hiyo ilisababishwa na upungufu wa fedha uliokuwa unakikabili kituo hicho.

Kwa mtazamo wangu hii ilisababishwa na kutokuwa na usimamizi makini wa mikataba uliosababisha Kituo kuingia gharama za ziada ambazo hazikuwa na ulazima.

Pia nilibaini kwamba Kampuni ya M/s Taji Co. Ltd inamiliki jengo la mgahawa lililojengwa katika ardhi ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Kutokana na mkataba wa makubaliano kati ya Chuo Kikuu cha Dodoma na kampuni ya M/s Taji Co. Ltd, kampuni imepewa hati ya kukodisha ya miaka 33 iliyoanza tarehe 1 Septemba, 2007 na kutegemewa kuisha muda wake tarehe 30 Agosti, 2040 kwa ajili ya kujenga na kuendesha mgahawa kama ilivyoelezwa katika hati ya kukodisha. Zaidi ya hayo, nilibaini kwamba jengo la mgahawa lililojengwa na Kampuni hivi sasa halifanyi kazi tangu wanafunzi na wafanyakazi kuhamishiwa kwenye maeneo tofauti ndani ya Chuo Kikuu cha Dodoma, ambapo ni mbali na ulipo mgahawa wa Kampuni hiyo.

Hali kadhalika, nilibaini kwamba hakukuwa na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Kampuni hiyo kuhusu jinsi ya kuendesha jengo hilo katika Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya muda wa mkataba kufikia kikomo.

Pia, Kampuni ya Taji Ltd imekuwa mpangaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma tangu mwaka 2007. Kampuni inatoa huduma ya mgahawa katika Chuo cha Sayansi ya Jamii na Binadamu na jengo Kuu la Utawala. Kodi ya mwezi kwa kila mgahawa kulingana na makubaliano ni kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 1.3. Hata hivyo, nilibaini hakukuwa na kodi ya pango iliyolipwa Chuo Kikuu cha Dodoma licha ya Kampuni kukumbushwa kwa hati ya madai. Mpaka sasa, deni la kodi limelimbikizwa na kufikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 84.5. Kadiri deni linavyozidi kukua bila ya kulipwa linaongeza hatari ya uwezekano wa Chuo kutolipwa na mpangaji huyo.

## 4.3 Madeni ya muda mrefu katika Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Wakati wa kuhakiki wadaiwa katika vitabu vya hesabu vya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kwamba baadhi ya madeni ya wadaiwa yamekuwa hayaonyeshi kupungua katika mwaka hali inayoashiria makusanyo hafifu ya madeni. Katika mazingira hayo, madeni ya muda mrefu yameendelea kuongezeka na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hali inayoweza kusababisha kushindwa kujiendesha.

Mapungufu haya yalibainika katika Shirika la Posta Tanzania ambapo madeni yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 2.695 yakijumuisha salio la Shilingi za Kitanzania milioni 118.675 ikiwa ni deni la waliokuwa mawakala/watumishi ambalo halijalipwa kwa muda mrefu.

Hali kadhalika, katika uhakiki wa salio la deni la wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania, nilibaini kwamba masurufu ya wafanyakazi ya muda mrefu yalipanda na kufika kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 306.29 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2012 kutoka kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 164.23 kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2011. Hii ilichangiwa na utoaji wa masurufu mapya kabla ya masurufu ya zamani kurejeshwa.

Zaidi, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam haikukusanya madeni yake ya muda mrefu kutoka kwa wanafunzi kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 215.664. Pia, Shirika la Nyumba la Taifa lilikuwa linawadai wapangaji wake deni la muda mrefu lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 3.29. Hakukuwa na ushahidi iwapo kiasi hiki kitalipwa kwa Shirika la Nyumba la Taifa kwani kiasi kikubwa kilikuwa katika mgogoro na wadaiwa. Ingawa mkataba wa pango unalipa Shirika mamlaka ya kumwondoa mpangaji endapo hatalipa kodi kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu, hakukuwa na ushahidi wa wapangaji walioondolewa na Shirika katika nyumba hizo.

### 4.4 Kutosuluhishwa kwa Vitabu vya Hesabu na Taarifa za Kibenki kwa muda mrefu kwa Kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 436.2 katika Shirika la Posta Tanzania

Lengo la kuandaa taarifa ya usuluhishi wa kibenki ni kubaini tofauti zinazoweza kujitokeza kati ya kumbukumbu za vitabu vya Taasisi na kumbukumbu za Benki kwa ajili ya hatua za kusuluhishwa.

Mapitio ya taarifa za usuluhishi wa kibenki za Shirika la Posta Tanzania yalibaini kutosuluhishwa kwa tofauti ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 436.2 na hivyo kubakia kwa kipindi cha muda mrefu bila suluhu. Jedwali Na. 3 hapa chini linatoa maelezo;

**Jedwali 3:Orodha ya kutosuluhishwa kwa tofauti zilizojitokeza**

| Na | Maelezo | Mwaka | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Fedha zilizoingizwa katika kitabu cha fedha taslimu lakini hazijapokelewa Benki | 2006 hadi 2012 | 122,336,454 |
| 2. | Fedha zilizotolewa katika taarifa za Benki lakini hazijaonekana kutolewa katika kitabu cha fedha taslimu | 2008 hadi 2012 | 49,619,052 |
| 3. | Fedha zilipokelewa katika taarifa za Benki lakini hazijaonekana katika kitabu cha fedha taslimu | 2011 hadi 2012 | 264,250,611 |
| **Jumla** | | | **436,206,117** |

Hali kadhalika, nilibaini kutofanyika kwa wakati kwa usuluhishi kulisababisha baadhi ya akaunti za benki kuonyesha deni lenye kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 353.59 ambalo lilionyeshwa katika vitabu vya hesabu za Shirika kama fedha zilizotolewa zaidi ya fedha iliyopo katika akaunti ya benki. Hata hivyo, katika mapitio, nilibaini kwamba kulikuwa hakuna mkopo (Overdraft) uliokuwa umetolewa kwa Shirika na benki.

Akaunti za benki ambazo zilionyesha deni zimeonyeshwa katika jedwali Na. 4

**Jedwali 4: Akaunti za Benki Zilizoonyesha Deni**

| Na | Namba ya Akaunti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | NBC 011103020240 (Makao Makuu) | (58,770,905.66) |
| 2. | NBC 011105007500 (Makao Makuu) | (82,535,484.18) |
| 3. | NBC 011103020226 (Makao Makuu) | (212,291,878.22) |
| **Jumla** | | **(353,598,268.06)** |

### 4.5 Ucheleweshwaji wa Kuwasilisha Makato ya Kisheria

Kutokana na kifungu Na. 84 (1) na (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (Kama inavyorekebishwa mara kwa mara) mishahara na malipo mengine yote au mafao ambayo yanalipwa kwa waajiriwa yanapaswa kulipiwa kodi ya Lipa Kadiri Upatavyo (P.A.Y.E) na kiasi cha kodi kinachokatwa na mwajiri lazima kiwasilishwe kwa Kamishina wa Kodi ya Mapato kila siku ya tarehe 7 ya mwezi au kabla ya mwezi unaofuatia mwezi wa makato. Hata hivyo, Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania haikuwasilisha kwa wakati makato kwa ajili ya PAYE, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na michango ya SDL hali iliyopelekea limbikizo la deni kufikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 4.019, 2.063 na 2.679 sawia.

### 4.6 Deni la Mchango wa Mfuko wa Pensheni wa PPF katika Shirika la Posta Tanzania Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.6

Kifungu na (9) cha Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa PPF ya mwaka 1978 kinaainisha kwamba michango inayodaiwa inapaswa kulipwa ndani ya siku thelathini baada ya mwisho wa kila mwezi. Malipo yatakayowasilishwa baada ya siku thelathini ya kipindi cha matazamio yatapaswa kutozwa adhabu ambayo itakokotolewa kama riba (Compound Interest) katika kiasi kinachodaiwa kwa mwezi.

Katika mapitio ya mwaka, nilibaini kwamba Shirika la Posta Tanzania lilikuwa likidaiwa na Mfuko wa Pensheni wa PPF kutokana na michango ya mwaka 2005 na 2006 ikijumuisha adhabu kwa ajili ya ucheleweshaji

wa malipo ya makato kwa tawi la ofisi ya Mbeya na Makao Makuu hadi kufikia Shilingi za kitanzania bilioni 2.589. Hii imethibishwa kwa barua kutoka kwa Mfuko wa Pensheni wa PPF yenye kumbukumbu Na. PPF/GB.56/217/01/G.52 ya tarehe 4 Machi 2013 na kuambatanishwa notisi ya kutozwa adhabu. Gharama hii ya deni na adhabu hazikuwa zimeonyeshwa katika vitabu vya hesabu kwa mwaka wa ukaguzi kwa sababu kwamba deni hili limechukuliwa na Serikali tangu mwaka 2006. Ni wajibu wa Shirika kuhakikisha michango ya mwajiriwa na mwajiri yote kwa pamoja inawasilishwa haraka katika Mfuko husika kama sheria inavyotaka. Kwa hiyo, endapo Serikali itashindwa kulipa deni husika kwa Mfuko wa Pensheni wa PPF, Shirika litawajibika kwa deni lilobaki bila kulipwa kwa muda mrefu ili kuwezesha wahusika kulipwa stahiki zao za mafao baada ya kustaafu.

## 4.7 Wadai Wa Muda mrefu katika baadhi ya Taasisi za Umma

Katika ukaguzi wa madeni ya muda mrefu ya Mashirika ya Umma, nilibaini kwamba Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilikuwa na wadai wa muda mrefu kwa zaidi ya mwaka mmoja kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 236.833. Sikuweza kuthibitisha uwepo wa akaunti hizi baada ya kukosekana kwa ushahidi wa nyaraka ambazo hazikutolewa kwa ajili ya uhakiki wa kikaguzi. Masalio ya wadai bila ya kuwa na nyaraka za uthibitisho ambazo zimeonyeshwa katika jedwali na.5.

**Jedwali 5: Wadai wa muda mrefu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

| Na | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Wadai walioweka fedha | 38,697,473 |
| 2 | Fedha iliyowekwa na HESLB | 64,651,317 |
| 3 | Benki ya Standard Chartered | 2,252,272 |
| 4 | Benki ya Zanzibar | 4,962,224 |
| 5 | Fedha zilizohamishwa | 31,394,444 |
| 6 | Madai ya PPF/NSSF/SSS | 62,392,081 |
| 7 | Fedha zilizowekwa na Bungo | 17,827,871 |
| 8 | Mfuko wa Serikali ya Wanafunzi | 14,655,451 |
| **Jumla kuu** | | **236,833,133** |

Pia, udhaifu huu ulibainika katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tekinolojia cha Mbeya ambapo kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 100.22 zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya miaka saba.

## 4.8 Kutohuishwa kwa Daftari la Kumbukumbu za Mali za Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya

Uhakiki wa mali, mitambo na vifaa katika daftari la kumbukumbu la mali za Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, ulibaini kwamba daftari halikuhuishwa kwa muda mrefu. Mapitio yalibaini kwamba kiasi kilicho ripotiwa katika daftari la Kumbukumbu za Mali kilikuwa ni Shilingi za Kitanzania bilioni 16.6 na kiasi kilichoripotiwa katika hesabu kilikuwa ni Shilingi za Kitanzania bilioni 19.5 ambapo ilipelekea utofauti wa Shilingi za Kitanzania bilioni 3.89.

## 4.9 Kutohakikiwa kwa Vifaa Katika Maghala Vyenye Thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 136.46

Kutokana na aya Na. 6 ya Kiwango cha Uhasibu cha Kimataifa namba mbili (2), vifaa vinajumuisha mali zinazoshikiliwa kwa ajili ya kuuzwa katika hali ya kawaida ya biashara (bidhaa zilizokamilika kutengenezwa), mali zilizopo katika mchakato wa uzalishaji kwa ajili ya kutumika katika biashara (kazi zinazoendelea), na vitu vya kutengenezea na usambazaji ambavyo vilitumika katika uzalishaji (mali ghafi).

Katika ukaguzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, nilibaini kwamba vitabu vyao vya hesabu viliripoti thamani ya vifaa vya ghalani kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 129.95 na milioni 6.51 sawia. Hata hivyo, hakukuwa na nyaraka au ushahidi wa kuthibitisha uwepo, asili, aina, na thamani ya vifaa vilivyokuwa ghalani. Pia, kulikuwa hakuna daftari la ghala ambalo linathibitisha thamani ya vifaa vilivyohifadhiwa ghalani. Vifaa vya ghalani vya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania vilikuwa vimeropitiwa kwa zaidi ya miaka ishirini kwa thamani ile ile kinyume na Kiwango cha Uhasibu cha Kimataifa namba 2 ambacho kinatoa mchanganuo wa kuthamanisha vifaa vilivyopo ghalani.

## 4.10 Hali ya uhai wa baadhi ya Mashirika ya Umma

Kulingana na Kiwango cha Kimataifa cha Ukaguzi Na.570 chini ya dhana ya uhai endelevu, Taasisi inatazamwa kama itaendelea na shughuli zake kwa zaidi ya kipindi cha miezi kumi na mbili (12) ijayo. Dhumuni kuu ni kuhakikisha vitabu vya hesabu vinaandaliwa katika hali endelevu isipokuwa kama Menejimenti ina dhamira ya kusimamisha uendeshaji au haijabainisha njia nyingine isipokuwa kufanya hivyo. Mali na Madeni yanawekwa katika kumbukumbu kwa namna ambayo Taasisi itaweza kuuza mali zake na kulipa madeni yake katika hali ya kawaida ya kibiashara.

Wakati wa mapitio ya hesabu, nilibaini kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yalipata hasara na kushindwa kulipa madeni ya muda mfupi. Hali hii ilipelekea uwiano wa madeni na mali kutoshabihiana na uwiano unaokubalika wa kihesabu wa 2:1.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zimekumbwa na tatizo la kutetereka kwa mtaji wa kujiendesha;

**Jedwali 6:Hali ya Uhai wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma**

| Na. | Jina la Taasisi | Hasara Iliyopatikana(Sh.) | | Uwiano wa mali na madeni (Kiwango kinachokubalika 2:1) | | Jumla ya Madeni Iliyozidi Jumla ya Mali (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWAKA 2011/12 Sh. | MWAKA 2012/13 Sh. | MWAKA 2011/2012 | MWAKA 2012/2013 | |
| 1. | DIT | Bilioni1.5 | Milioni 68.4 | 0.53:1 | 0.6:1 | - |
| 2. | TFC | Bilioni1.58 | Bilioni 3.78 | 0.40:1 | 0.28:1 | Bilioni 4.59 |
| 3. | OUT | - | Bilioni 1.09 | - | 0.69:1 | - |
| 4. | TDB | Milioni 58.145 | Milioni 75.903 | 1.50:1 | 0.24:1 | Milioni 49.67 |
| 5. | COSOTA | - | Milioni 231.1 | - | 0.28:1 | Milioni 124.14 |

Uwiano ulioonyeshwa kwenye jedwali Na. 6 unaonyesha uwepo wa mashaka makubwa juu ya uwezo wa Taasisi hizi kuendelea kujiendesha endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa na Serikali kuyanusuru Mashirika hayo.

## 4.11 Ucheleweshwaji wa Malipo ya Fidia na Yaliyosababisha Limbikizo la Riba ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.3

Miongoni mwa shughuli kuu ambazo Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania imekuwa ikizifanya ni ununuaji wa ardhi kutoka maeneo yaliyotengwa na kulipa fidia kwa wenye ardhi baada ya kuthaminishwa na mthamini wa Serikali. Kulingana na Sheria za ardhi kiasi ambacho hakitalipwa kama fidia kitalimbikiza riba ya kiwango cha asilimia sita (6%) kila mwaka.

Katika ukaguzi, nilibaini kwamba Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania haijalipa limbikizo la fidia la Shilingi za Kitanzania bilioni 58.26. Fedha hizo zilikuwa ni kwa ajili ya kununua ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Ukaguzi wa Mamlaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 ulibaini kuwa riba ya jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 3.3 ambayo ilikuwa imelimbikizwa kwa muda mrefu haikuwa imelipwa. Hali hii inapelekea malipo yasiyo ya lazima ya kiasi kikubwa cha riba ambacho Mamlaka ingeweza kuepuka iwapo fidia ingelipwa kwa wakati.

## 4.12 Kutothamanishwa kwa Ardhi na Majengo ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya

Kiwango cha Uhasibu cha Kimataifa namba 16 (Aya ya 58) kinaeleza kwamba ardhi na majengo ni mali tofauti ambazo zinaripotiwa katika vitabu vya hesabu kwa kutenganishwa, hata kama vimenunuliwa pamoja. Majengo yanakuwa na ukomo wa matumizi na hivyo ni mali inayochakaa huku ardhi ikiwa inaongezeka thamani kadiri muda unavyokwenda.

Katika upitiaji wa vitabu vya hesabu vya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya nilibaini kwamba Chuo kimeripoti ardhi na jengo kwa pamoja kwa thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 15.22. Mali hizi mbili zilikuwa hazikuthamanishwa au kuwekwa kulingana na matakwa aya Na. 58 ya Kiwango cha Uhasibu cha Kimataifa Na.16.

## 4.13 Kutolipwa kwa Mikopo Iliyodhaminiwa na Serikali

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulilitoa mikopo kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zilipata udhamini wa Serikali. Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uliripoti mikopo ambayo imedhaminiwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa asilimia 100. Hakuna marejesho ambayo yamefanyika kwenye mfuko hadi mwisho wa mwaka huo wa fedha. Pia, nilibaini kuwa udhamini wa Serikali ulikuwa ni dhaifu kwa sababu mfuko haukuwa na uwezo wa kuilazimisha Serikali kulipa. Hivyo, mfuko umekuwa katika hatari zaidi ya kutokukusanya fedha ya mikopo iliyotolewa ambayo inaweza kupelekea kushindwa kujiendesha. Ifuatayo ni orodha ya mikopo iliyodhaminiwa na Serikali;

- Mkataba wa kutoa fedha awamu ya pili kwa ajili ya kujenga majengo ya Wizara uliosainiwa tarehe 29 Disemba, 2009 ikiwa na kiasi cha mkopo wa Shilingi za Kitanzania bilioni 23.12.

- Mkataba kwa ajili ya ufadhili wa ujenzi wa nyumba za Wizara uliosainiwa tarehe 12 Agosti, 2008 na 29 Disemba, 2009 ikiwa na mkopo wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 25.38.

- Mkataba wa ujenzi wa majengo ya Wizara uliosainiwa tarehe 17 Agosti, 2007 wenye kiasi cha mkopo wa Shilingi za Kitanzania bilioni 5.63.

- Mkataba wa kutoa fedha wa ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Jamii na Binadamu katika Chuo Kikuu cha Dodoma wenye kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 277.75.

- Mkataba wa kutoa fedha kwa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa Tanzania (NIDA) tarehe 30 Disemba, 2012 wenye kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 20.

## 4.14 Kutoandaliwa Mpango Mkakati wa Shirika katika Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania

Katika ukaguzi wa Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania, nilibaini kuwa Bodi ilikuwa haina Mpango Mkakati ulioandaliwa. Zaidi, nilibaini kuwa hakuna mpango wa kiutendaji ulioandaliwa. Pia, hakukuwa na ripoti ya utendaji zilizoandaliwa ili kuangalia mafanikio ya shughuli zilizopangwa katika mwaka wa mapitio. Hali hii inasababisha Taasisi hii kutokuwa na malengo ya muda mfupi, wa kati na mrefu katika kujiendesha.

## 4.15 Kutoonyeshwa kwa Akaunti ya Dhamana ya Utendaji katika Vitabu vya Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania

Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania ilifungua akaunti yenye jina la "Warehousing Receipt System Performance Bond" tangu mwaka 2010 kulingana na mahitaji ya kifungu Na. 19(1) cha Sheria ya Stakabadhi ya Maghala ya mwaka 2005. Kifungu hiki kinasema kwamba kila mwendesha maghala aliyeomba kibali chini ya Sheria hii atalazimika kutekeleza na kuwasilisha kwa Bodi dhamana inayotosheleza na ya kuaminika kwa ajili ya kufuatilia utendaji wa aliyepewa leseni ya kuendesha ghala.

Ukaguzi ulibaini kwamba kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 469.98 zilipokelewa na kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 223.26 zililipwa kama zilivoonyeshwa katika taarifa za benki na vitabu vya hundi kwa akaunti hii. Hata hivyo, nilibaini kwamba Bodi ilikuwa haina daftari la fedha, taarifa ya usuluhishi na kumbukumbu za mapokezi, malipo au matumizi zilizohifadhiwa kwa ajili ya akaunti hii. Hali kadhalika,

nilibaini kwamba akaunti hii ilikuwa haijaonyeshwa na Bodi katika vitabu vyake vya hesabu tangu ilipofunguliwa.

### 4.16 Utoaji Vibali vya Ghala na Stakabadhi ya Dhamana kabla ya Malipo Kufanyika kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 260

Kifungu Na.29 cha Kanuni ya Stakabadhi ya Maghala ya mwaka 2006 kinaeleza kwamba dhamana ya ghala chini ya kifungu Na.19 cha sheria lazima isajiliwe na Bodi kabla ya kibali kutolewa kwa mwendeshaji wa ghala.

Hata hivyo, nilibaini kwamba Bodi ilitoa stakabadhi kwa mwendesha ghala kwa ajili ya gharama za dhamana kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 260 kinyume na matakwa ya Kanuni za Stakabadhi ya Maghala ya mwaka 2006. Kwa upande mwingine, kiasi hicho hicho hakikuhifadhiwa benki katika mwaka wa ukaguzi. Hii ina maana kwamba waendesha maghala wanaweza kuendesha maghala bila kuwa na dhamana ya utendaji kwa wakati na kuwaweka wakulima na Bodi katika hatari ya kutofidiwa endapo kutatokea uharibifu au hasara. Mfano, kampuni ya Chimbuli Trading Ltd ilipewa kibali Na. 25-2012 cha tarehe 13 Novemba 2012 kabla ya malipo ya ada ya kibali. Jedwali hapa chini linaonyesha mchanganuo;

**Jedwali 7:Stakabadhi zilitolewa kabla ya malipo ya ada ya leseni**

| Tarehe | Jina la Mlipaji | Namba ya Hundi | Kiasi (Sh.) | Namba ya Stakabadhi |
|---|---|---|---|---|
| 14/11/2012 | Chimbuli Trading Co. Ltd | 190885 | 59,000,000 | 415 |
| 14/11/2012 | Chimbuli Trading Co. Ltd | 190886 | 200,000,000 | 416 |
| 28/2/2013 | Wakefield Inspection Services Ltd | 180490 | 1,000,000 | 429 |
| **Jumla** | | | **260,000,000** | |

### 4.17 Kodi Iliyolipwa bila ya Kuwepo kwa Mkataba wa Kupangisha Kiasi cha Shilingi za kitanzania Million 62.5

Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania imepanga ofisi katika jengo la kitega Uchumi la Shirika la Bima ya Taifa ghorofa ya 12. Kodi ilitakiwa kulipwa kwa mwezi kwa Dola za Kimarekani. Kwa mwaka 2012/2013, Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania ililipa gharama za kodi ya shilingi za kitanzania milioni 62.5. Ukaguzi uliofanyika ulibaini kwamba kulikuwa hakuna makubaliano ya upangishaji kati ya Shirika la Bima la Taifa (Mpangishaji) na Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania (Mpangaji).

Kodi yote ilikuwa imelipwa kupitia barua ya ofa yenye kumbukumbu namba h&r/NDL/08/01 ya tarehe 12 Agosti, 2009 kwa ajili ya ghorofa ya 12, upande A. Katika ofa, kiasi cha kodi kilichopendekezwa ni Dola za Kimarekani 2,730 kwa mwezi katika kipindi cha miaka miwili. Katika mapitio ya mkataba, kiasi cha kodi kingebadilika kulingana na hali ya soko kama ilivyoandikwa katika aya ya 4 ya barua ya ofa. Hata hivyo, ukaguzi haukufanikiwa kupata mkataba wa awali wa upangishaji au ule uliotumika kuhuisha kodi ili kuweza kuthibisha usahihi wa kodi iliyolipwa. Kukosekana kwa makubaliano ya upangishaji kunaiingiza Bodi katika hatari ya kulipa madai ya kodi yasiyostahili.

## SURA YA TANO

## USIMAMIZI WA SHERIA YA UNUNUZI NA MIKATABA

### 5.0 Utangulizi

Tanzania imefanya maboresho makubwa ya mifumo ya ununuzi iliyopelekea kuanzishwa kwa sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 na hatimaye Sheria mpya ya hivi karibuni Na.7 ya mwaka 2011 ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika kwa manufaa ya Umma. Hivyo basi, ili kuhakikisha kwamba Sheria ya Ununuzi inafuatwa, kifungu Na. 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuainisha katika ripoti zake kama taratibu zote za ununuzi zimezingatiwa na Taasisi husika.

Sura hii, inatoa majumuisho ya taarifa za usimamizi wa ununuzi na mikataba katika Mashirika naTaasisi za Umma zilizoonekana kuwa ni muhimu kutolewa taarifa. Ukaguzi wa ununuzi na mikataba ulifanyika sambasamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2013, 31 Disemba, 2013 na 30 Juni, 2014. Matokeo ya ukaguzi wa ununuzi na mikataba iliyoingiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yameainishwa ndani ya sura hii.

### 5.1 Usimamizi wa Ununuzi

Kulingana na kifungu Na. 3 cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 ununuzi unamaanisha kununua, kukodisha, kupata bidhaa, ujenzi au huduma inayofanywa na taasisi kwa kutumia fedha za umma, kwa niaba ya Wizara au Idara ya Serikali au Shirika la Umma na ikijumuisha kazi zote zinazohusiana na upatikanaji wa bidhaa au huduma ikiwa ni pamoja na kuainisha mahitaji, kuteua na kutangaza zabuni na kutoa mikataba. Yafuatayo ni mambo ambayo yalionekana kuwa na kasoro kwenye kaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

#### 5.1.1 Muundo Usio Sahihi wa Bodi ya Zabuni

Kifungu Na. 2 (1) katika jedwali la pili la Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinaelekeza namna ya uundwaji wa Bodi ya Zabuni kwamba patakuwepo na mwenyekiti, wajumbe 6 ambao ni wakuu wa vitengo au idara na katibu ambaye ndiye Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi.

Mapitio ya muundo wa Bodi ya Zabuni katika Mamlaka ya Udhibiti wa Soko la Hisa na Mitaji (CMSA) yalibaini kwamba Bodi ya Zabuni katika Mamlaka hii imeundwa na wajumbe watano (5) badala ya wajumbe nane (8) kama Sheria inavyoelekeza.

### 5.1.2 Mapungufu ya Kiutendaji katika Vitengo vya Ununuzi

Katika ukaguzi wangu nilihakiki ubora wa utendaji kazi wa vitengo vya ununuzi katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kama inavyobainishwa katika kifungu Na. 38 cha Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011. Katika uhakiki huu nilibaini kuwa, Kitengo cha Ununuzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza hakikutimiza wajibu wake wa kusimamia ununuzi katika Mamlaka.

Kitengo hiki kilianzishwa tangu mwaka 2010 kikiwa na wajumbe 5 wote wakiwa ni wataalamu wa fani ya ununuzi. Muundo huu ni kinyume na matakwa ya Kifungu Na. 37 (2) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinachovitaka vitengo vya Ununuzi kuwa na mchanganyiko wa wajumbe katika fani za taaluma nyinginezo ikiwa ni pamoja na fani ya utawala. Kasoro hii ilipelekea kitengo kutofanya vizuri katika maeneo ya kutunza kumbukumbu za ununuzi, udhibiti wa ununuzi, mgawanyo wa majukumu, taratibu za zabuni, uandaaji wa taarifa za ununuzi, kutokuwa na umakini katika kuandaa mpango wa ununuzi na mapungufu katika kutunza kumbukumbu za taarifa za Bodi ya Zabuni, kutokushirikishwa kwa watumiaji katika mchakato mzima wa ununuzi kulikopelekea ununuzi yasiyokidhi viwango na kucheleweshwa kutangazwa kwa zabuni. Mapungufu haya yalikwenda kinyume na kifungu Na. 38 cha Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinachoelezea majukumu ya Kitengo cha Ununuzi.

Katika ukaguzi wa Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania, nilibaini kuwa majukumu ya Kitengo cha Ununuzi yanachanganywa na majukumu mengine kama vile utunzaji wa bohari na shughuli za usafirishaji. Kwa utendaji huu nilibaini kuwa Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi anawajibika moja kwa moja kwa mtendaji mkuu lakini watumishi walio chini yake wanawajibika kwa Mkuu wa Idara ya Fedha kupitia Meneja wa Fedha. Kwa utaratibu huu nilibaini kuwepo kwa Meneja wa Usafirishaji na Usambazaji chini ya Kitengo cha Ununuzi ambapo kazi yake ni kununua na kukabidhi bidhaa kwa Boharia. Utaratibu huu ulipelekea ununuzi ya takribani Shilingi za Kitanzania milioni 971.2 ambayo hayakupitishwa na Kitengo cha Ununuzi kinyume na matakwa ya kifungu Na. 34 na Na.35 cha Sheria ya Ununuzi Na.21 ya mwaka 2004 (Kifungu Na.37 cha Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011).

Mapungufu ya kiutendaji yalibainika pia katika ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ambapo kitengo cha Ununuzi kilikuwa na mtumishi mmoja tu. Kadhalika, hali kama hiyo ilibainika katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Baraza la Taifa la

Mazingira (NEMC) ambapo licha ya kuwa na mtumishi mmoja pia hakuwa na weledi katika fani ya ununuzi.

### 5.1.3 Mazingira ya Kutatanisha katika Utoaji wa Zabuni ya Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.4

Ukaguzi wangu wa michakato ya ununuzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza nilibaini kuwa Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ilipitisha maamuzi ya kutoa zabuni ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mamlaka kwa Mkandarasi tofauti na aliyependekezwa na Kamati ya Tathmini.

Kwa mujibu wa ripoti ya Kamati ya Tathmini, Mkandarasi aliyependekezwa alikuwa ni Ngogo Engineering Ltd kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.4. Mapendekezo haya yalikubaliwa na Kitengo cha Ununuzi na kupelekwa kwenye Bodi ya Zabuni lakini Bodi katika kikao chake cha 112 iliyakataa mapendekezo haya na kutoa zabuni kwa kampuni ya DF MISTRY bila kutoa sababu za uamuzi huo. Kwa maamuzi hayo, Bodi ya Zabuni ilikiuka Kanuni Na. 52 (1) ya Tangazo la Serikali Na.446 la Kanuni za Ununuzi za Mwaka 2013. Kanuni hizi zinaielekeza Bodi ya Zabuni kwamba endapo haitaridhika na mapendekezo ya Kitengo cha Ununuzi juu ya zabuni yeyote, irejeshe kwa maandishi mapendekezo yaliyopendekezwa ili yapitiwe upya. Endapo Bodi ya Zabuni haitaridhika na mapendezo yatakayotolewa, suala hili liwasilishwe kwa Afisa Masuuli/Mkuu wa Taasisi husika na endapo halitapata ufumbuzi shauri hili liwasilishwe kwenye Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi Tanzania kwa mashauriano zaidi.

### 5.1.4 Utoaji wa Zabuni katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza bila Kuzingatia Uthibitisho wa Ulipaji Kodi kwa Mkandarasi Shilingi za Kitanzania Bilioni 4.4

Ni matakwa ya kisheria kuwa mkandarasi yeyote au mtoa huduma au mnunuzi wa mali ya serikali kwa njia ya zabuni anatakiwa kuwa na cheti cha uthibitisho wa ulipaji kodi, ikiwa ni pamoja na uthibitisho wa uwasilishwaji wa makato ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Pia, ni lazima kampuni au mtu husika athibitishe kuwa anazingatia Sheria ya mazingira, Sheria ya kazi na matakwa ya Sheria ya hali bora na usalama kazini. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni Na.14 (1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi za Mwaka 2005.

Ukaguzi wa mikataba 10 yenye jumla ya thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 4.4 iliyoingiwa kati ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza na Wazabuni ulibaini ukiukwaji wa sheria ya ununuzi kwa kifungu tajwa hapo juu. Wazabuni hawa walishindwa kuwasilisha kwenye Mamlaka vyeti vya uthibitisho wa ulipaji kodi toka Mamlaka ya Mapato Tanzania kama uthibitisho kuwa wana wajibu wa kulipa kodi.

### 5.1.5 Ununuzi ya Gari katika Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam bila Kufuata Vigezo vilivyowekwa Shilingi za Kitanzania milioni 53.9

Mapitio ya nyaraka mbalimbali za ununuzi katika Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam yalibaini ununuzi ya gari lenye namba ya usajili SU 39949 Nisan X 37 lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania milioni 53.9 bila kuzingatia vigezo vilivyopitishwa na Chuo. Nyaraka za zabuni ziliainisha kuwa gari husika lilitakiwa liwe na milango inayoendeshwa kwa umeme (Automatic) na pia liwe na tairi zenye ukubwa wa 255/70 R15. Kinyume na matakwa hayo, Mzabuni alikipatia Chuo gari lenye milango isiyoendeshwa kwa umeme na tairi zenye ukubwa wa 255/70 R na sio 255/70 R15. Mapungufu haya yanaashiria kwamba Chuo hakikukagua gari husika kuhakiki ubora na vigezo viilivyokubalika kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 244 na 245 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2013. Kanuni hizi zinaelekeza kwamba kila Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma inayofanya ununuzi, ni lazima ateue kamati itakayohakiki ubora wa mali iliyonunuliwa na kujihakikishia kwamba vigezo vilivyowekwa vimetimizwa kikamilifu kwa mujibu wa mkataba. Kinyume na hapo, bidhaa au mali iliyonunuliwa irejeshwe kwa Mzabuni ndani ya siku saba.

### 5.1.6 Mapungufu katika Utunzaji wa Kumbukumbu za Ununuzi.

Kifungu Na. 38 (1) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kinavitaka Vitengo vya Ununuzi kutunza kumbukumbu zote zinazohusiana na ununuzi na mauzo ya mali za Serikali katika hali inayoridhisha. Kadhalika, kanuni Na. 88 (4) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi Na.446 ya Mwaka 2013 inaelekeza kwamba kumbukumbu zote za ununuzi zinatakiwa kutunzwa katika hali ya ubora ili kurahisisha marejeo ya kumbukumbu husika pindi zitakapohitajika. Kinyume na matakwa haya, katika ukaguzi wangu nilibaini baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo hazikutunza vyema kumbukumbu zake zinazohusiana na ununuzi kama inavyoelekezwa na mwongozo wa utunzaji kumbukumbu uliotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi Tanzania (PPRA).

Haya yalibainika katika ukaguzi wa Kampuni ya Ubungo Plaza ambapo mafaili ya kumbukumbu za zabuni hayakuwa yametunzwa vyema kwenye majalada husika. Mtiririko wa kumbukumbu za ununuzi kuanzia ununuzi ulipoanzishwa hadi mikataba ilipotiwa saini haukuwa mzuri. Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, kasoro zilibainika katika utunzaji wa kumbukumbu zinazohusiana na zabuni mbalimbali hali iliyosababisha ugumu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa ununuzi. Hali kadhalika, ukaguzi wa Chuo Kikuu Dodoma, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ulibaini kasoro za kutokutunzwa kwa nyaraka za kumbukumbu za zabuni kama Sheria inavyoelekeza.

### 5.1.7 Mapungufu katika Uandaaji na Uidhinishaji wa Mpango wa Ununuzi

Kwa mujibu wa kifungu Na. 49(2)-(3) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2011, Mamlaka ya uidhinishaji wa bajeti inatakiwa kuidhinisha mpango wa ununuzi kwa kuzingatia bajeti ya mwaka husika. Kifungu hiki kinasisitiza zaidi kwamba mpango wa ununuzi ni lazima uzingatiwe na ununuzi yoyote nje ya mpango wa ununuzi usifanyike kabla ya kupata kibali cha Afisa Masuuli.

Katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO), nilibaini kuwa shirika liliandaa mpango wa ununuzi wa mwaka lakini mpango huu haukuidhinishwa na mamlaka ya uidhinishaji wa bajeti yaani Bodi ya Wakurugenzi. Kadhalika, nilibaini ucheleweshaji wa matangazo ya zabuni kinyume na matakwa ya Sheria ambapo mpango wa mwaka wa ununuzi ulitangazwa mwezi Mei, 2013 miezi mitano baada ya kuanza mwaka wa fedha. Hii, inabainisha kuwa baadhi ya zabuni zilitekelezwa bila kutangazwa kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 18 na 19 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma ya tangazo la Serikali Na 446 za mwaka 2013.

Ukaguzi wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) ulibaini ununuzi wa kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 45.7 nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu cha 45 cha Sheria ya ununuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni ya 25(3) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma ya tangazo la Serikali Na.97 la Mwaka 2005. Kanuni hii inazitaka Taasisi za Umma kuandaa mpango wa ununuzi kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo ndani ya mpango mkakati. Pia, nilibaini kutokukamilika kwa wakati kwa mpango wa ununuzi katika Kampuni ya Ubungo Plaza ambapo mpango wa ununuzi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2013 ulikamilika mwezi Machi, 2013. Kutokana na ucheleweshwaji huu Kampuni iliendelea kutekeleza shughuli zake za ununuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza

ya mwaka wa fedha bila kuwa na mpango wa ununuzi. Licha ya kuchelewa, mpango huu wa ununuzi haukuweza kukidhi mahitaji yote ya ununuzi kwa mwaka na hivyo kupelekea baadhi ya ununuzi kufanyika nje ya mpango wa ununuzi kinyume na Kanuni Na. 69 (1) (b) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446).

Tatizo la ucheleweshwaji wa uandaaji wa mpango wa ununuzi lilijitokeza pia katika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania (VETA) kituo cha Kagera ambapo mpango huu uliidhinishwa tarehe 22 Agosti, 2013 miezi miwili baada ya kuanza kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Katika Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania- Huduma za Kifedha (UTT-MFI) ukaguzi ulibaini kuwa kampuni hii haikuandaa mpango wa ununuzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2014 kinyume na Kifungu Na. 49(1) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011. Hali kadhalika, ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza na Chuo Kikuu cha Dodoma ulibaini mapungufu ya uaandaaji wa mpango wa ununuzi ambapo Mamlaka ya Mwanza ilinunua bidhaa zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 151.7 ya mpango wa ununuzi wakati Chuo Kikuu cha Dodoma mpango wa ununuzi ulionyesha kasoro mbalimbali za kimsingi kama vile ukosefu wa namba za zabuni, kutokuonyesha muda wa kutekeleza zabuni na kutokuainishwa kwa mafungu (Lot) ya zabuni Pia ilibainika kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma hakikutangaza fursa za ununuzi kwenye mtandao wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi (PPRA) kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446).

Ukaguzi wa Mfuko wa Pensheni wa LAPF ulibaini kuwepo kwa ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2014. Ununuzi huu ulihusisha kandarasi ya ununuzi wa huduma za ushauri juu ya uandaaji wa michoro ya ofisi mpya za Makao Makuu katika jengo la Millenium Tower - Dar es Salaam iliyopewa zabuni Na. PA. 095/HQ/2012/2013/c/21 na Ukarabati wa majengo 8 katika kitalu ‘B’ yaliyoko eneo ‘D’ Manispaa ya Dodoma iliyopewa zabuni Na.PA095/HQ/2013/2014/w/01. Ukaguzi huu pia ulibaini ununuzi ya thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 12.41 katika Benki Kuu ya Tanzania nje ya mpango wa ununuzi.

### 5.1.8 Ununuzi yanayozidi Ukomo na Yasiyo na Ushindani

Kwa mujibu wa kifungu Na. 31(3) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 taasisi yeyote ya Umma hairuhusiwi kufanya ununuzi zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na sheria kwa kila aina ya zabuni.

Katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) tulibaini uwepo wa zabuni ambazo thamani ya ununuzi yake ilizidi kiwango kilichopitishwa kisheria kwa aina ya zabuni za namna hiyo. Licha ya kukiuka viwango vya ununuzi Shirika halikutoa taarifa ya matumizi yaliyozidi kiwango kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi Tanzania (PPRA) ndani ya siku 14 kuanzia siku zabuni husika zilivyoanza kutekelezwa. Mifano ya zabuni zilizotekelezwa zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali 8: Zabuni zilizotekelezwa zaidi ya ukomo uliowekwa kisheria**

| Namba ya Zabuni | Njia iliyotumika | Gharama ya Zabuni (Sh.) | Viwango vya ukomo vilivyoidhinishwa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| PA/001/13 /HQ/N/004 | Ushindani wa ndani (NCB) | 3,872,833,802 | Milioni 500 | 3,372,833,802 |
| PA/001/12 /HQ/G/008 | Ushindani wa ndani (NCB) | 2,030,173,176 | Milioni 800 | 2,029,373,177 |

Katika ukaguzi wa hesabu za Kampuni ya Simu Tanzania nilibaini ununuzi yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.442 bila kuzingatia viwango vya ukomo vilivyoainishwa kwenye jedwali la pili la Kanuni za Sheria ya Ununuzi Tangazo la Serikali Na.97 na 98 la mwaka 2005. Ukiukwaji huu wa matakwa ya kisheria haukupata idhini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi (PPRA) kama inavyoelekezwa na kifungu cha 31(3) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004. Zabuni hizi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali 9: Zabuni zilizotekelezwa kinyume na matakwa ya sharia ya Ununuzi wa Umma**

| Na. | Namba ya Zabuni | Njia ya ununuzi | Kikomo (Sh.) | Gharama za ununuzi (Sh.) | Kiwango kilichozidi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PA/032/13/HQ/G/010 | Njia isiyo ya ushindani (SS) | Milioni 500 | 699,532,608 | 199,532,608 |
| 2 | PA/032/13/HQ/W/003 | Zabuni maalum (RT) | Milioni 500 | 1,579,100,800 | 1,097,100,800 |
| 3 | PA/032/13/HQ/NC/004 | Zabuni maalum (RT) | Milioni 200 | 381,966,107 | 181,966,107 |
| 4 | PA/032/13/HQ/G/016 | Zabuni maalum (RT) | Milioni 500 | 781,308,960 | 281,308,960 |
| **Jumla** | | | | **3,441,908,475** | **1,741,908,475** |

### 5.1.9 Ununuzi Usiozingatia Ukomo wa Bajeti

Kwa mujibu wa kifungu Na. 54(2(d)) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni Na. 20(2 (e)) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97) inazitaka zabuni za aina yeyote ile ambazo thamani yake inazidi kiwango kilichoidhinishwa kwenye bajeti zikataliwe. Pia kanuni Na. 62 (1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97) inasisitiza kwamba kabla ya kutekeleza zabuni yeyote ni lazima watendaji wa taasisi husika wahakikishe kuwa tathmini ya zabuni inazingatia kiasi cha fedha kilichotengwa kwenye bajeti.

Kinyume na matakwa haya, katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) nilibaini uwepo wa ununuzi wa takribani Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.2 kupitia zabuni Na.PA/001/13/HQ/H/106 bila kuzingatia kiasi kilichotengwa kwenye bajeti yaani Shilingi za Kitanzania Milioni 400. Katika zabuni nyingine Na.PA/001/13/HQ/H/G/106 TANESCO waliingia mkataba wa Shilingi za Kitanzania milioni 340.8 ambayo ni zaidi ya bajeti iliyotengwa ya Shilingi za Kitanzania milioni 154. Ukaguzi huu haukuweza kupata ushahidi wa kuwepo kwa marejeo ya bajeti kwa kiasi kilichotumika nje ya makisio.

### 5.1.10 Kutokuwepo kwa Muda wa Kutosha katika Kuandaa na Kuwasilisha Nyaraka za Zabuni

Wakati wa ukaguzi katika Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) nilibaini uwepo wa tangazo la zabuni Na.PA/001/13/HQ/N/030 yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 1.94 lililotangazwa tarehe 17 Juni, 2013. Zabuni hii ilitangazwa kwenye gazeti la Guardian ambapo mwisho wa kupokea zabuni ilikuwa tarehe 26 Julai, 2013 siku 39 kutoka tarehe tangazo lilipotangazwa. Muda huu ni mfupi ukilinganisha na muda uliowekwa kisheria katika jedwali la tatu la Kanuni ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97). Mapitio ya zabuni Na.PA/001/13/HQ/N/023 iliyotangazwa na TANESCO pia yalibaini kutotolewa kwa muda wa kutosha kwa Wazabuni kuwasilisha maombi ya zabuni. Ukaguzi huu ulibaini kuwa tangazo la kuitisha zabuni lilitolewa tarehe 17 Aprili, 2013 na mwisho wa kupokea zabuni ulikuwa tarehe 30 Aprili, 2013 yaani siku 13 tangu tarehe ya kuitisha zabuni. Kwa mujibu wa jedwali la tatu la Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97) muda uliowekwa ni siku 21. Kadhalika, zabuni Na.PA/001/13/HQ/G/104 iliitishwa tarehe 13 Machi, 2013 na kuwekewa muda wa mwisho tarehe 22 Machi, 2013 sawa na siku 9 tu. Muda huu ni mfupi ukilinganisha na muda wa siku 21 uliowekwa kisheria.

Kwa mujibu wa zabuni zilizotajwa hapo juu, mnamo tarehe 19 Machi, 2013 TANESCO ilifanya marekebisho ya nyaraka za zabuni kuhusiana na zabuni tajwa bila kuzingatia kipengele cha muda. Maamuzi haya ni kinyume na matakwa ya Kifungu Na. 61(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni Na. 65(4),74(8) na 80(6) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97). Vifungu hivi vinaelekeza kuwa Wazabuni ni lazima wapewe muda wa kutosha kuandaa na kuwasilisha nyaraka za zabuni.

### 5.1.11 Matumizi ya Njia ya Ununuzi bila Kuzingatia vigezo Vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake

Ukaguzi wa zabuni mbalimbali katika Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), uilibaini kuwa Kampuni ilitumia njia ya zabuni zuifu (Restricted Tendering) kuwapata Wakandarasi bila kufuata vigezo vilivyoainishwa na Sheria ya Ununuzi wa mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

Katika mapitio ya zabuni Na.PA/032/13/HQ/W/003 iliyohusu mradi wa ununuzi na ujengaji wa minara, uzio, vyoo na kibanda cha mlinzi wenye thamani ya Dola za Kimarekani 986,938 nilibaini kuwa Kampuni ilitumia njia ya ununuzi wa zabuni zuifu bila kuzingatia matakwa ya

Kanuni ya 152 (a) hadi (d) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446). Mapungufu haya yalionekana pia katika zabuni Na.PA/032/13/HQ/NC/004 juu ya utoaji wa huduma za ulinzi kwenye majengo ya Shirika yaliyoko Kanda ya Kaskazini - Dar es Salaam na Ex Telecom yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania milioni 381.9. Kadhalika, ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ulibaini ununuzi uliofanyika kwa njia ya Zabuni Zuifu kwenye zabuni Na AE/055/2013-14/HQ/G/08 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.963 na zabuni Na.AE/055/2013-14/HQ/G/60 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania milioni 320.1. Ununuzi huu haukuzingatia Kanuni Na. 152 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446).

Katika ukaguzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara (MUCCOBs) nilibaini matumizi ya njia ya ununuzi wa chanzo kimoja (Singo source) bila kuzingatia matakwa ya Kanuni Na. 159 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa mwaka 2013.

### 5.1.12 Kutokutangazwa kwa Fursa za Zabuni katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446) inazitaka Taasisi za Umma pindi zinapotaka kununua bidhaa, kandarasi au huduma kuandaa mpango wa mwaka wa ununuzi na kuutangaza kwenye gazeti la Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi. Wakati wa mapitio ya zabuni mbalimbali zilizofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma nilibaini kuwa Chuo hakikuandaa mpango mkuu wa ununuzi na kuupeleka kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi kwa matangazo. Kasoro hii ilizuia wazabuni kufahamu fursa za ununuzi zilizokuwepo katika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa mwaka 2013/2014.

### 5.1.13 Kasoro katika Zabuni Chuo Kikuu cha Dodoma Shilingi za Kitanzania 603,185,320

Ukaguzi wa shughuli za ununuzi katika Chuo Kikuu cha Dodoma ulibaini kasoro katika utekelezaji wa zabuni ya ujenzi wa maabara na uwekaji wa samani uliogharimu Shilingi za Kitanzania 603,185,320.00. Mradi huu ulitekelezwa na Kampuni ya Jafar Ind.Sain Ltd ya Dar es Salaam.

Mapitio ya kumbukumbu za zabuni hii yalibaini kutokuzingatiwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 katika maeneo ya kutoa mrejesho kwa Bodi ya Zabuni, kutokuwepo kwa nyaraka za kuanzisha ununuzi ambao haukuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Kasoro hizi ni kinyume na Kifungu Na. 36 (b) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya mwaka 2011.

Kasoro nyingine ilihusiana na idadi ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni ambapo kama ilivyoainishwa na Kanuni ya 56 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446) wajumbe walioshiriki walikuwa 8 badala ya wanne (4). Kasoro nyingine iliyojitokeza ni kutojulishwa kwa Wazabuni walioshindwa jina la Mzabuni aliyeshinda na kupewa mkataba ambapo ni kinyume na Kifungu cha 60 (14) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya 2011 na Kanuni ya 235 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013. Pia nilibaini kuwa Chuo hakikuteua kamati za ukaguzi wa bidhaa kabla ya kupokelewa ili kujiridhisha na ubora wake. Hii ni kinyume na Kanuni ya 144 na 245 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446).

### 5.1.14 Ununuzi kwa kutumia Mkataba wa Ununuzi Mdogo Mdogo (LPO) na Masurufu (Imprest) bila Kuzingatia Ukomo Uliowekwa Kisheria

Katika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma juu ya utekejelezaji wa Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 nilibaini ununuzi yaliyofanyika kwa njia ya LPO na Masurufu bila kuzingatia ukomo wa thamani ya zabuni. Jedwali la saba katika Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 limeweka ukomo wa viwango vya ununuzi kwa kutumia LPO kuwa ni kati ya Shilingi za Kitanzania milioni 10 na milioni 20. Aidha kwa upande wa ununuzi kwa kutumia masurufu, zabuni haitakiwi kuzidi Shilingi za Kitanzania milioni 5.

Hata hivyo katika ukaguzi wa nyaraka za ununuzi katika Chuo Kikuu Dodoma nilibaini ununuzi wa takriban Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.237 ambayo yalifanywa kwa kutumia LPO. Katika nyaraka za malipo kwa watoa huduma zilizofanyiwa uhakiki ilibainika kuwa malipo kwa kila hati yalizidi viwango vilivyoainishwa kwenye sheria tajwa hapo juu. (Rejea kiambatisho cha VI).

Katika ukaguzi wa Taasisi ya Tekinologia Dar es Salaam (DIT), ukaguzi ulibaini ununuzi wa Shilingi za Kitanzania Milioni 148.8, TAFIRI Shilingi za Kitanzania Milioni 162.2 na TANAPA Shilingi za Kitanzania milioni 60.9 kwa kutumia njia ya masurufu (imprest). Kiwango kilichoidhinishwa hapa ni Shilingi za Kitanzania milioni 5 tu, zaidi ya hapo ununuzi huu unapaswa kufuata mchakato wa zabuni.

### 5.1.15 Kasoro zilizobainika Katika Utoaji wa Zabuni Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mapitio ya shughuli za ununuzi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania yalibaini uvunjifu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 kama ifuatavyo:-

### 5.1.15.1 Mkataba wa Ununuaji, Ujengaji na Mafunzo juu ya Mtandao wa Electronic Single Window System (ESWS) Euro Milioni 5.04

Zabuni hii ilitolewa kwa Kampuni ya Phaeros Group BVBA kwa garama ya Euro Milioni 5.04. Mapitio ya nyaraka za ununuzi ulibaini uwepo wa ucheleweshwaji katika kuwajulisha wazabuni walioshindwa kwenye ushindani kinyume na Kifungu Na. 71(4) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004 na pia Kanuni Na. 17(1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma za mwaka 2005. Katika mkataba huu wazabuni walioshindwa walipewa taarifa tarehe 10 Februari, 2014 baada ya mkataba kutiwa saini. Pia, ilibainika kuwa baadhi ya barua kwa wazabuni hazikuwafikia na hivyo kusababisha baadhi ya wazabuni kupeleka malalamiko kwenye Mamlaka ya Rufaa ya Ununuzi wa Umma (Public Procurement Appeal Authority) kesi iliyopewa Na.37 na 40 ya mwaka 2013/2014.

Utoaji wa zabuni hii kwa Kampuni ya Phaeros Group BVBA ulifanyika bila kuzingatia thamani ya fedha kwa kuwa mapendekezo ya Kamati ya Tathmini juu ya Mzabuni aliyenukuu bei ndogo haukuzingatiwa. Kwa mujibu wa Kamati ya Tathmini mzabuni aliyenukuu bei ndogo na kupendekezwa na kamati alikuwa ni Web Fountaine kwa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 6.2 dhidi ya Mzabuni aliyepewa kazi hii kwa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 8.37. Uamuzi huu ulikwenda kinyume na Kifungu Na. 43 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni Na. 90(4) hadi (5) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2005 pia kifungu Na.35.1 cha nyaraka za zabuni ambazo zinaelezea kuwa Mzabuni atakaye nukuu bei ndogo na akakidhi vigezo vilivyowekwa ndiye apewe kazi.

Hali kadhalika, nilibaini kuwa vigezo vya ushindani vilivyowekwa kati ya 80% na 20% katika masuala ya kiufundi na kifedha vilikuwa ni kinyume na vile vilivyokuwa kwenye nyaraka za zabuni. Baada ya mapitio ya ripoti ya Mamlaka ya Rufaa za Ununuzi (PPAA) nilibaini kuwa vigezo hivi vilichomekwa wakati wa zoezi la tathmini ya zabuni. Kwa maamuzi haya Mamlaka ya Bandari ililipa gharama zisizo za lazima kutokana na rufaa iliyokatwa na Kampuni ya Web Fontaine dhidi ya maamuzi ya Bodi ya Zabuni. Kwa upande wake Bodi ya Rufaa ya Ununuzi wa Umma iliamuru Mamlaka ya Bandari (TPA) kulipa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 40. Ukaguzi huu haukuweza kubaini hatua zilizochukuliwa kwa watendaji waliokiuka Sheria ya Ununuzi katika suala hili.

**5.1.15.2 Kandarasi ya Kusawazisha na Kushindilia Eneo la Ardhi katika Bandari ya Dar es Salaam-'Gerezani Creek Marshalling' Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.236**

Zabuni hii ilitolewa kwa Kampuni ya Ruvuma Contractors and Supply Limited kwa mkataba wa Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.236. Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa hapakuwepo na maombi ya kuanzisha mradi toka Bandari ya Dar es Salaam ambayo ndio mhusika wa mradi huu. Kwa mujibu wa kifungu cha 39(1) (b-d) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 kinaelekeza kwamba, (b) maombi ya utekelezaji wa mradi au uanzishaji wa ununuzi unapaswa kufanywa na idara au kitengo husika kupitia Kitengo cha Ununuzi; (c) mwenye mradi kuandaa hadidu rejea na; (d) kuandaa vigezo vya kitaalamu kwa mradi husika na kuviwasilisha kwenye Kitengo cha Ununuzi. Kwa mujibu wa mapitio ya mradi huu wahusika wa mradi huu (User departments) hawakuhusishwa kikamilifu katika mchakato wa ununuzi.

**5.1.15.3 Kuhamisha na Kufunga Tishari (Floating Dock) toka Bandari ya Mwanza kwenda Bandari ya Kyela Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.994**

Zabuni hii ilitekelezwa na Kampuni ya Songoro Marine Transport Ltd kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.994. Mapitio yangu katika nyaraka za ununuzi yalibaini kwamba zabuni hii ilitolewa kwa Mkandarasi (Songoro Marine Transport Ltd) ambaye hakukidhi vigezo vya awali. Katika hatua ya pili ya tathmini ya zabuni, Kamati ya Tathmini ilibaini kwamba Mzabuni aliyebaki baada ya uchambuzi wa kina hakukidhi viwango hivyo na hivyo kupendekeza zabuni itangazwe upya jambo ambalo liliridhiwa na Bodi ya Zabuni kwenye mkutano wake wa kawaida wa 94 uliofanyika tarehe 20/2/2014. Hata hivyo, licha ya mapendekezo ya Bodi ya Zabuni, Mamlaka ya Bandari haikutangaza upya zabuni hii badala yake iliomba ufafanuzi toka kwa Mkandarasi (Songoro Marine Transport Ltd). Kitendo hiki ni kinyume na Kanuni Na. 90 (16) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97). Kanuni hii inaelekeza kwamba kama nyaraka za zabuni zilizowasilishwa haziendani na zabuni husika iliyotangazwa nyaraka hizi hazitokubaliwa na taasisi husika na haitaweza kuingia kwenye ushindani kwa kufanya masahihisho ya eneo lenye utata au kwa kuondoa kipengele chenye shida. Kadhalika, Kifungu Na. 35(2) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinafafanua zaidi kwamba 'hakuna mtu yeyote au kampuni itakayoruhusiwa kuingia mkataba na taasisi ya Umma bila ridhaa ya Bodi ya Zabuni'.

#### 5.1.15.4 Ununuzi ya Huduma za Ushauri Kwa Ajili ya Kuboresha Bandari katika Ziwa Victoria Euro 589,174

Katika ukaguzi wa mwaka 2013/2014, nilibaini kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia mkataba na Kampuni ya Haskoning DHV Nederland B.V kufanya upembuzi na kubuni namna nzuri ya kuboresha bandari za Ziwa Victoria (Mwanza, Musoma na Bukoba) kwa gharama ya Euro 589,174. Uchambuzi wa zabuni hii ulibaini kasoro kadhaa ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa kumbukumbu za kikao cha kufungua zabuni; kumbukumbu za nukuu za bei za zabuni zilizosomwa siku ya ufunguzi pamoja na orodha ya wajumbe waliohudhuria ufunguzi wa zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni Na.199 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446). Pia, Mamlaka haikuweza kuthibitisha kwamba Wazabuni walioshindwa walijulishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 71 (4) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni Na.17(1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2005.

#### 5.1.15.5 Zabuni ya Ununuzi wa Huduma ya Ushauri kwa Ajili ya kufanya Upembuzi yakinifu Juu ya Maradi wa Kujenga Bandari Kavu katika Eneo la Kisarawe Euro 248,000

Zabuni hii ilitolewa kwa Kampuni ya Haskoning DHV Nederland B.V kwa gharama ya Euro 248,000. Uhakiki wangu katika kutekeleza Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake ulibaini kuwa Bodi ya Zabuni na Afisa Masuuli hawakuidhinisha nyaraka za zabuni na pia tangazo la fursa za zabuni kinyume na kifungu Na. 33(1) (c) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011. Kifungu hiki kinasisitiza kwamba ni lazima nyaraka za zabuni ziidhinishwe na Bodi ya Zabuni katika Taasisi husika. Pia, kifungu Na. 35 (1) (a) cha Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinakataza mtu yeyote ambaye si Afisa Masuuli kutoa matangazo ya zabuni, kuitisha zabuni au kuitisha kusudio la kutangaza zabuni. Kadhalika, Kanuni ya 181(4) na Kanuni ya 185(1) kwa pamoja zinataka nyaraka za zabuni ziidhinishwe na Bodi ya Zabuni kabla ya kutangazwa gazetini.

Nilibaini pia kwamba mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na ukweli kwamba Mamlaka ya Bandari Tanzania haikuwa na umiliki halali wa eneo la Kisarawe ambalo mradi huu ulitakiwa kufanyika. Juhudi za kupata umiliki halali wa ardhi ya Kisarawe zilikwamisha kuanza kwa mradi na hivyo kupelekea Mamlaka kusogeza mbele muda wa kupokea zabuni. Hadi kipindi cha kukamilisha ukaguzi katika Mamlaka hii tarehe 16/10/2014 umiliki halali wa ardhi ulikuwa haujapatikana ingawa mkataba wa kuanza kazi kwa Mkandarasi Mshauri ulishatiwa saini tarehe 17/09/2014.

### 5.1.15.6 Mkataba wa Ununuzi wa 'Terminal Tractor No.12' Katika Bandari ya Dar es Salaam Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.735

Ukaguzi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania ulibaini kuwepo kwa mkataba kati ya Kampuni ya Eristic (T) Investment Limited juu ya Ununuzi wa 'Terminal Tractor No.12' kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.735. Mapitio ya kina kwenye mkataba huu yalibaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

Ukaguzi huu ulibaini kwamba, awali kandarasi hii ilitolewa kwa kampuni ya Achelis & Shne Gmbh kwa gharama ya Euro Milioni 1.224 licha ya kuwa hakushinda kwenye uchambuzi wa awali kwa mujibu wa Kamati ya Tathmini ya Zabuni. Wakati jitihada za kuidhinisha zabuni hii zikiendelea Kitengo cha Ununuzi kupitia Waraka Na.48/2014 kiliwasilisha maoni tofauti na yale ya Kamati ya Tathmini iliyopelekea Bodi ya Zabuni kufanya upya tathmini ya zabuni hii katika kikao chake cha kawaida Na. 941 kilichofanyika Machi 2014. Ripoti ya pili ya tathmini ilipendekeza zabuni hii ipewe Kampuni ya MOL Transport Solution kwa gharama ya Euro Milioni 1.1. Hata hivyo Kitengo cha Ununuzi hakikuridhia mapendekezo haya na hivyo kumwandikia Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni kupitia Waraka Na.99 kwa kupendekeza zabuni hii itolewe kwa Kampuni ya Eristic Ltd kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.735 mapendekezo yaliyoridhiwa na Bodi ya Zabuni. Maamuzi haya yalitolewa kwa kigezo kwamba suala la Kampuni ya Eristic (T) Investment Limited kutokuwa na cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi na kushindwa kukidhi vigezo vya uendeshaji havikuwa na nguvu kisheria.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mamlaka ya Rufaa za Ununuzi wa Umma (PPAA) iliyotokana na malalamiko yaliyowasilishwa na Kampuni ya Kihelya Auto Tractor co.Ltd, maoni ya Mamlaka (PPAA) ni kuwa kukosekana kwa cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi ni mapungufu ya msingi tofauti na maoni yaliyotolewa na Kitengo cha Ununuzi. Pia nilibaini kwamba kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni kilichotumika kubadili bei ya mkataba ya Kampuni ya MOL Transport Solution dhidi ya bei iliyoonyeshwa na Kampuni ya Eristic Ltd hakikuwa sahihi. Bei iliyoonyeshwa na Kampuni ya Eristic Limited ilikuwa Shilingi za Kitanzania 1,735,000,000 dhidi ya Shilingi za Kitanzania 2,913,157,298.64 iliyoonyeshwa na Kampuni ya MOL Transport Solution baada ya kubadilisha Euro 1,100,056 kwa Shilingi za Kitanzania 1,648.19 kwa Euro 1. Kiwango cha ubadilishaji fedha kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania kwa tarehe hiyo hiyo ilikuwa Shilingi 2,243.5 kwa Euro 1.

Kama hii haitoshi Mamlaka ya Bandari Tanzania ilichukua maamuzi ya kutoa zabuni kwa Kampuni ya Eristic Limited huku ikijua kwamba kuna malalamiko yaliyopelekwa PPRA na Kampuni ya Kihelya Auto Limited kuhusiana na zabuni hii. Hali hii ilipelekea PPRA kutoendelea na mapitio ya maamuzi ya zabuni hii yaliyofanywa na Mamlaka na hivyo kuwasilisha malalamiko haya kwenye Mamlaka ya Rufaa za Ununuzi wa Umma (PPAA). Matokeo ya rufaa yalikuwa kwamba tathmini ya zabuni hii haikufuata Sheria ya Ununuzi wa Umma hivyo kupelekea Mamlaka ya Bandari kuamriwa imlipe Kihelya Auto Co.Limited fidia ya Shilingi 20,000,000 na kwamba mlalamikaji awasilishe malalamiko yake Mahakama Kuu.

**5.1.15.7 Zabuni ya Ununuzi wa 'Cargo Handling Gears' baina ya Mamlaka na 'Mpomabiva Investment Ltd'.**

Mapitio ya zabuni Na.AE/016/2013-14/DSM/G/43 juu ya ununuzi wa 'Cargo Handling Gears' chini ya 'Frame work Contract' ilibainika kwamba bei ya mkataba ilikuwa juu zaidi ya bajeti kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania 288,309,880 bila idhini ya Mamlaka husika. Pia ukaguzi ulibaini kwamba Wazabuni wote hawakukidhi vigezo vilivyowekwa hivyo kukataliwa na Bodi ya Zabuni kwa kuamuru zabuni itangazwe upya. Licha ya maamuzi haya, ukaguzi huu haukuweza kupata ushahidi wa ripoti ya tathmini ya pili ya zabuni hii wala wajumbe waliohusika kwenye zoezi la pili la tathmini. Licha ya mapungufu yote haya mnamo tarehe 19/06/2014 Kitengo cha Ununuzi katika Bandari ya Dar es Salaam kilitoa ripoti kwa Meneja wa Bandari wakishauri zabuni itolewe kwa Kampuni ya Mpomabiva Investment Ltd kwa kuwa taratibu zote za ununuzi zilifuatwa jambo ambalo halikuweza kuthibitishwa. Kwa ushauri huu Kitengo cha Ununuzi kilimpotosha Meneja wa Bandari juu ya mapendekezo ya Kamati ya Tathmini. Hatimaye Bodi ya Zabuni ilifanya maamuzi ya kuipa Kampuni ya Quality Motors Ltd ambayo awali ilienguliwa na Kamati ya Tathmini.

**5.1.16 Kukosekana kwa Taarifa za Uhakiki wa Bidhaa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine.**

Kwa mujibu wa Kanuni Na. 244(1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma za mwaka 2013 kila Taasisi ya Umma inaponunua bidhaa au huduma ni lazima zikaguliwe kuhakiki ubora wake. Hali kadhalika, Kanuni ya 245 inamtaka kila Afisa Masuuli kuteua kamati ya uhakiki na upokeaji wa bidhaa. Ukaguzi wetu katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine juu ya matakwa haya ya kisheria ulibaini kwamba bidhaa na huduma hazikaguliwi kabla ya kupokelewa na kuingizwa kwenye matumizi.Pia, hapakuweza kupatikana ushahidi wa uteuzi wa Kamati za Ukaguzi na kupokea bidhaa kama sheria inavyotaka.

## 5.2 Usimamizi wa Mikataba

### 5.2.1 Kuchelewa kukamilika kwa Miradi kulikosababishwa na Usimamizi Usioridhisha wa Mikataba

Ilibainika wakati wa ukaguzi kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikusimamia vyema mikataba kati yao na wakandarasi mbalimbali. Udhaifu huu ulipelekea miradi husika kutokukamilika kwa wakati na mingine kuwa chini ya kiwango. Kasoro kama hizi zilibainika wakati wa ukaguzi wa hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwenye ujenzi wa jengo la ghorofa mbili katika tawi la Mbeya. Jengo hili lilijengwa na Mkandarasi B.H Ladwa kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 2.944 kwa makubaliano ya kumaliza ujenzi ndani ya wiki 45 kutoka tarehe (ya mkataba) 14 Februari, 2011. Hata hivyo mradi ulichukua wiki 188 kukamilika ukiwa na kasoro mbalimbali kama vile umeme usiokidhi matumizi, mifumo ya maji na vifaa vya kuzimia moto kutofanya kazi na mashine ya kufua umeme (generator) iliyofungwa kutofanya kazi.

Ukaguzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania ulibaini uwepo wa mikataba ambayo Taasisi iliingia na Wakandarasi mbalimbali bila kuonyesha tarehe ya ukomo kinyume na Kanuni ya 74(1) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446). Kanuni hii inasisitiza uwepo wa tarehe ya kukamilika kwa mkataba kwa kufanya upembuzi yakinifu juu ya muda halisi utakaotumika kuleta bidhaa, huduma au kukamilisha kazi ya ujenzi inayohusika. Mikataba ambayo tarehe za kumalizika kwake hazikuonyeshwa ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 10: Mikataba ambayo haionyeshi ukomo**

| Jina la Mkandarasi | Tarehe ya mkataba | Mrahaba | Aina ya kazi |
|---|---|---|---|
| Oxford University Press | 16.09.2011 | 12.5% | Kuandika na Kuchapa vitabu |
| Educational Books Publishers | 16.09.2011 | 12.5% | Kuchapa vitabu |
| Dar es Salaam University Press | 16.09.2011 | 12.5% | Kuchapa vitabu |
| Mture Educational Publishers | 16.09.2011 | 12.5% | Kuchapa vitabu |

Katika Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania nilibaini ucheleweshwaji wa miradi uliopelekea kuongezeka kwa gharama zisizokuwa za lazima. Mapitio ya zabuni Na.PA/001/08/HQ/W/46 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 34,848,390.78 kwa ajili ya ujenzi wa mtandao wa umeme kiwango cha 132KV, nilibaini kwamba mradi huu ulipangwa kumalizika

ndani ya miezi 18 yaani Septemba 2011. Hata hivyo, mradi huu ulichelewa kukamilika hadi Juni 2013 kutokana na ugumu uliojitokeza wa kupata eneo la mradi. Kwa ucheleweshwaji huu Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi walianza kazi bila kuwa na mkataba halali hivyo kupelekea TANESCO kutakiwa kulipa gharama za kusubiria kuanza kazi kiasi cha Euro 981,831, Dola za Kimarekani 1,423,098.60 pamoja na adhabu ya Dola za Kimarekani 682,940.09.

Katika mkataba mwingine uliopewa namba ya zabuni PA/001/13/HQ/G/006 uliokuwa wa kujenga ‘‘CMS Hardware’’ nilibaini kuwa mradi huu haujakamilika licha ya ukweli kwamba ulitakiwa kukamilika baada ya wiki 8 kutoka tarehe ya kuingiwa kwa mkataba yaani Disemba 2013. Sikuweza kupata ushahidi kama Mkandarasi alilipishwa fidia kwa kucheleweshа mradi. Mkataba Na.PA/001/10/HQ/G/076 wa ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano (EDMS) kwa gharama ya Dola za Kimarekani 467,340 ulikuwa haujakamilika kufikia kipindi cha ukaguzi Aprili, 2014 ambapo ulitakiwa kukamilika ndani ya wiki 12 toka tarehe ya mkataba 5 Mei, 2011.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi kama ambavyo mikataba inaelekeza ni kinyume na Kanuni Na. 114 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446). Kanuni hii inayataka Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kusimamia vyema mikataba inayoingiwa na Wakandarasi mbalimbali kwa kuhakikisha kuwa hakuna ongezeko la gharama na pia bidhaa na huduma zilizonunuliwa zinapatikana kwa wakati kwa mujibu wa mkataba.

### 5.2.3 Mapungufu katika Usimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la ‘Linear Accelerator Treatment’ katika Taasisi ya Kansa Ocean Road Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.333

Kwa mujibu wa mkataba huu, ujenzi ulitakiwa kumalizika ndani ya wiki 32 lakini hadi kufikia tarehe 16 Disemba, 2014 kazi pekee iliyokuwa imekamilika kulingana na cheti cha Mkandarasi Mshauri cha tarehe 18 Disemba, 2013 ilikuwa ni maandalizi ya eneo la ujenzi. Kiasi cha fedha kilichokuwa kimelipwa kwa mujibu wa hati ya malipo kilikuwa Shilingi za Kitanzania milioni 349 ikijumuisha bima na malipo ya awali. Kwa mujibu wa menejimenti ya Taasisi (ORCI) mkataba huu ulitekelezwa kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa ya Shilingi za Kitanzania bilioni 8 toka serikalini na hakuna kiasi chochote kilichokuwa kimepokelewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

### 5.2.4 Mkataba Uliokwama Kutekelezwa baada ya Malipo Kufanyika katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania 22,686,380

Usimamizi makini wa mikataba ni jukumu la kila Taasisi ya Umma itakayoingia mikataba ya bidhaa, huduma, kandarasi za ujenzi au za ushauri. Katika kutimiza jukumu hili, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinatakiwa kusimamia uletwaji wa huduma na bidhaa kwa wakati uliokubalika. Kwa mujibu wa Kanuni Na 121 ya Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2005 (Tangazo la Serikali Na.97), endapo itabainika mkataba haukwenda sawa, hatua stahiki zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Mkandarasi aliyekiuka makubaliano hayo.

Mapitio ya mikataba katika Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Bima Tanzania yalibaini uwepo wa mkataba ulioingiwa tarehe 25 Juni, 2014 kuhusiana na zabuni Na.IE/019/2013-2014/HQ/W/002 kati ya Mamlaka na Wakala wa Ujenzi Tanzania (TBA). Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizokaguliwa, mkataba huu ulikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa uzio kuzunguka jengo la Mamlaka lililoko Zanzibar kwa gharama ya Shilingi 22,686,380. Hadi kufikia kipindi cha kuaandika ripoti hii, kazi ya ujenzi wa uzio huo ilikuwa haijaanza hivyo kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa ya ujenzi.

### 5.2.5 Udhaifu katika Kusimamia Mikataba ya Pango la Nyumba

Ukaguzi wa mikataba ya pango la nyumba katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini mapungufu katika usimamizi wa mikataba ya pango la nyumba kwa baadhi ya Mashirika. Wakati wa ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara, baadhi ya wapangaji walibainika kutokuwa na mikataba ya pango. Kwa wale waliokuwa na mikataba, baadhi ya mikataba ilikuwa imeisha muda wake kati ya mwaka 2007 na 2013. Wapangaji hawa waliendelea kuishi kwenye nyumba za mamlaka bila mikataba kwa takribani miezi 8 hadi 15 na hakuna jitihada zilizofanywa na menejimenti kuandika mikataba mipya.

### 5.2.6 Kuchelewa kuanza na Kumalizika kwa Mkataba katika Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

Kanuni Na. 114 ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (Tangazo la Serikali Na.446), Taasisi ya Umma ina wajibu wa kuhakikisha mikataba yote ya ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi inasimamiwa vizuri hususani (a) kusimamia gharama za mkataba na muda wa kuleta au kutoa huduma husika na kwa kiwango kilichokubalika; (b) kusimamia mwenendo wa mkataba na muda wa kukamilika kwake kwa mujibu wa makubaliano;(c) kuchukua hatua pale ambapo vipengele vya mkataba vimekiukwa na

(d) kuhakikisha kuwa wajibu uliopo kwenye mkataba unatimizwa kikamilifu. Kinyume na matakwa haya ya kisheria, mapitio ya mikataba ya ununuzi katika Shirika la Hifadhi za Taifa yalibaini udhaifu katika usimamizi wa mikataba kati ya Hifadhi na Wakandarasi mbalimbali.

Katika ukaguzi nilioufanya kwenye zabuni Na.PA/037/2013-2014/ANP/W/119 kuhusiana na ukarabati wa barabara ya Miriakamba iliyoko katika Hifadhi za Arusha, nilibaini kuwa kandarasi hii haikusimamiwa vizuri. Mkataba wa ujenzi ulitiwa sahihi tarehe 25 Juni, 2014 katika makubaliano kuwa kazi ya ujenzi ianze siku 14 baada ya Mkandarasi kutoa barua ya kukubali ofa ambayo ilitolewa tarehe 20 Machi, 2014. Muda wa mkataba huu ulikuwa miezi 3 kutoka tarehe ya kukubali ofa ambayo ni tarehe 20 Machi, 2014. Hata hivyo, kufikia kipindi cha kukamilisha ukaguzi huu Novemba 2014, mradi huu ulikuwa haujaanza. Ucheleweshwaji wa mikataba ulibainika pia katika Hifadhi ya Tarangire ambapo Hifadhi iliingia mkataba na Kiliroads Engineers tarehe 26 Machi, 2013 wenye gharama ya Shilingi za Kitanzania 63,000,000. Mradi huu ulikuwa wa kujenga bwalo la chakula katika shule ya Sekondari Eng'eno iliyoko kijiji cha Sukuro Wilaya ya Simanjiro.

Mapungufu mengine yalibainika wakati wa kukagua mkataba wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hifadhi ya Rubondo uliogharimu Shilingi za Kitanzania 109,899,453. Mkataba huu ulitiwa saini tarehe 28 Februari, 2013 kati ya Hifadhi na Kabiriti Engineering kwa makubaliano ya kukamilika tarehe 19 Septemba, 2013. Wakati mkataba huu ukiendelea kutekelezwa, TANAPA iliongeza muda wa kukamilika kwa kandarasi hii kutoka tarehe 14 Oktoba, 2013 na hatimae tarehe 21 Oktoba, 2013 na mwisho kabisa tarehe 27 Disemba, 2013. Hadi tunakamilisha ukaguzi huu 14 Julai, 2014 Mkandarasi hakuwa amekamilisha kazi hii hivyo kusababisha kuchelewa kwa miezi saba (7).

Katika Hifadhi ya Ziwa Manyara, Hifadhi iliingia mkataba na Vituo vya Afya ili kutoa huduma za afya kwa wafanyakazi na familia zao. Ukaguzi huu ulibaini kwamba mikataba ya huduma za afya ilikuwa imekwisha muda wake na hapakuwepo na jitihada za kuirejea japo huduma zilikuwa zinaendelea kutolewa. Katika Hifadhi ya Ruaha tulibaini ujenzi wa bweni la shule ya Sekondari ya Lukuvi kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania 162,639,000 uliochelewa kukamilika kwa mwaka 1. Mradi huu ulipaangwa kuanza tarehe 25 Machi, 2013 na kutarajiwa kumalizika tarehe 10 Juni, 2013. Hadi tunahitimisha ukaguzi huu mradi ulikuwa bao haujakamilika ukiwa na hatari ya

kupoteza fedha zilizolipwa awali kwa kuwa mkataba haukuwa na kipengele cha kumbana Mkandarasi endapo angeshindwa kukamilisha kazi kwa wakati.

### 5.2.7 Kuchelewa Kuanza kwa Uzalishaji katika Mradi wa Ushirikiano wa Kuendeleza 'Buck Reef Gold Mine' kati ya STAMICO na Kampuni ya Tanzania American International Corporation (2000) Limited

Ukaguzi wa mkataba kati ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na kampuni ya Tanzania American International Corporation (2000) Limited ya Dar es Salaam, ambapo kampuni washirika 'Buckreef Gold Company Limited' iliyoanzishwa tarehe 24 Oktoba, 2011 kwa madhumuni ya kuendeleza 'Buckreef Gold Mine umethibitika kutoendelea vizuri kiasi kwamba mradi hauonyeshi dalili za kukamilika kwa wakati.

Katika mkataba huu ilikubalika kwamba uzalishaji utaanza ndani ya miezi 30 toka siku ya kutiliana saini makubaliano na endapo muda wa kuanza uzalishaji utachelewa, 'Tanzania American International Corporation (2000) Limited ingeilipa STAMICO fidia ya ucheleweshaji kiasi cha Dola za Kimarekani 500,000 kama mradi utasogezwa mbele kwa mara ya kwanza, Dola za Kimarekani 625,000 kwa mara ya pili na Dola la Kimarekani 750,000 kwa vipindi vyovyote vitakavyofuata. Hata hivyo, hadi kufikia muda wa kukamilisha ripoti hii zaidi ya miezi 38 tangu kampuni tanzu ilipoanzishwa, mradi ulikuwa haujaanza uzalishaji na hapakuwepo dalili wala ushahidi wa ulipwaji wa fidia kwa ucheleweshwaji kama ambavyo mkataba unaelekeza.

## SURA YA SITA

## USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA

### 6.0 Utangulizi

Rasilimali ni mali zinazomilikiwa na Taasisi au Shirika kwa ajili ya matumizi yake ya kila siku katika kuendesha shughuli zake. Rasilimali zinajumuisha mali zinazoshikika na zisizoshikika ambazo taasisi inazimiliki. Mali hizo ni kama mitambo, vifaa mbalimbali, uwekezaji, fedha taslimu, madeni yanayodaiwa, akiba ya vifaa, mifumo ya ndani ya kompyuta, tovuti na malipo ya awali.

Sura hii ni muhimu kwa sababu ya changamoto zinazoyakabili Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kufuatilia na kusimamia rasilimali za Taifa. Pia, pamoja na changamoto hizo, hili ni eneo ambalo kuna uwezekano mkubwa kwa watumishi wasio waaminifu kufanya ubadhirifu wa mali za Umma. Kwa mwaka huu wa ukaguzi, nimeainisha masuala ambayo ni muhimu kwa Serikali, Bunge na wadau wengine kuyatolea maelekezo ya namna nzuri ya kuyatekeleza kama ifuatavyo;

### 6.1 Ucheleweshwaji katika Kukamilisha Miradi Mbalimbali yenye Thamani ya zaidi ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 3

Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, zinatekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za ndani au fedha za Wafadhili. Wakati wa Ukaguzi, ilibainika kuwa, baadhi ya miradi ilikuwa haijakamilika kwa wakati hivyo kuchangia kuongezeka kwa gharama za mradi husika, kushikiliwa kwa fedha ambazo zingefanya shughuli nyingine, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa thamani ya fedha. Kwa mwaka wa fedha 2013/14, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha ilikuwa na miradi minne (4) ya kuchimba visima yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 157,298,390 ambayo iliachwa bila kuendelezwa katika kipindi chote cha mwaka huo. Aidha, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, ilikuwa na miradi mitano (5) yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 1,104,964,614 ambayo imekaa bila kuendelezwa kwa zaidi ya miaka sita (6). Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC) kilikuwa na kasi ndogo katika ujenzi wa mradi wa Biogas katika Gereza la Namajani na Mlale JKT wenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 781,425,425 ambao ulipaswa kukamilika tarehe 31 Disemba, 2013 lakini hadi kufikia mwezi Disemba 2014, mradi huo ulikuwa haujakamilika. Mradi huu unatozwa adhabu ya 0.1% kwa kila siku inayocheleweshwa, hali inayopelekea kuongezeka kwa gharama za mradi huo.

Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) ilikuwa na miradi sita (6) ambayo ilipaswa kuwa imeshakamilika lakini ilikuwa haijakamilika. Pia, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Arusha) ilikuwa na mradi wa ujenzi wa bweni wenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 432,372,254 ambao ulipaswa kuwa umekamilika kufikia tarehe 26 Novemba, 2010 lakini mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2013/14 mradi huo ulikuwa bado haujakamilika.

Taasisi ya Kansa ya Ocean Road ilikuwa na mradi wa kuanzisha Mfumo wa Kompyuta wa Taarifa za Afya (NIARA Software), ambao ulipaswa kufanya kazi miezi mitatu baada ya kuanzishwa kwake (Tarehe 1 Machi, 2011). Hata hivyo, mradi huo haujaanza kufanya kazi ikiwa imepita zaidi ya miaka minne (4) sasa, ambapo fedha kiasi cha Shilingi za Kitanzania 293,513,527.30 sawa na 94.99% ya gharama zote kilikuwa kimeshalipwa. Mfumo huu ulitegemewa kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa Taasisi lakini hata hivyo ilibainika kuwa muda wake wa matumizi unakaribia kufika kikomo bila ya kupatikana kwa thamani ya fedha ziliyotumika.

## 6.2 Kasoro Zilizobainika katika Usimamizi wa Mafuta ya Magari

Ukaguzi ulibaini uwepo wa kasoro kadhaa kwenye usimamizi wa mafuta ya magari katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Katika Chuo cha Wanyama Pori cha Mweka, nilibaini kuwa madereva walikuwa wakipewa mafuta kutokana na kuponi ambazo hupewa muuzaji wa mafuta, ambaye baadae huzitumia kama uthibitisho wa kulipwa. Hata hivyo ilibanika kuwa hakuna usuluhishi uliokuwa ukifanyika baina ya kuponi, ankara na hati ya kupokea bidhaa hali inayotoa mwanya kwa madereva wasio waaminifu kwa kushirikiana na muuzaji kughushi malipo. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi-Makao Makuu, walibainika kuwa na vitabu vya kusaini vya magari ambavyo havikuhakikiwa na maofisa waandamizi ili kufahamu kiasi cha mafuta kilichotumika kulingana na umbali ambao gari limetembea. Baadhi ya vitabu hivyo havikuwa na taarifa za kujitosheleza. Taasisi ya Kansa ya Ocean Road, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma walikuwa na vitabu visivyokuwa na taarifa kamili huku vitabu vingine vikiwa havipo kabisa. Shirika la Magazeti Tanzania lilikuwa na taarifa tofauti kati ya ripoti ya mwezi ya matumizi ya mafuta na vitabu vya kusaini magari huku Taasisi ya Mifupa Muhimbili ikiwa haina kabisa ripoti ya robo mwaka inayoonyesha matumizi ya mafuta kwa vipindi tofauti. Bila usimamizi makini wa mafuta, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zitashindwa kufahamu kiasi cha mafuta kinachotumika kwa

safari za kiofisi jambo linaloongeza gharama kwa Mashirika na Taasisi hizo.

## 6.3 Ucheleweshwaji wa Huduma na Bidhaa kwa Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Serikali ilitoa waraka wa kuzitaka taasisi zote zilizopo chini yake, kununua magari yao kwa kupitia Wizara ya Miundombinu. Mnamo mwaka 2010, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) waliwasilisha ombi lao la kununuliwa magari matano na Wizara hiyo. Hata hivyo, kati ya magari matano (5) yaliyoombwa, ni magari manne (4) tu ndiyo yalipokelewa na Mamlaka hiyo huku kukiwa na kutoeleweka juu ya gari la tano aina ya Toyota Land Cruiser Hard Top lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 106,723,967 ambalo mpaka wakati wa ukaguzi Wizara imeshindwa kulikabidhi kwa Mamlaka hiyo. Pia, Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC) waliingia mkataba na Kampuni ya Scan Tanzania mnamo mwezi Mei mwaka 2012 kwa ajili ya ununuzi wa vipuli vya matrekta ambapo kituo kililipa kiasi cha Pauni za Kiingereza 70,785.65 sawa na Shilingi za Kitanzania 157,500,200. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014 vipuli vya kiasi cha Shilingi za Kitanzania 142,935,903.37 vilikuwa havijapokelewa na Kituo hicho (CARMATEC).

## 6.4 Kutokukusanywa Kikamilifu kwa Kodi ya Pango

Ilibainika katika Makao Makuu ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kuwa, kati ya Mwezi Julai na Disemba mwaka 2013, wafanyakazi waliokuwa wakiishi katika nyumba za Mamlaka hiyo walikuwa wakilipa kiasi cha Shilingi za Kitanzania 20,000 kwa nyumba ndogo na Shilingi za Kitanzania 30,000 kwa nyumba kubwa kwa mwezi kinyume na taratibu zilizoainishwa katika jedwali la 13 la kanuni na masharti ya wafanyakazi ambalo linafafanua kuwa mfanyakazi anayeishi kwenye nyumba ya Mamlaka atalipa asilimia 8 ya mshahara wake kama kodi ya pango. Pia, katika Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi Tanga, ilibainika kuwa, aliyekuwa Meneja wa Rasilimali Watu ambaye baadaye alihamishiwa Mkoani Mbeya kisha kuamua kuacha kazi, bado anaishi kwenye nyumba ya Mamlaka hiyo mjini Tanga. Ingawa Mamlaka hiyo ilishawahi kulifikisha suala hilo kwenye Mahakama ya Ardhi ya Mkoa huo na uamuzi kutolewa tarehe 11 Machi, 2011 kwa faida ya Mamlaka bado mwajiriwa huyo wa zamani hajahama na wala halipi kodi ya pango.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa wapangaji katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine hawajalipa kodi ya pango inayokadiriwa kufikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania 44,468,595 na Chuo hicho hakijajumuisha deni hilo kwenye vitabu vyake vya hesabu. Pia, Shirika la Maendeleo ya

Petroli Tanzania (TPDC) limepangisha baadhi ya nyumba zake kwa wapangaji wasio wafanyakazi wa shirika hilo. Hata hivyo, kiasi cha Shilingi za Kitanzania 78,604,500 kilikuwa hakijalipwa kwa zaidi ya miaka miwili na wapangaji walioondoka bila kulipa. Ukaguzi pia ulibaini mfanyakazi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC) ambaye hastahili, amepewa nyumba ya Taasisi hiyo katika kiwanja Na. 14/15 bila kulipa kodi. Kutokukusanywa kwa kodi kunayakosesha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma mapato huku yakiendelea kulipia gharama za matunzo na matengenezo ya majengo hayo.

## 6.5 Kutokujumuishwa kwa Baadhi ya Mali katika Vitabu Vya Hesabu

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu vinaelezea Mali kuwa ni rasilimali iliyo chini ya Taasisi, inayotokana na miamala iliyofanyika kipindi cha nyuma ambapo faida mbalimbali zinategemewa kupatikana kwa Taasisi hizo. Ukaguzi wa Mwaka 2013/14 ulibaini kuwa, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zina mali ambazo hazijajumuishwa katika vitabu vya hesabu. Ilibainika kuwa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania inamiliki ardhi iliyopewa na Serikali katika maeneo mbalimbali ya nchi ambayo haikujumuishwa kwenye hesabu kama mali inayomiliki. Chuo Kikuu cha Dodoma pia kina majengo yenye thamani ya Shilingi bilioni 452.1 (Tathmini ya mwaka 2011) ambayo yalijengwa kwa ufadhili wa mifuko ya pensheni ya NSSF, PSPF, LAPF, PPF na NHIF ambayo hayakujumuishwa kwenye hesabu zake. Ingawa majengo hayo hayajakabidhiwa kisheria kwa Chuo hicho, Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu vinataka Mali itambuliwe kwa namna inavyotumika na kuleta faida kwa Taasisi badala ya kutazama umiliki wake kisheria. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi-Kipawa bado inaripoti jengo lililokamilika na ambalo limeanza kutumika kwa miaka miwili (2) sasa kama jengo linaloendelea na ujenzi, huku ardhi yake ikiwa haijajumuishwa kabisa katika vitabu vya hesabu. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa ilikuwa na viwanja vitatu (3) katika maeneo ya Lukobe, Kingolwira na Kilakala ambavyo havikujumuishwa katika orodha ya mali zinazomilikiwa na Mamlaka hiyo japo ilithibitika pia kuwa walikuwa na hati za viwanja hivyo.

## 6.6 Kuongezeka kwa Vifo vya Wanyamapori Kutokana na Ajali za Barabarani

Moja kati ya majukumu ya Shirika la Hifadhii la Taifa (TANAPA) ni kulinda na kuhifadhi maliasili ya wanyama, kuendeleza na kuhifadhi mbuga, kuangalia afya za wanyama, kushirikisha jamii zinazoishi karibu na mbuga katika utunzaji wa mazingira na kukuza na kuongeza utalii. Mbuga ya Wanyama ya Mikumi iliyo chini ya Shirika la Hifadhii

la Taifa imebainika kuwa na tatizo la kuuwawa kwa wanyama katika mbuga hiyo kutokana na ajali za barabarani. Kulingana na ripoti ya usimamizi wa viumbe hai, jumla ya wanyamapori 107 waligongwa na kufa katika ajali za barabarani kati ya kipindi cha mwezi Julai 2013 hadi mwezi Machi 2014. Serikali kushindwa kudhibiti ajali hizi kutaifanya Shirika la Hifadhii la Taifa kushindwa kutimiza moja ya wajibu wake kisheria wa kuhifadhi na kulinda wanyama.

## 6.7 Kupotea kwa Mapato Kutokana na Uzalishaji Chini ya Kiwango

Mfumo wa kusimamia mwenendo wa mawasiliano kwa njia ya simu (Telecommunication Traffic Monitoring System) ni mfumo mpya unaotumiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kusimamia mwenendo wa mawasiliano wa simu za Kimataifa. Mfumo huu pia unaweza kusimamia simu za ndani, simu zisizotumia mitandao, miamala inayofanyika kwa njia ya simu, kutambua na kuzuia simu ambazo zina viashiria vya udanganyifu pamoja na kufanya kazi kama mfumo wa utambuzi na usajili wa mawasiliano. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikiwa kukusanya kiasi kikubwa cha fedha zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 26.22 kutokana na simu za kimataifa kilichoakisiwa na Mamlaka hiyo. Hata hivyo, Mamlaka hiyo bado haijaanza kuboresha mfumo huo ili uweze kutumika pia kwa simu za ndani ili kuwaongezea mapato zaidi. Shirika la Magazeti Tanzania limekuwa likichapisha magazeti mengi zaidi bila kujali kiwango cha mahitaji na mauzo yanayofanyika. Kwa mwaka wa fedha 2013/14 kiasi cha magazeti 8,346,834 kilizalishwa, ambapo kati ya hayo ni magazeti 5,362,641 tu ambayo yaliuzwa. Gharama za kuzalisha magezeti ambayo hayakuuzwa ilikuwa ni Shilingi za Kitanzania 1,171,996,899 sawa na 36% ya gharama zote za uzalishaji.

Pia, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same, ilitoza kiasi cha asilimia 53 tu ya maji yaliyozalishwa (mita za ujazo 413,567). Ilibainika kuwa, kiasi kikubwa cha maji yaliyozalishwa cha takribani asilimia 47 kilikuwa kikipotea. Kiasi hiki ni kikubwa kuliko kiasi kinachokubalika cha upotevu wa maji cha asilimia 20-25. Kama kiasi kilichopotea cha zaidi ya upotevu unaokubalika kingeuzwa kwa watumiaji, Mamlaka ingepata kiasi cha Shilingi za Kitanzania 114,764,250. Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam pia ilikuwa na kiwango kikubwa cha upotevu wa maji cha asilimia 57.4 ambacho ni kikubwa kuliko kiasi kinachokubalika cha asilimia 20-25. Kiasi cha fedha kisichokusanywa kutokana na upotevu wa maji hayo kwa mwaka 2013/14 kinakadiriwa kuwa Shilingi za Kitanzania bilioni 9.6. Kushindwa kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kujiendesha kwa ufasaha kunaweza kuyasababishia kupoteza mapato zaidi.

## 6.8 Mapungufu Kwenye Usimamizi wa Fedha

Fedha ni kile kiasi ambacho taasisi inakimiliki kama fedha Taslimu au kilichohifadhiwa benki na kinachozunguka kwenye shughuli za kawaida za taasisi, ambacho ni rahisi sana kuibiwa kuliko rasilimali zingine. Kuzuia na kugundua wizi/matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma kunahitaji usimamizi sahihi unaohusisha kuweka mifumo ya udhibiti wa ndani ya Taasisi inayogusa maeneo yote husika. Maeneo ambayo ni lazima yazingatiwe ni pamoja na ukusanyaji, na usimamizi wa matumizi ya fedha, hususani fedha taslimu. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka wa fedha 2013/2014, nilibaini mapungufu mbalimbali ambayo yasiporekebishwa yatasababisha matumizi yasiyo sahihi ya fedha za Umma ikiwa ni pamoja na wizi.

Kwa mfano, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi-Makao Makuu Dar es Salaam ilikuwa na kiasi cha Shilingi za Kitanzania 152,650,626 kilichotolewa benki ambacho ni zaidi ya akiba iliyokuwepo. Kiasi cha Shilingi za Kitanzania 21,964,038 kilichoonekana kutolewa kwenye akaunti ya benki kwa muda mrefu lakini hakipo kwenye vitabu vya hesabu na kiasi cha Shilingi za Kitanzania 82,992,929 kilichopaswa kuwasilishwa benki, kimekaa muda mrefu sasa bila kuonekana kwenye taarifa za benki. Chuo cha Mafunzo na Ufundi Stadi Mbeya kimeripoti kiasi cha Shilingi za Kitanzania 122,350,000 ambacho hakioani na taarifa za usuluhishi baina ya benki na vitabu vya hesabu kwa zaidi ya miaka mitano (5) hali inayoashiria uwepo wa vitendo vya udanganyifu.

## 6.9 Mambo ambayo Serikali inapaswa Kuyachukulia Tahadhari ya Mapema

Taasisi ya Kansa ya Ocean Road ina upungufu mkubwa wa vifaa vya uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa wa Kansa. Mahitaji halisi kwa sasa ni mashine thelathini na sita (36), wakati Taasisi hiyo ina mashine kumi na moja (11) tu ambapo kati ya hizo tatu (3) zimeshapitwa na wakati (zinangoja kuondolewa) na nne (4) zinahitaji kufanyiwa matengenezo. Hali hiyo imepelekea ucheleweshwaji wa matibabu hasusani ya mionzi kwa wagonjwa ambapo humchukua mgonjwa zaidi ya miezi mitatu kutibiwa, wakati viwango vinavyokubalika kimatibabu ni chini ya wiki mbili (2). Pia, Serikali inapaswa kufahamu juu ya mpango wa Tume ya Ushindani (FCC) kujenga ofisi zake, ambapo tayari imetenga kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 5.3. Mshauri Mwelekezi wa Tume ya Ushindani, Wakala wa Majengo Tanzania, amependekeza ununuzi wa jengo la Hoteli ya Grand Villa lenye thamani ya Shilingi za Kitanzania bilioni 3.9 (Muuzaji akitaka Shilingi za Kitanzania bilioni 4.2), na kubadilishwa kuwa Ofisi. Hata hivyo,

hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa tathmini ya kutosha ilifanyika kufahamu gharama halisi za kubadili jengo hilo la hoteli kuwa ofisi. Bila tathmini ya kina kufanyika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya manunuzi ya ofisi zinaweza zisitoshe.

## 6.10 Kuwa na Mali Zinazozidi Mahitaji Husika

Kufikia tarehe 30 Juni, 2014, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam ilikuwa ina vifaa vingi vyenye thamani kubwa ya Shilingi za Kitanzania 1,296,416,650 ambavyo vilirudishwa na Mkandarasi baada ya kumalizika kwa miradi ya maji na hivyo kuhifadhiwa katika ghala la Mamlaka hiyo. Vifaa hivi vilinunuliwa mahsusi kwa ajili ya mradi huo na sio kwa ajili ya kutumika katika shughuli za kila siku za Mamlaka hiyo. Ingawa vifaa hivi vinaweza kutumika baadae katika miradi hiyo iliyokwishakamilika, uhifadhi wa vifaa vingi vyenye thamani kubwa unaiweka Mamlaka katika hatari ya uchakavu na uharibifu wa vifaa hivyo ambao unaweza kushusha thamani yake. Pia, fedha ambazo zilitumika kwenye kununua vifaa hivyo, zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za kimaendeleo. Chuo cha Ufundi Stadi VETA mkoa wa Lindi kina vifaa vya maabara ambavyo vilinunuliwa kwa Shilingi za Kitanzania 286,876,830 mnamo mwezi Agosti, 2011 lakini vimefungiwa kwenye kontena na vimekuwa havitumiki mpaka leo kwa kuwa chuo hicho hakijaanza kutoa kozi ya kutumia vifaa hivyo. Vifaa hivyo vya maabara vinajumuisha pia kemikali tofauti ambazo zinakaribia kuisha muda wake wa matumizi. Pia, Taasisi ya Kansa ya Ocean Road ilipokea mashine mbili za mionzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) mnamo tarehe 22 Oktoba, 2014. Hata hivyo, ilibainika kuwa Mashine hizo hazikuwa zikitumika wala kuhifadhiwa katika hali nzuri kwa kuwa hakukuwa na eneo lililoandaliwa kwa ajili ya kuhifadhi mashine hizo. Uongozi wa Taasisi hiyo ulikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kuelezea kuwa, japo walipokea kama msaada, mashine hizo hazikuwa zikihitajika na Taasisi hiyo.

## 6.11 Kukosekana kwa Udhibiti wa Mita Zilizoharibika

Kwa kawaida mita zilizoharibika au ambazo zimebadilishwa na mita mpya, zinapaswa kurudishwa kwenye ghala la vifaa kusubiri taratibu zilizoainishwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake katika kuziondoa. Hata hivyo, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga ilibainika kutokuwa na usimamizi mzuri wa mita zinazorejeshwa kutoka kwa wateja. Pia hakukuwa na mabadiliko yoyote yaliyofanyika katika vitabu vya hesabu kuziondoa mita hizo. Hali kama hiyo pia ilionekana katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara ambapo kulikuwa na tofauti ya mita 372 kati ya mita zilizopaswa kuwepo ghalani na mita zilizokuwepo.

## 6.12 Tofauti Kati ya Deni Lililoripotiwa baina ya Mfuko wa Huduma za Mawasiliano na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2014, Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) uliripoti kuidai Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar kiasi cha Shilingi 1,272,851,390. Hata hivyo, Kampuni hiyo ya Zanzibar ilikiri kudaiwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania 135,666,155 tu hivyo kuacha tofauti kubwa ya Shilingi 1,137,185,235 baina ya taarifa za Taasisi hizo mbili. Hatua za haraka zisipochukuliwa kuondoa tofauti hiyo, kuna shaka kubwa kuwa pande mbili hizi zitaingia kwenye mgogoro.

## 6.13 Mali Kutokufanyiwa Tathmini

Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (Na. 16) vinazitaka Taasisi kuzifanyia tathmini mali zao kila baada ya miaka 3 hadi 5 ili kujua thamani halisi ya mali hizo katika muda huo. Hata hivyo, ilibainika kuwa, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine Morogoro hakijathaminisha mali zake kwa muda wa miaka 12. Shirika la Madini Tanzania walifanya kwa mara ya mwisho tathmini ya majengo yake yanayotumika kama vitega uchumi mwaka 2008. Hali kama hiyo pia imebainika katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma, Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC), Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Elimu Tanzania ambapo Mali zao hazikuwa zimefanyiwa tathmini kutoka mwaka 2008. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga haijafanya tathmini ya mali zake kutoka mwezi Mei, 2009. Kutokufanya tathmini ya thamani za mali kwa muda mrefu, kunaweza kusionyeshe hali halisi ya thamani za mali za Taasisi.

## 6.14 Masuala Yanayohusiana na TEKNOHAMA

### 6.14.1 Kutotumia Mifumo ya Kompyuta katika Shughuli za Taasisi

Katika miaka ya hivi karibuni, Teknolojia imekuwa ikibadilika kwa kasi kubwa huku kukiwepo na mifumo mingi ya kompyuta zinazotengenezwa kwa dhumuni la kukidhi haja za Taasisi kubwa, za kati na zile ndogo. Hata hivyo, katika ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nilibaini kuwa kuna baadhi ya Taasisi haziendani na mabadiliko ya kiteknolojia zikiwa zinaendelea kutumia mifumo isiyo ya kielektroniki ambayo ina changamoto za kuweza kuhifadhi taarifa nyingi kwa usahihi, na yenye kuchukua muda mwingi. Kutokuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa kuandaa hesabu za Taasisi, kunapelekea kuwepo kwa makosa mengi na pia kunatoa mwanya wa kufanyika kwa udanganyifu. Mamlaka ya Rufaa za Zabuni, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Baraza la Ushauri kwa Watumia huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji na Mamlaka ya Bandari Tanzania bado wanatumia njia zisizo za

kielektroniki kuandaa hesabu zao. Chuo cha Usafirishaji kilinunua mfumo wa uhasibu aina ya pastel mnamo mwaka 2012, lakini mpaka sasa haujaanza kutumika huku wakiendelea na mifumo isiyo ya kielektroniki.

Pia, ilibainika kuwa, Chuo cha Diplomasia (CFR) kinaendelea kuweka kumbukumbu zake za udahili wa wanafunzi kwa njia zisizo za kielektroniki, hali inayochangia taarifa zenye makosa. Kwa mfano, idara ya udahili ilikuwa na taarifa ya wanafunzi 888 waliodahiliwa katika mwaka wa fedha wa 2013/14, huku idara ya uhasibu ikiwa na taarifa ya wanafunzi 879 tu, tofauti ambayo ilikosa maelezo. Chuo cha Kilimo Sokoine kinadhibiti mauzo ya bidhaa zinazotokana na misitu, kwa kuangalia ankara, stakabadhi na hati ya kuruhusiwa kuingia lango kuu. Hata hivyo, shughuli zote hizo zinafanyika kwa mfumo usio wa kielektroniki hali iliyopelekea kushindwa kupata mtiririko wa miamala kwa ajili ya ukaguzi. Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma ilinunua 'software' aina ya 'ARUTI' kwa ajili ya kusimamia taarifa za mishahara na rasilimali watu kutoka kwa kampuni ya NPK Technology kwa Dola za Kimarekani 7,400. Hata hivyo, 'software' hiyo iliacha kufanya kazi miwezi miwili tu baada ya kununuliwa. Kwa sasa Mamlaka hiyo imerudia mfumo wake wa awali usio wa kielektroniki.

### 6.14.2 Kutokuwepo Kwa Sera za Teknohama au Uwepo wa Sera Zilizopitwa na Wakati

Katika ukaguzi wa shughuli za Teknohama, Ilibainika kuwa Sera ya Teknohama ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliboreshwa kwa mara ya mwisho Disemba, 2011. Hata hivyo, toka kipindi hicho, hadi sasa, Mamlaka hiyo imepitia mabadiliko mengi ya Kiteknolojia, yanayohitaji kuakisiwa katika sera hiyo. Hali kama hiyo pia ilibainika katika Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Chuo cha Wanyama Pori Mweka ambavyo vina sera za teknohama ambazo hazijitoshelezi kikamilifu kukidhi haja ya Taasisi hizo kwa sasa.

## SURA YA SABA

## USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

### 7.0 Utangulizi

Usimamizi wa rasilimali watu ni nguzo muhimu katika kusimamia watumishi. Idara ya rasilimali watu ina wajibu wa kubuni na kutekeleza sera mbalimbali zinazosimamia watumishi. Watumishi ni rasilimali ya Taasisi. Baadhi ya majukumu muhimu ya idara ya rasilimali watu ni kuajiri watumishi na kuwapa motisha, kuwapa mafunzo na maendeleo ya kitaaluma.

Usimamizi bora wa rasilimali watu unaweza kusaidia Taasisi kufikia malengo iliyojiwekea, kuhamasisha ari ya kazi na watumishi kuridhika na utendaji kazi katika ngazi zote kwa kujenga mahusiano mazuri kati ya mwajiri na mwajiriwa. Sura hii inalenga kuongelea maeneo muhimu ambayo endapo yataboreshwa yataongeza tija katika utendaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

### 7.1 Tathmini ya Upimaji na Utendaji wa Watumishi Kutofanyika

Mfumo wa upimaji wa watumishi huwezesha kufanya tathmini ya utendaji wa wafanyakazi, hivyo kuwezesha uongozi kufanya maamuzi kwa misingi ya kitaalam katika maeneo mbalimbali kama kupandisha vyeo, kushusha vyeo, nyongeza za mishahara na uteuzi wa mfanyakazi bora. Na pia baada ya tathmini kutoa maoni kwa wafanyakazi kwa lengo la kuboresha utendaji. Katika ukaguzi uliofanyika, kulikuwa hakuna ushahidi kuwa tathmini ya utendaji wa watumishi ilifanyika katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Hivyo watumishi hao hawakuweza kujua hali halisi ya utendaji wao na kutambua maeneo ya udhaifu wao ili kuyafanyia maboresho. Mapungufu haya yalibainika katika Chuo cha Ardhi, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Ubungo Plaza, Shirika la Masoko Kariakoo, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Ustawi wa Jamii na Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga.

### 7.2 Stahiki za Wafanyakazi Hazikuonyeshwa kwa Mujibu wa Kiwango cha Uhasibu Namba 19

Kiwango cha Uhasibu Na. 19 (ilivyorekebishwa 2011) kinatoa mwongozo wa namna ya kuonyesha stahiki za mfanyakazi ikiwa ni pamoja na zile za muda mfupi kama vile mishahara, likizo ya mwaka na stahiki baada ya ajira kama vile mafao ya kustaafu, mafao ya utumishi wa muda mrefu na

mafao ya kuachishwa kazi. Kiwango hicho cha uhasibu kinataka gharama za mfanyakazi kutambuliwa katika kipindi ambacho mtumishi anastahili na sio kipindi ambacho mtumishi atalipwa.

Ilibainika kuwa Chuo cha Ardhi hakikutimiza matakwa ya kiwango cha Uhasibu Na.19 kwa kutoonyesha gharama za likizo za wafanyakazi ambazo zilikua hazijalipwa. Hii ni wazi kuwa gharama za likizo na madai mengine vilionyeshwa kwa kiwango cha chini.

## 7.3 Kukosekana kwa Nyaraka Muhimu katika Majalada ya Wafanyakazi

Majalada ya wafanyakazi yaliyotengenezwa na kutunzwa vizuri ni muhimu kwa kuwa yanakuwa na nyaraka zote muhimu zinazohusiana na kila mfanyakazi. Pia, ni rahisi kupata taarifa endapo zinahitajika wakati wa kufanya maamuzi kama vile kumpandisha mfanyakazi cheo, kumthibitisha mfanyakazi au uamuzi mwingine wowote kuhusiana na rasilimali watu. Utunzaji mzuri wa majalada husaidia kupata nyaraka sahihi kwa wakati na kusaidia katika kufanya maamuzi kwa haraka zaidi.

Mapitio ya majalada ya wafanyakazi katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yalibainika kukosa nyaraka muhimu kama vile nakala za vyeti vya taaluma, barua za uteuzi na kupandishwa vyeo ambazo zilitumika katika kutathmini uwezo binafsi na stadi zinazohitajika. Majalada ambayo yalitunzwa bila nyaraka muhimu kama ilivyoainishwa kwenye sera na miongozo ya rasilimali watu yalibainika katika Taasisi za Ubungo Plaza, Mfuko wa Benjamin William Mkapa na Taasisi ya Mifupa Muhimbili.

## 7.4 Ucheleweshaji wa Kukusanya na Kuwasilisha Makato ya Kisheria ya Wafanyakazi kwenye Mifuko ya Pensheni na TRA

Makato ya Kodi kwa Wafanyakazi ni kodi inayotozwa kwenye mapato ya wafanyakazi. Katika mfumo huu, mwajiri kwa mujibu wa sheria anatakiwa kufanya makato ya kisheria kwenye mshahara wa mfanyakazi. Wakati wa kupitia utaratibu wa uchangiaji wa makato ya kisheria katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yalikua hayazingatii kuwasilisha makato kwa muda uliopangwa. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Makato ya Kodi ya Wafanyakazi kwa mujibu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ni siku ya 7 baada ya mwisho wa mwezi wa makato kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004 (Kama ilivyorekebishwa 2008). Mamlaka hizi zipo katika hatari ya kutozwa riba na adhabu ambazo zinaweza kuwa na athari kwa kushindwa kutimiza wajibu kama ilivyotarajiwa. Mapungufu haya yalionekana katika Shirika la Tija la Taifa, Mamlaka ya Rufani za Zabuni, Baraza la

Kiswahili Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Baraza la Taifa la Mazingira, Shirika la Madini Tanzania na Bodi ya Korosho Tanzania.

Sheria mpya Na.8 ya mwaka 2013 ya Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali (PSPF) inaupa Mfuko nguvu ya kutoza adhabu kwa wanachama wanaochelewesha michango. Ukaguzi uliofanyika katika Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali ulibaini kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilichelewesha michango yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania milioni 60.906. Hapakuwa na ushahidi ambao unaonyesha kwamba Mfuko ulitoza adhabu kwa mwajiri husika.

Mapitio ya madeni ya wadai kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2014 yalibaini kuwa, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilionyesha linadaiwa Shilingi za Kitanzania 1,240,103,538.96 na Shilingi za Kitanzania 594,372,016.50 kwa ajili ya kodi ya Mapato na michango ya SDL. Kiasi cha kodi ambacho hakijawasilishwa kilitokana na makato ya mishahara ambayo haikupokelewa kutoka Hazina na hivyo kulipwa kwa kutumia fedha za ndani.

Ilibainika kuwa Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO) halikuzingatia matakwa ya kifungu Na. 81 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 na kifungu Na. 46 cha Sheria ya Mifuko ya Pensheni kama ilivyorekebishwa mwaka 2012. Hadi mwezi Juni, 2014 DAWASCO ilikua na deni la kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 10 ikiwa ni malimbikizo ya PAYE, SDL na michango ya NSSF, PSPF, LAPF na PPF. Madeni haya yanaongezeka mwaka hadi mwaka na Shirika limeshindwa kulipa kiasi kinachodaiwa. Mazingira haya yanaonyesha hali ya kutokujulikana juu ya wafanyakazi kulipwa mafao yao pindi watakaapostaafu au kusitishwa kwa ajira zao iwapo makato hayo ya kisheria hayatawasilishwa.

## 7.5 Nafasi Ambazo Hazijajazwa kwenye Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Mapitio ya mahitaji ya rasilimali watu katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania yalibaini kuwa nafasi muhimu hazikuwa na wafanyakazi kwa muda mrefu. Wakurugenzi wengi walistaaafu katika kipindi cha mwaka bila nafasi zao kujazwa hali iliyopelekea nafasi hizo kuendelea kukaimiwa. Nafasi zilizoachwa wazi katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania zilikuwa za Mkurugenzi wa Fedha na Utawala, Mkurugenzi wa Utafiti na Mkurugenzi wa Uwekezaji.

Ilibainika kuwa, nafasi za Meneja wa Mfumo wa Usimamizi wa Habari na Meneja Masoko na Huduma kwa Wateja zilikuwa wazi katika

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza. Pia, ilibainika kuwa, baada ya Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Wanawake Tanzania kuondoka, BoT iliandika barua ya tarehe 19 Desemba, 2013 yenye kumbukumbu Na. FA.56 / 433/050 / Vol.III / 17 na kutoa maelekezo kuwa nafasi hiyo ijazwe ndani ya miezi mitatu baada ya tarehe ya barua yao. Nafasi hii haikujazwa hadi wakati wa kukamilisha ukaguzi huu.

Wakati wa kupitia mpango wa rasilimali watu wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili wa mwaka 2014-2019, kulinganisha na idadi ya sasa ya wafanyakazi, ilibainika kuwa kulikuwa na nafasi za ajira arobaini na nne (44) zilizopaswa kujazwa. Nafasi hizi zimesababisha shughuli kama vile matengenezo ya mashine, matengenezo ya magari na usimamizi wa mali kusimamiwa na Kurugenzi nyingine hivyo kukwamisha utendaji wa Taasisi. Kutokana na kwamba mpango mkakati wa mwaka 2014-2019 umeandaliwa kwa kuzingatia nafasi zilizo wazi za ajira, Taasisi itakua na vikwazo katika kutimiza malengo iliyojiwekea kama nafasi hizo hazitajazwa.

Pia ilibainika kuwa DAWASA haina mtunza ghala ambaye jukumu lake la kila siku ni usimamizi wa mali zilizoko ghalani. Kutokana na kukosekana kwa mtunza ghala, udhibiti wa mali zilizopo ghalani unakuwa ni mdogo.

Ukaguzi uliofanyika Katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ulithibitisha kuwa Shirika lilikua na upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika maeneo ya mipakani kwenye vituo vya kukagulia bidhaa kabla ya kuingizwa nchini. Kati ya vituo vya ukaguzi hamsini na mbili (52) vilivyopo nchini ni vituo vitano (5) tu ndivyo ambavyo vina wakaguzi wa TBS. Hii ina maana kwamba bidhaa nyingi zinaingizwa nchini bila kukaguliwa au kupimwa na TBS. Ukosefu wa wafanyakazi unaweza kusababisha matatizo makubwa ikiwa ni pamoja na kuingizwa nchini kwa bidhaa zisizokidhi viwango na zenye madhara.

Tathmini ya muundo wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (MWEKA) ilithibitisha kuwa kuna nafasi zilizokuwa wazi za Mkaguzi wa Ndani na Afisa Mipango. Nafasi hizi ni muhimu kujazwa ili chuo kifanye kazi kwa ufanisi. Kuchelewa kujaza nafasi hizi kunaweza kusababisha kushindwa kufikia malengo ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Pia, Maafisa wanaokaimu nafasi zao kwa muda mrefu bila kuthibitishwa wanaweza kupoteza ari ya utendaji wa kazi na uwajibikaji na hivyo kuzorotesha kufikia malengo ya Taasisi husika.

## 7.6 Benki Kuu Kutopitisha Maombi ya Wakuu wa Idara ya Benki ya Wanawake Tanzania

Kifungu cha 19 (4) cha kanuni za Taasisi za Fedha (Udhibiti na Ukaguzi wa Ndani), za mwaka 2005 zinahitaji Benki Kuu ishauriwe juu ya uteuzi wa Mkaguzi wa Ndani kwa kupewa taarifa za awali kwa ajili ya kufanya upekuzi kabla ya kumthibitisha.

Tathmini ya ukaguzi ilibaini kuwa Benki ya Wanawake Tanzania iliishauri BoT juu ya uteuzi wa mkaguzi wa ndani kwa ajili ya upekuzi kupitia barua yao yenye kumbukumbu Na.TWB / HQ / VET / 06-13 / 04 ya tarehe 27 Juni, 2013. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi kutoka Benki Kuu kujibu barua wala hatua za kufuatilia kutoka Benki ya Wanawake. Vile vile kiutaratibu, Wakuu wa Idara lazima wafanyiwe upekuzi na Benki Kuu kabla ya kuthibitishwa na Benki husika. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa hakuna ushahidi wa Benki kupokea kibali kutoka Benki Kuu kwa ajili ya ajira ya Mwanasheria na Mkuu wa Uendeshaji. Benki inaweza kulipa faini kwa kushindwa kutekeleza sheria na kanuni.

## 7.7 Kutokuwepo Mpango wa Kurithisha Madaraka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga

Menejimenti ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga inaundwa na wafanyakazi wenye uzoefu na ujuzi. Mamlaka ina sera ya kuwapa mafunzo sahihi wafanyakazi wake ili kuboresha utendaji wao wa kazi na kuongeza ufanisi kazini. Katika ukaguzi uliofanyika iligundulika kuwa Mamlaka haina mpango wa kurithisha madaraka.

## 7.8 Posho ya Nyumba Iliyolipwa Kinyume na Waraka wa Serikali Na. TYC / T / 200/583/18 katika Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam(DMI)

Wafanyakazi wa Chuo cha Mabaharia wenye ngazi ya mshahara chini ya PGSS18 hupokea posho ya nyumba kwa kiwango cha asilimia 30 ya mishahara yao. Utaratibu huu ni kinyume na waraka wa Serikali Namba TYC/T/200/583/18. Katika mkutano wa kawaida wa Bodi ya DMI uliofanyika tarehe 23 Novemba, 2012, Bodi ilielekeza Menejimenti kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya kulipia posho za nyumba na matengenezo na kuwasilisha pendekezo kwa Bodi kwa ajili ya kibali na hatimaye kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupitishwa kama ilivyoelezwa katika Dokezo la Bodi Na.35/2012. Katika kupitia muhtasari wa kikao cha Bodi kilichofanyika tarehe 23 Novemba, 2012 Taasisi ilishauriwa na Msajili wa Hazina kuwa ni kinyume na utaratibu kukiuka maamuzi ambayo yameshatolewa na Serikali.

## 7.9 Ujira Kulipwa Mara Mbili kwa Wakala wa Mpango wa Pamoja wa Bima

Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) liliingia mkataba na kampuni ya Intertrade Express Ltd mwaka 2007 kama wakala wa kusimamia utekelezaji wa mpango wa pamoja wa bima na kampuni ya bima ya Afrika Life Assurance (T) Ltd. Mwaka 2011, mkataba ulikatizwa na Shirika la Hifadhi za Taifa ilifanya usuluhisho wa hesabu kuangalia kiasi ambacho Shirika lililipa kwa malipo ya bima kuanzia mwaka 2007-2011 na kubainisha kwamba, jumla ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania 957,807,633 hakikuwa kimewasilishwa na wakala kwa kampuni ya Bima. Ilibainika pia kuwa wakala alikuwa akiwasilisha mchango baada ya kufanya makato ya asilimia 10. Pia uchunguzi uliofanyika ulibaini pia kuwa wakala amekuwa akilipwa fedha na kampuni ya Bima. Kitendo cha kuwasilisha makato baada ya kutoa asilimia 10 ni kinyume na kifungu cha 37 na 136 cha Sheria ya Bima sura ya 394 ya mwaka 2002 ambayo inamtaka wakala kulipwa na Kampuni ya Bima. Pia ilibainika kuwa, kwa mujibu wa Mkataba kati ya Shirika na Wakala, Wakala hakutakiwa kulipwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa ajili ya huduma zilizotolewa na Kampuni ya Bima.

Nilibaini pia kuwa, Wakala alikataa kuweka wazi kiasi alichokuwa amekata kabla ya kuwasilisha fedha za Shirika la Hifadhi za Taifa kwenye Kampuni ya Bima na kiasi alicholipwa baada ya kuwasilisha fedha ambazo amekwisha zikata kwa kipindi chote kati ya 2007-2011 ambavyo ni kinyume na kifungu B.3(f) cha Kanuni za Maadili ya Bima Tanzania ambazo huzuia kufanyika kwa malipo yoyote kwa kuongeza makato bila kuonyesha lengo la makato hayo. Shirika la Hifadhi za Taifa iliiandikia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) tangu Septemba, 2013 kutafuta ufumbuzi wa kurudishiwa makato yaliyofanyika kinyume na utaratibu bila mafanikio.

## 7.10 Mapungufu Katika Kupitisha Gharama Zinazohusiana na Mishahara

Katika tathmini yangu ya kazi za rasilimali, ilionekana kuwa kitengo cha rasilimali watu cha Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hakikushirikishwa katika kuidhinisha baadhi ya marupurupu ya wafanyakazi. Marupurupu ambayo hayajapitiwa na hayana idhini ya idara ya rasilimali watu ni pamoja na posho ya kufanya kazi masaa ya ziada na malipo mengineyo ambayo ni sehemu ya mishahara ya wafanyakazi.

Kifungu cha 5.4 kifungu kidogo cha iv (a) - (b) cha kanuni za utumishi za Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA), kinahitaji malipo ya kufanya kazi masaa ya ziada kuidhinishwa na mwenye mamlaka na pawe na uhitaji wa kufanya kazi kwa muda wa ziada na uthibitisho

kuwa kazi haiwezi kukamilika katika masaa ya kawaida. Aidha maombi ya kulipwa masaa ya ziada yanahitaji idhini ya mkuu wa idara na afisa msimamizi baada ya kujazwa kwa fomu inayoonyesha jina na saini ya idhini kutoka kwa mkuu wa idara ya fedha.

Ukaguzi wa posho za kufanya kazi muda wa ziada katika Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) ulibainisha kuwa katika baadhi ya malipo, sababu na kibali cha maombi ya kufanya kazi muda wa ziada havikupatikana. Fomu zilikua zikijazwa na kupitishwa kwenye mfumo wa malipo kabla ya idhini na malipo kuongezwa kwenye sehemu ya mshahara.

## 7.11 Haja ya Kubadili Mpango wa Matibabu Katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Mpango wa matibabu wa sasa wa Shirika la Viwangoa Tanzania (TBS) unahitaji wafanyakazi kulipia huduma zao za matibabu kwa fedha taslimu na kuwasilisha madai TBS kwa ajili kurudishiwa pesa walizotumia kwenye matibabu. Utaratibu huu wa sasa unasababisha taarifa za afya ambazo ni siri za watumishi kuhusu magonjwa yao kujulikana kwa wafanyakazi na kuondoa dhana ya kuwa ugonjwa ni siri ya daktari na mgonjwa. Pia, kutokana na utaratibu huu inaweza kuwawia vigumu baadhi ya wafanyakazi wa shirika kupata huduma za matibabu wakati wa dharura. Shirika linapaswa kutumia Mifuko ya Bima ya Afya iliyoko sokoni ili kulipunguzia gharama za matibabu kwa Wafanyakazi ambazo zingeweza kuepukika.

## 7.12 Mabadiliko ya Muundo wa Mishahara VETA kwa Mwaka 2013/2014 Bila Idhini ya Msajili wa Hazina

Menejimenti ya VETA ilibadili Mfumo wa mishahara wa mwaka 2013/2014 bila idhini ya Msajili wa Hazina ambapo ni kinyume na waraka wenye kumbukumbu Na. SHC/B.40/6/21 wa tarehe 28 Machi, 1994. Pia nilibaini kuwa, wafanyakazi wenye taaluma sawa walikuwa wakilipwa mishahara tofauti kwa maelezo kuwa walizingatia vigezo vya uzito wa kazi na muda ambao mtumishi ametumikia. Hata hivyo, vigezo vilivyotumika havikua vimeandikwa popote kwenye mpango wa watumishi au kanuni za wafanyakazi. Mabadiliko yoyote yaliyotolewa kuhusu stahili za wafanyakazi yalitakiwa kuwa na nyaraka zinazoonyesha kuwa utaratibu huu umepitishwa na mamlaka husika.

## 7.13 Udhaifu Uliobainishwa Kwenye Makato ya Kisheria Yaliyotolewa na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mapitio ya gharama za mishahara yalibainisha mapungufu kadhaa katika makato ya kisheria yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania. Makato ya kisheria ya NSSF yalifanywa kwa watumishi

ambao aidha walikua wamefariki au wamestaafu. Makato hayo yaliyolipwa zaidi ni kiasi cha Shilingi za Kitanzania milioni 488.8 kwa ajili ya bandari ya Dar es Salaam.

**Jedwali 11:Makato ya kisheria yaliyolipwa zaidi NSSF na Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam**

| Mwezi | Kiasi kilichotakiwa kupelekwa NSSF (Sh.) (a) | Kiasi Kilichopelekwa (Sh.) (b) | Kiasi Kilicholipwa zaidi (b-a) |
|---|---|---|---|
| Nov-13 | 297,113,403 | 414,092,407 | 116,979,004 |
| Des-13 | 310,150,123 | 408,046,648 | 97,896,525 |
| Machi-13 | 372,252,662 | 646,263,034 | 274,010,372 |
| | | | **488,885,901** |

Tofauti kadhaa zilibainika kati ya kiasi kilichopelekwa na kiasi kinachoonyeshwa katika muhtasari wa mishahara kuhusiana na PAYE na SDL. Matokeo yake makato ya kisheria ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.35 yalilipwa zaidi na Makao Makuu ya Bandari, Bandari za Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Kyela kama jedwali hapa chini linavyoonyesha:

**Jedwali 12:Kiasi cha PAYE na SDL kilicholipwa zaidi (Bandari Makao makuu, Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Kyela)**

| Mwezi | Makato | Kiasi kwa mujibu wa muhtasari wa mishahara (Sh.) | Jumla (a) (Sh.) | Kiasi kwa mujibu wa malipo yaliyofanyika (b) (Sh.) | Tofauti (a-b) (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| Julai-13 | PAYE | 627,865,260 | 767,662,852 | 1,258,483,770 | (490,820,918) |
| | SDL | 139,797,592 | | | |
| Aprili-14 | PAYE | 706,789,134 | 860,988,167 | 1,723,897,786 | (862,909,619) |
| | SDL | 154,199,033 | | | |
| **Jumla** | | **1,628,651,019** | **1,628,651,019** | **2,982,381,556** | **(1,353,730,537)** |

SDL ilikokotolewa kwa kiwango cha asilimia 6 badala ya asilimia 5. Hii ilisababisha makato ya kisheria kuwasilishwa kwa ziada ya Shilingi za Kitanzania bilioni 1.12 kama inavoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo;

**Jedwali 13: Kiasi cha SDL Kilicholipwa Kinyume na Utaratibu – Bandari ya Dar es Salaam**

| Maelezo | Kiasi (Sh.) | Taarifa |
|---|---|---|
| Jumla ya mishahara kabla ya makato | 112,239,868,679 | |
| SDL 6% (a) | 6,734,392,121 | Kiwango kilichokokotolewa na menejimenti |
| SDL 5% (b) | 5,611,993,434 | Kiwango kilichokokotolewa kwa mujibu wa kanuni |
| **Tofauti (a-b)** | **1,122,398,687** | |

Menejimenti wanapaswa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya malipo yote yanayoingizwa kwenye kitabu cha jumla cha Mamlaka na kuhakikisha kuwa malipo yote yanafanyika baada ya kuhakiki viambatanisho muhimu ili hesabu za Mamlaka ziweze kuwa na usahihi na kuzuia Mamlaka kupata hasara zisizo za msingi.

## 7.14 Baadhi ya Gharama za Mishahara Kufanyika Nje ya Mfumo wa PAYTAN Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)

Ukaguzi wa gharama zinazoendana na mishahara pamoja na mishahara ulibaini kuwa katika Chuo cha Wanyama Pori, baadhi ya malipo yake yalifanyika nje ya mfumo wa mishahara (PAYTAN). Ilithibitishwa kuwa jumla ya Shilingi za Kitanzania 55,083,005 zililipwa nje ya mfumo wa mishahara wa PAYTAN. Malipo hayo yalipelekea kutokea kwa makato kidogo ya kisheria ya mchango ya pensheni kutoka kwa wafanyakazi na mwajiri na yale ya PAYE. Chuo kipo katika hatari ya kulipa adhabu kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2006.

## 7.15 Wafanyakazi wa Mikataba wa Shirika la Magazeti Tanzania Kutokua na Mikataba Iliyoboreshwa

Kampuni inatumia wafanyakazi wa muda katika kutekeleza baadhi ya majukumu katika ofisi zake za mikoani. Hata hivyo, ilibainika kuwa idadi kubwa ya wafanyakazi hao wamefanya kazi na Shirika kwa miaka mingi bila kuwa na mikataba rasmi. Kwa mfano, vibarua waliopo Zanzibar wamekuwa wakifanya kazi kwa zaidi ya miaka 8 na mmoja katika mkoa wa Arusha amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 5 bila mkataba rasmi. Shirika linaweza kuwa linakiuka sheria za kazi kwa kutowapa vibarua mikataba halali.

## 7.16 Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Katani Tanzania Aliyestaafu Kukaimishwa Nafasi ya Mkurugenzi Mkuu Bila Mkataba Halali

Tathmini yangu ya rasilimali watu na utawala katika Bodi ya Katani Tanzania umebaini kuwa, Kaimu Mkurugenzi Mkuu alikuwa tayari amestaafu katika umri wa miaka 60 kama inavyotakiwa kisheria. Mkurugenzi huyo mstaafu bado anafanya shughuli zake kama Mkurugenzi wa Bodi bila ya kuwa na Mkataba wa kumpa uhalali wa wadhifa wake. Aidha, nilibaini kuwa halipwi mishahara yake na badala yake analipwa posho ya kukaimu kwa mujibu wa kanuni za Bodi. Kutokana na kukosekana kwa mkataba wa kisheria wa wadhifa wake ni wazi kuwa Bodi haina Mkurugenzi mwenye mamlaka kwa mujibu wa sheria ya bodi ya Katani. Aidha, ukosefu wa mkataba na mshahara unaweza kuwa na athari kubwa juu ya utendaji wake. Bodi ya Katani iliandika barua yenye kumbukumbu. Na.CAC.65/598/01B/ 116 ya tarehe 24 Januari, 2014 kwa Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma kuomba mkataba wa miaka miwili kwa ajili ya Mkurugenzi mstaafu lakini hakuna majibu yaliyotolewa hadi wakati wa kuhitimisha ukaguzi huu.

## 7.17 Kutofanyika kwa Tathmini ya Mafunzo Katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliandaa mpango wa mafunzo kwa mujibu wa sera ya mafunzo ya TPDC ambayo inasema kwamba "mafunzo ya wafanyakazi yanahitaji kufanywa kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo na katika kutekeleza mpango wa maendeleo wa mafunzo kwa wafanyakazi”. Katika kipindi cha mwaka, jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 5.975 zililipwa na Shirika kwa ajili ya mafunzo. Wakati wa ukaguzi niliomba kupewa mpango wa mafunzo na utekelezaji wake kwa ajili ya ukaguzi lakini hapakuwa na ushahidi kama mpango huo uliandaliwa au kutekelezwa na kama ulikuwa unafanyiwa tathmini kila mwisho wa mwaka.

Kanuni za wafanyakazi ambazo zimepitwa na muda zinamtaka mfanyakazi aliyehudhuria mafunzo ya muda mfupi kuwasilisha ripoti ambayo inaonyesha aina ya mafunzo, mada zilizofundishwa, njia zilizotumika kufundishia, manufaa ya mafunzo na mapendekezo. Hata hivyo hakukuwa na ushahidi kuwa wafanyakazi waliopelekwa mafunzoni waliwasilisha taarifa baada ya mafunzo. Kutokana na kukosekana kwa taarifa hizo baada ya mafunzo, ni vigumu kutoa tathmini ya ufanisi wa mipango na mafanikio ya mafunzo na matumizi ya maarifa na stadi zilizopatikana kwenye mafunzo hayo katika sehemu zao za kazi.

# SURA YA NANE

# UTAWALA BORA

## 8.0 Utangulizi

Utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na kufuata utawala wa sheria. Katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma utawala bora unahusu majukumu na mahusiano baina ya menejimenti ya shirika husika, bodi ya wakurugenzi, kamati ndogo za bodi ya wakurungenzi, wanahisa na wadau wengineo. Uwepo wa utawala bora unajenga muundo ambao unahakikisha tija kwa kila mdau anayehusika kwa kuhakikisha uwepo wa maadili na namna bora ya kufanya kazi kwa kufuata taratibu na sheria.

Hivi karibuni, masuala yahusuyo utawala bora katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamezua mijadala kutokana na tuhuma mbalimbali zitokanazo na matumizi mabaya ya madaraka na kesi nyingi za jinai zinazowahusu baadhi ya wafanyakazi wake. Bodi za Wakurugenzi zimekabidhiwa dhamana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia shughuli za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa niaba ya watanzania wote.

Kwa miaka kadhaa, nimekuwa nikitoa taarifa kuhusu mapungufu katika utawala bora na mapendekezo ya namna ya kuyarekebisha. Masuala mengi yaliyohojiwa katika miaka ya nyuma yamefanyiwa kazi na Serikali pamoja na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Nimefarijika na mipango na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali na Mashirika hayo katika kutekeleza mapendekezo niliyoyatoa katika eneo la utawala bora kama ilivyobainishwa na majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kutokana na juhudi hizo, baadhi ya mapendekezo yametekelezwa na mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ingawa kumekuwa na utekelezaji wa masuala ya utawala bora, bado kumekuwa na mapendekezo ambayo yalitolewa katika ripoti zangu za nyuma ambayo bado yanajirudia kila mwaka.

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa katika ripoti zilizopita na ambayo hayajafanyiwa kazi ni pamoja na kukosekana kwa kanuni za uendeshaji wa Bodi za Wakurugenzi, uwepo wa Wabunge katika Bodi za Wakurugenzi, udhaifu katika utendaji wa Idara za Ukaguzi wa Ndani, kutokuwa na wajumbe wenye taaluma ya uhasibu au fedha

katika Kamati za Ukaguzi za Bodi za Wakurugenzi, kutoandaliwa kwa umakini kwa mipango ya ukaguzi wa ndani na kuwa na watumishi wachache katika Idara za Ukaguzi wa Ndani kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Wakati wa ukaguzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kuwepo kwa masuala kadhaa ambayo ni kinyume na kanuni na taratibu za utawala bora. Masuala hayo yameainishwa kama ifuatavyo;

## 8.1 Kukosekana kwa Miongozo ya Uendeshaji wa Shughuli Mbalimbali za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Miongozo au kanuni ni maelekezo yanayoainisha hatua za kiutekelezaji. Miongozo hiyo inalenga kuwepo mpango wa utekelezaji wa masuala mbalimbali kufuatana na kanuni bora za utendaji. Kanuni bora za utendaji zinahitaji majukumu mbalimbali ya utekelezaji kuhifadhiwa kimaandishi ili majukumu hayo yawe na miongozo stahiki.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2013/2104 nilibaini kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikuwa na miongozo ya uendeshaji au miongozo hiyo ilikuwa imepitwa na wakati kama ifuatavyo; Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) hakikuwa na miongozo ya uendeshaji wa shughuli za hospitali; Bodi ya Bima za Amana (DIB) haikuwa na miongozo ihusuyo ufilisi, ulipaji amana na miongozo ya uwekezaji; Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) haikuwa na taratibu za uendeshaji wa kuhudumia malalamiko ya wateja, usomaji mita, utoaji ankara, ukusanyaji mapato, uunganishaji wa maji, ukataji wa maji na uunganishaji upya wa maji yaliyokatwa, ukusanyaji wa madeni na masuala ya tekinolojia ya habari na mawasiliano.

Mashirika mengine ni, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) ambacho kilikosa miongozo ya ukaguzi wa ndani, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) hakikuwa na miongozo ya usajili wa makampuni yenye ukomo wa madeni, katika Benki ya Wanawake hakukuwa na Sera ya Fedha na ile ya kusimamia viashiria vya hatari. Katika taasisi ya CARMATEC hakukuwa na sera, taratibu au kanuni za kuongoza masuala ya uzalishaji, utafiti, usimamizi wa viashiria vya hatari, masuala ya nyumba na sera ya kuzuia ubadhirifu (fraud), wakati katika Taasisi ya Utafiti wa Viatilifu vya Kudhibiti Visumbufu katika Ukanda wa Tropiki (TPRI) hakukuwa na sera ya utumishi kama ilivyotakiwa na kanuni za fedha za taasisi hiyo, katika Shirika la Utangazaji la Taifa sera ya mawasiliano ikiwemo sera ya uokoaji wa taarifa muhimu za shirika ilikuwa haijapitishwa na mamlaka husika tangu mwaka 2010, katika Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji halikuwa na kanuni za utumishi na mpango wa ulipaji wa mishahara kwa wafanyakazi.

Kutokuwepo kwa miongozo ya kimaandishi kuhusiana na shughuli au kazi za Taasisi, kunaweza kusababisha udhaifu katika kufanya tathmini ya menejimenti na wadau wengine juu ya shughuli za kiutendaji na udhibiti wa ndani wa Taasisi husika.

## 8.2 Uundwaji wa Baraza la Ushauri la Shirika la Masoko Kariakoo Kinyume na Sheria ya Masoko ya Kariakoo ya Mwaka 1974

Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 1984. Kifungu Na. 5 (2) (a) na (b) cha sheria ya uanzishwaji wa shirika hilo kinatamka kwamba mwenyekiti wa Bodi atateuliwa na Rais wakati wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana.

Uendeshaji wa Shirika la Masoko Kariakoo kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wa shirika umewekwa chini ya Bodi ya Wakurugenzi, ambapo shughuli za kila siku hufanywa na Mkurugenzi Mkuu atakayeteuliwa na Rais kama inavyoelezwa katika kifungu namba 5(5) cha sheria hiyo.

Nimebaini kuwa Shirika hilo limekuwa likiendeshwa bila chombo halali cha usimamizi tangu mwaka 2000 baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Bodi ya Wakurugenzi na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kutumia kifungu Na. 7(1) cha Sheria ya Masoko Kariakoo ingawa kifungu hicho hakimpi mamlaka hayo Waziri na hivyo maamuzi hayo kuwa ni kinyume cha sheria.

Kutokana na kuvunjwa huko kwa Bodi ya Wakurugenzi, uendeshaji wa Shirika hilo uliwekwa chini ya Jiji la Dar es Salaam ambalo liliteua Baraza la Uendeshaji kama chombo cha uangalizi wa shirika kinyume na kifungu Na. 5(2) (a) na (b) cha Sheria ya Masoko ya Kariakoo. Zaidi ya hayo, Mkurugenzi Mkuu ambaye alitakiwa kuteuliwa na Rais aliteuliwa na Waziri kinyume na kifungu cha 5(4) cha Sheria hiyo.

Ukiukwaji huo wa Sheria ya uanzishwaji wa Shirika kunafanya uwepo wa Baraza hilo la uendeshaji kutokuwa halali na hivyo maamuzi yote yaliyofanywa katika kipindi hicho kuwa kinyume cha Sheria.

Kutokana na ukiukwaji huo wa Sheria, sikuweza kutoa maoni yangu ya ukaguzi kwa hesabu za Shirika hilo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2014 mpaka pale Mamlaka husika itakapotatua ukiukwaji wa sheria

kwa kufuata matakwa ya Sheria hiyo ili kuendana na kanuni za utawala bora.

## 8.3 Ucheleweshwaji wa Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania analo jukumu la kuwateua wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi. Wajumbe wengine huteuliwa na Mawaziri wenye dhamana za Mashirika husika. Katika ripoti zangu zilizopita nimekuwa nikiandika juu ya ucheleweshwaji wa uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi ambapo majibu ya Serikali yamezungumzia juu ya waraka namba SAB 55/204/01/159 wa Septemba 2010 ukiwaeleza maafisa masuuli kupendekeza wajumbe wapya wa Bodi miezi sita (6) kabla ya kipindi cha Bodi kuisha. Kama katika miaka iliyotangulia, ucheleweshwaji wa uteuzi wa Bodi umendelea kuonekana katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Wakati wa ukaguzi wa masuala ya utawala bora katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nilibaini kuwa muda wa Bodi kadhaa ulikuwa umekwisha pasipo kuwa na hatua za kuteua Bodi mpya. Kuchelewa kuteuliwa kwa Bodi za Wakurugenzi kuna madhara katika utendaji wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Miongoni mwa madhara hayo ni pamoja na kutoweza kuajiri wafanyakazi katika ngazi za juu, kuidhinisha makadirio, kufanya maamuzi ya kimkakati, kufuatilia masuala ya kimaadili katika kutoa ripoti na kuidhinisha hesabu za Mashirika na Taasisi zao.

Hadi wakati wa kuandaa ripoti hii kulikuwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kumi na sita (16) ambazo Bodi zake zilikuwa zimekwisha muda wake. Mashirika hayo ni Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFIRI), Chuo cha Mipango (IRDP), Bodi ya Katani Tanzania, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Bodi ya Pareto Tanzania, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika ya Elimu Kibaha (KEC), Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CARMATEC), Makumbusho ya Taifa, Kamisheni ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi (NLUPC), Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) na Shirika la Masoko Kariakoo.

Zaidi ya hayo, nilibaini kwamba, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yamekuwa yakifanya kazi bila ya Bodi za Wakurugenzi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Mashirika hayo ni Shirika la Masoko ya Kariakoo, ambalo limefanya kazi bila Bodi kwa takriban

miaka kumi na minne. Mashirika mengine ni Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), Makumbusho ya Taifa na Bodi ya Sukari Tanzania ambayo yamekosa Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Nimebaini pia, kuwa Shirika la Elimu Kibaha (KEC), halikuwa na mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wengine watatu na hivyo kuifanya Bodi hiyo kutokamilika, hali ambayo imezuia utekelezaji wa kazi muhimu zilizohitaji idhini ya Bodi.

## 8.4 Idadi Kubwa ya Wajumbe wa Bodi Kinyume na Sheria ya Uanzishaji wa Shirika

Mapitio ya miundo ya Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma yalibaini kuwa baadhi ya Bodi za Wakurugenzi zilikuwa na wajumbe zaidi ya idadi iliyotajwa katika Sheria iliyoanzisha mashirika hayo.

Kwa mfano, kulingana na Jedwali la kwanza la Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009, idadi ya wajumbe wa bodi inapaswa kutozidi wajumbe kumi. Hata hivyo ilibainika kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Chalinze ilikuwa na wajumbe kumi na moja kinyume na matakwa ya Sheria.

Ukiukwaji huo wa sheria una athari katika ongezeko la gharama za Bodi za Wakurugenzi ambazo zingeweza kuepukwa. Hivyo, ninashauri kwamba, mamlaka hiyo iwasiliane na mamlaka ya uteuzi ili kurekebisha upungufu uliojitokeza kwa lengo la kufuata matakwa ya sheria.

## 8.5 Mapungufu katika Udhibiti wa Ndani wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

### 8.5.1 Kutokuwepo kwa Kamati za Ukaguzi na Kufanya Kazi bila Ufanisi kwa Kamati Hizo

Kamati ya Ukaguzi ni kamati ndogo ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo kazi yake kubwa ni kuishauri Bodi ya Wakurugenzi katika kutimiza majukumu yake ya uangalizi na usimamizi. Kazi hizi ni pamoja na; kusimamia ubora wa taarifa za hesabu za taasisi, kuajiri, usimamizi uchaguzi wa sera na kanuni za kiuhasibu, kusimamia udhibiti wa ndani, kusimamia utii wa sheria na maadili, kusimamia utendaji kazi wa mkaguzi wa ndani, kujadili na kutoa maelekezo kwa menejimenti kuhusu sera za usimamizi wa viashiria vya hatari.

Wakati wa kutathmini utendaji kazi wa kamati za ukaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, nilibaini kutokuwepo kwa Kamati ya

Ukaguzi katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) kwa mwaka mzima na hivyo kusababisha mpango wa ukaguzi wa ndani kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji, utaratibu ambao husababisha mgongano wa kimaslahi na ni kinyume na kanuni za utawala bora kwa sababu idara za ukaguzi wa ndani hazipaswi kutoa taarifa za kikazi kwa Mkurugenzi Mtendaji. Nilibaini pia kuwa katika Kituo cha Uwekezaji (TIC) hakukuwa na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya mkaguzi wa ndani. Hali hii inaashiria udhaifu wa kazi za ukaguzi wa ndani katika kituo hiki.

Katika Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Kamati ya Ukaguzi haikufanya kazi yeyote katika mwaka husika. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA) Kamati ya Ukaguzi haikufanya mapitio ya ripoti ya mkaguzi wa ndani. Katika Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kamati ya ukaguzi ilikutana mara mbili tu na hivyo kusababisha baadhi ya taarifa za mkaguzi wa ndani kutojadiliwa.

Mashirika mengine ambayo hayakuwa na kamati za ukaguzi ni Taasisi ya Mifupa (MOI), Shirika la Maendeleo Tanzania (NDC), CARMATEC, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Chalinze na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA).

### 8.5.2 Kamati za Ukaguzi za Bodi Kutokuwa na Wajumbe Wenye Taaluma ya Uhasibu au Fedha

Kamati ya ukaguzi ikiwa kamati ya kitaalam ya Bodi ya Wakurugenzi ina jukumu la kuishauri Bodi ya Wakurugenzi katika kutimiza majukumu yake ya uangalizi na usimamizi, hivyo Kamati hii ni muhimu katika muundo wa utawala bora.

Katika uundaji wa kamati hizi za ukaguzi, idadi kubwa ya wajumbe ni lazima wawe wajumbe huru kutoka nje ya Taasisi. Kamati za Ukaguzi hufanya uangalizi kwa kutoa ushauri na maoni kwa Bodi kuhusu utawala bora, usimamizi wa viashiria vya hatari, na udhibiti wa ndani kuhakikisha kwamba mifumo hiyo imeundwa vizuri na kufanya kazi kukidhi mahitaji ya malengo ya Taasisi husika.

Kulingana na kanuni za utawala bora, ili Kamati za Ukaguzi ziweze kufanya kazi zake kwa umakini na kuwa na maamuzi bora na huru, baadhi ya wajumbe wake ni sharti wawe na taaluma ya uhasibu au fedha.

Hata hivyo, ukaguzi wa mwaka huu umebaini kuwa baadhi ya kamati hazikuwa na wajumbe wenye taaluma ya uhasibu au fedha na hivyo kusababisha ugumu wa Taasisi hizo kufanya tathmini ya taarifa za

fedha, viashiria vya hatari na uundaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani wa Taasisi.

Mifano ya Mashirika na Taasisi ambazo hazikuwa na wajumbe wenye taaluma ya uhasibu na fedha ni Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (PSPF), Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Mamlaka ya Udhibiti ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

### 8.5.3 Udhaifu wa Utendaji Kazi wa Idara za Ukaguzi wa Ndani

Ufanisi wa vitengo vya ukaguzi wa ndani ni sehemu muhimu katika upimaji wa umadhubuti wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika utendaji wa Taasisi. Uimara wa kitengo cha ukaguzi wa ndani unategemea nafasi ya kitengo katika muundo wa Taasisi, namna ya utoaji taarifa katika muundo wa shirika na idadi ya watumishi wenye sifa stahiki.

Wakati wa mapitio ya kazi za ukaguzi wa ndani za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma nilibaini kwamba idara nyingi za ukaguzi hazikuwa na idadi ya wafanyakazi ya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Hali hii ilibainika katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) ambapo idara ya ukaguzi ilikuwa na watumishi wawili tu waliofuzu na mmoja ambaye bado alikuwa anaendelea na mafunzo wakati idadi ya watumishi waliokuwa wakihitajika ilikuwa ni watano na hivyo kusababisha kutokamilika kwa kazi za ukaguzi. Katika Chuo Kikuu cha Dodoma, ilibainika kucheleweshwa kwa ukaguzi na kutoandaaliwa kwa mpango kazi wa ukaguzi kutokana na upungufu wa wafanyakazi katika idara ya ukaguzi. Ikilinganishwa ukubwa wa shughuli za Chuo Kikuu kuwa na wakaguzi watatu tu ambapo wawili ndio wenye sifa, inazorotesha uwezo wa kitengo cha ukaguzi katika chuo hiko katika utekelezaji wa mpango wa ukaguzi wa mwaka. Upungufu huo umeendelea kudumu kwa zaidi ya miaka mitatu.

Nilibaini pia kwamba katika Chuo cha Ardhi (ARU) na Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi (TAFIRI) kulikuwa na upungufu wa wafanyakazi katika kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), kulikuwa na mkaguzi mmoja tu wa ndani ambaye alikuwa akifanya kazi zote za ukaguzi. Katika Taasisi ya Utafiti wa Viatifilifu katika Ukanda wa Tropiki (TPRI) kulikuwa pia na upungufu wa wafanyakazi katika idara ya ukaguzi. Tatizo hili la upungufu wa wafanyakazi katika

idara ya ukaguzi wa ndani lilibainika pia katika Mamlaka ya Ukanda waa Uwekezaji Tanzania (EPZA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Pia, wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini mapungufu mbalimbali yahusuyo uandaaji wa mpango mkakati wa kaguzi za ndani na mpango wa mwaka wa kaguzi za ndani kama ifuatavyo; Katika Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) mpango wa mkakati ikiwa ni njia mojawapo ya utekelezaji ya mpango mkakati wa usimamizi wa viashiria vya hatari ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango mzima wa ukaguzi wa ndani ulikuwa haujaandaliwa na chuo kikuu hicho. Pia, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga haikuwa na mpango wa mkakati wa ukaguzi wa ndani. Ilibainika pia mpango kazi wa ukaguzi wa mwaka haukuwasilishwa kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na hivyo kusababisha kazi nyingi za ukaguzi wa ndani kufanywa pasipo kuidhinishwa.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo hazikuwa na mipango ya ukaguzi iliyoidhninishwa ni pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi, Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA). Wakati, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA), ilikuwa na mpango mzuri wa ukaguzi wa ndani ambao haukuweza kutekelezwa kiukamilifu na hivyo kutokuwa na ripoti ambayo ingesaidia uboreshaji wa mamlaka hiyo.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambayo mipango yake ya ukaguzi haikutekelezwa kiukamilifu ni Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA). Pia ilibainika kwamba Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam (DIT) kina mpango wa ukaguzi ambao haukuzingatia viashiria vya hatari. Katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, ilibainika kwamba, mpango wa ukaguzi ulioandaliwa haukuzingatia maeneo yote muhimu ya shughuli za Chuo. Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), mpango wa ukaguzi ulioandaliwa haukupitiwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Mapungufu mengine yaliyobainika ni pamoja na ucheleweshwaji wa utekelezaji wa hoja za mkaguzi wa ndani katika Shirika la Elimu Kibaha.

### 8.5.4 Kutokuwapo na Sheria ya Kuanzisha Kamati za Ukaguzi katika Mashirika ya Umma na Kutokuwepo kwa Kamati za Ukaguzi

Ukaguzi wa baadhi ya Mashirika ya Umma ulibaini kuwa kuna taratibu mbalimbali zinazotumiwa katika kuanzisha Kamati za Ukaguzi. Kanuni

ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004) inaeleza uanzishaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali na Mikoa. Sheria hii haielekizi uanzishwaji wa Kamati za Ukaguzi katika Mashirika ya Umma na hivyo hayalazimiki kwa sheria hii kuanzisha Kamati za Ukaguzi. Pia, muundo wa kamati ulioelezwa kwenye Kanuni Na. 31 ya Kanuni za fedha za Mwaka 2001 inawataka wajumbe wa kamati za ukaguzi wawe maafisa wa ngazi za juu wa Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali na Mikoa wakati ambapo Mashirika ya Umma yameanzisha Kamati za Ukaguzi kwa kufuata misingi ya kanuni za utawala bora. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mkanganyiko katika uundaji wa kamati za ukaguzi za Mashirikia na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mfano, katika Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania ambapo Kamishna na Naibu Kamishna walikuwa wajumbe wa kamati ya ukaguzi.

Ukaguzi huo ulibaini kutokuwepo kwa Kamati za Ukaguzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same, Bodi ya Korosho Tanzania na Shirika Hodhi la Rasilimali za Reli Tanzania (RAHCO).

## 8.6 Kutokuwepo kwa Miongozo ya Ukaguzi wa Ndani kwa Baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma

Ukaguzi wa ndani ni kazi huru ya ukaguzi na ya kiushauri yenye lengo la kuweka taarifa sahihi za Shirika na hivyo kuongeza thamani na kuboresha utendaji wa shughuli za Shirika. Pia husaidia taasisi kukamilisha kazi zake kwa kuweka mfumo maalum wa kutathmini na kuboresha udhibiti wa viashiria hatarishi na kuimarisha utawala bora. Ukaguzi wa ndani ni chachu katika kuboresha utawala bora katika Taasisi na kudhibiti viashiria vya hatari kwa kutoa mapendekezo kulingana na uchambuzi wa taarifa mbalimbali za shughuli za taasisi.

Kama ilivyo kwa Bodi za Wakurugenzi na Kamati za Ukaguzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pia kinapaswa kiwe na miongozo ya utendaji wa ukaguzi ambayo itaongoza kitengo katika utendaji kazi wake wa kuishauri Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi kuhusu njia bora ya kutekeleza majukumu yao.

Mashirika ambayo hayakuwa na miongozo ya utendaji kazi ni Shirika la Elimu Kibaha (TEC), Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA CCC). Mwongozo wa Ukaguzi wa ndani katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) haikupata idhini ya bodi na hivyo kazi za uangalizi za Bodi na Kamati za Ukaguzi za Bodi hazikuweza kudhihirika.

## 8.7 Uwezekano wa Kuwepo kwa Muingiliano wa Madaraka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Muingiliano wa udhibiti ni hali ambayo hutokea iwapo makampuni yanaweza kutumia udhaifu uliopo katika mifumo ya udhibiti ili kukwepa kanuni ambazo zinawabana. Hali hii inatokana na kuwepo na zaidi ya mdhibiti mmoja katika sekta zenye kanuni tofauti bila kuwepo kwa mipaka inayoeleweka.

Wakati wa ukaguzi wa kazi za Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), nimebaini kwamba Sheria No. 8 ya Udhibiti wa Mifuko ya Jamii ya mwaka 2008 inataja wadhibiti wawili wa sekta ya Hifadhi ya Jamii. Pamoja na mamlaka yenyewe kuwa na udhibiti wa mifuko, pia Benki Kuu imepewa nguvu ya udhibiti kwenye masuala ya usimamizi wa fedha za mifuko ikiwemo udhibiti wa akiba ya fedha, uangalizi wa uwekezaji na kutoa maamuzi ya kiuwekezaji ambazo zote ni kazi za msingi za mifuko ya hifadhi ya jamii.

Uwepo wa wadhibiti wawili unaweza kusababisha muingiliano hasa kwenye usimamizi wa uwekezaji ambao ni eneo muhimu katika sekta husika. Hii inaweza kusababisha mifuko kuegemea kwenye mapungufu katika mfumo wa udhibiti ili kukwepa mahitaji ya udhibiti yanayowakabili.

Pia, wadhibiti hao wawili wanaweza wasiwe na maono ya aina moja katika baadhi ya mambo yaliyopo kwenye kanuni zinazotawala sekta hii na hivyo kutoa nafasi kwa Taasisi zinazodhibitiwa kutumia mwanya unaoweza kutokana na kutokuelewana kwa wadhibiti hawa wawili na hivyo kutokea kwa viashiria vya kutotii mamlaka za udhibiti.

## 8.8 Uwezekano wa Kuwepo kwa Muingiliano wa Kimaslahi kati ya Bodi za Wakurugenzi za DAWASA na DAWASCO

Bodi ya wakurugenzi ni chombo kinachochukua majukumu ya kutambua maeneo yenye viashiria vya hatari katika taasisi, kutoa maamuzi na usimamizi wa uwekezaji, kutoa maamuzi katika masuala ya fedha na kutathmini ufanisi wa mipango ya kibiashara na makisio. Bodi pia zina jukumu la kuhakikisha mfumo kamili wa udhibiti wa ndani na kanuni za utawala bora zinafuatwa ili kuzingatia maslahi ya Taasisi zinazoisimamia.

Katika mapitio ya miundo ya Bodi za Wakurugenzi ya DAWASA na DAWASCO kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na ile ya Bodi ya DAWASCO katika kipindi cha kuanzia mwaka 2014/2015 ilibainika kwamba mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA ni mjumbe wa Bodi ya

DAWASCO na Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASCO ni mjumbe wa Bodi ya DAWASA.

Kwa kuzingatia kuwa DAWASCO wameingia mkataba wa utumiaji wa miundo mbinu ya DAWASA na kwamba kila upande una haki na wajibu wake ndani ya mkataba huo, hivyo kwa Mwenyekiti wa Bodi moja kuwa mjumbe katika Bodi nyingine kutazinyima Bodi hizo kujadili maslahi ya taasisi wanazozisimamia kama ilivyo katika mkataba au maslahi mengine ya kibiashara ambayo hayako kwenye mkataba kwa uhuru na uwazi.

Naishauri mamlaka ya uteuzi, kuangalia uwezekano wa kurekebisha muundo wa wajumbe wa Bodi hizo kuondoa mgongano wa kimaslahi ambao unaweza kujitokeza kutokana na uhusiano uliopo ambapo wenyeviti wa Bodi za DAWASA na DAWASCO kuwa wajumbe wa bodi za DAWASCO na DAWASA. Badala yake Bodi hizo zitengeneze utaratibu wa mawasiliano ambapo wawakilishi wa Bodi za Wakurugenzi watajadili masuala ya maslahi ya pamoja kuepuka mgogoro wowote wa kimaslahi unaoweza kujitokeza.

## 8.9 Kutokuwepo kwa Miongozo ya Bodi za Wakurugenzi

Miongozo ya Bodi hutoa maelekezo kwa Wajumbe wa Bodi juu ya utawala na mwelekeo wa Taasisi. Miongozo hutoa taratibu za uendeshaji na taarifa kuhusu muundo na utendaji wa wajumbe wa Bodi, kazi zao na wajibu wao. Miongozo hii pia hutoa miiko ya maadili, miiko ya utendaji kazi ikiwemo sera ya migongano ya kimaslahi, mahudhurio ya mikutano ya Bodi, taratibu za kutathmini utendaji kazi wa Bodi, taratibu za kutathmini utendaji kazi wa Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, Maelezo kuhusu wajumbe wa Bodi, Kalenda ya Bodi pamoja na mpango kazi wa Bodi.

Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibaini Bodi za Wakurugenzi ambazo hazina miongozo ya kusimamia shughuli zake. Taasisi hizo ni DAWASCO na Baraza la Ushauri kwa walaji EWURA (EWURA CCC). Kutokuwepo kwa miongozi ya Bodi kwaweza kusababisha kushindwa kwa bodi kutimiza wajibu wake ipasavyo.

## 8.10 Kutokuwepo kwa Daftari la Viashiria Hatarishi

Ili kuwa na utendaji kazi ulio bora, utawala bora, mpango mzuri wa udhibiti wa viashiria hatarishi wa taasisi unahitaji kuunda na kuwa na mchakato endelevu utakaosaidia utambuzi, tathmini na jinsi ya kushughulikia viashiria hatarishi kwa taasisi husika.

Ili kuweza kuandaa mpango wa menejimenti ya viashiria vya hatari, ni muhimu kuandaa daftari la viashiria hatarishi litakalokusanya viashiria vya hatari vyenye athari kwa Taasisi. Daftari hili litatumika kama hifadhi kuu ya taarifa ya viashiria hatarishi na kuwezesha taarifa hizi kuchambuliwa, kuwekwa katika viwango stahiki na kuunganishwa na ngazi husika ya utawala wa Taasisi.

Kazi muhimu ya daftari hili ni kuipa menejimenti, Bodi za Wakurugenzi au Mabaraza na wadau wengine taarifa muhimu kuhusu viashiria vya hatari vinavyoikabili Taasisi. Pia, huwapa wadau mtazamo kuhusu hali ya sasa ya kila kiashiria cha hatari kwa kila wakati.

Wakati wa ukaguzi wa udhibiti wa viashiria hatarishi nilibaini mapungufu kadhaa katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambayo ni pamoja na kutoidhinishwa na Baraza la Chuo kwa daftari la viashiria hatarishi katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), hivyo kulifanya daftari hilo kutokuwa nyaraka halali na Menejimenti kushindwa kulitumia. Hali hii yaweza kusababisha athari kwa Chuo hiki Kikuu.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo hazikuwa na daftari la viashiria hatarishi ni Chuo Kikuu cha Ardhi, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA). Taasisi nyingine ni Shirika la Elimu Kibaha (KEC), Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili (MUHAS) na Kituo cha Kansa cha Ocean Road (ORCI).

## 8.11 Kukaimu Nyadhifa za Juu kwa Kipindi cha Muda Mrefu

Viongozi wakuu au viongozi wandamizi katika taasisi ni timu ya watu walioshika nyadhifa za juu katika uongozi na wenye majukumu ya kila siku ya kuongoza Taasisi au shirika.

Viongozi hawa wanashikilia nafasi za juu za kimaamuzi walizopewa na mamlaka husika ya uteuzi kama vile Bodi za Wakurugenzi au Waziri wa sekta husika. Hawa wote ni wawakilishi wa wanaomiliki kampuni au Shirika.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa baadhi ya nyadhifa za juu katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zilikuwa zikishikiliwa kwa kukaimishwa.

Mfano wa nafasi iliyokaimishwa ni ya Meneja Mkuu wa Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MSRU) ambapo nafasi hiyo ipo wazi tangu Octoba, 2012. Mamlaka ya uteuzi wa Meneja Mkuu ni

Waziri wa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi. Nafasi nyingine zilizokaimishwa ni za Manaibu Waangalizi (Wardens) wenye dhamana ya 'Dar es Salaam Marine Reserve' (DMRs) na 'Tanga Coelacanth Marine Park' (TACMP). Hali hii inaathiri utendaji wa taasisi hiyo kwa kuwa maamuzi makubwa ya uendeshaji wa Shirika hayafanyiki kwa wakati. Pia, katika Shirika la Bima ya Afya (NHIF), nafasi ya Mkurugenzi Mkuu imekuwa wazi baada ya kustaafu kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu miaka miwili iliyopita. Tangu wakati huo Bodi ilimteua Kaimu Mkurugenzi Mkuu ikisubiri taratibu za ajira kukamilika. Hali hii ni kinyume na Aya Na. D.25 (3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma inayotaka nafasi wazi zisikaimiwe kwa zaidi ya miezi sita (6).

## 8.12 Kuchelewa kusaini Mikataba na Bodi za Wakurugenzi

Kifungu Na. 10 (2) (k) cha Sura ya 370 ya sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2002 pamoja na ile ya Mashirika ya Umma ya 1992 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 zinamtaka Msajili wa Hazina kutia saini mikataba ya makubaliano ya malengo baina yake na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mikataba hiyo ikiwa na nia ya kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Bodi na kuinua mapato na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa upande mwingine, mikataba na Bodi ya Wakurugenzi ni muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa vigezo vya kufuatilia uwajibikaji na utawala bora. Hali kadhalika, mikataba hii katika utawala bora ni muhimu ili kuinua uwajibikaji na utawala bora katika shirika ikiwa ni pamoja na kuweka nguzo za kulisimamia shirika na kuwapima wakurugenzi kwa utekelezaji wa majukumu yao. Katika ripoti zangu za miaka iliyopita, nilisisitiza utekelezaji wa pendekezo la kuzitaka bodi za wakurugenzi za mashirika kusaini mikataba ya kiutendaji ingawaje pendekezo hili bado halijatekelezwa katika mashirika mengi na taasisi nyinginezo. Ninatambua kuwepo kwa juhudi za serikali katika kutekeleza pendekezo langu kama inavyooneshwa katika waraka na. 1 wa Msajili wa Hazina wa tarehe 1 Januari, 2012 ukiyakumbusha mashirika kuzingatia sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2002 na barua yenye kumb. Na. CAN 114/572/01/8 ya tarehe 13 Februari, 2014.

Pamoja na juhudi hizo bado tatizo la kutukuwepo mikataba baina ya Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi limeendelea kuonekana katika mashirika na taasisi mbalimbali katika mwaka huu wa ukaguzi. Sehemu ambapo tatizo hili limeonekana ni Tume ya Ushindani (FCC), Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), Chuo cha Usafirishaji Tanzania (NIT) na Kampuni ya Madini Tanzania (STAMICO). Kukosekana kwa mikataba hii kunaifanya bodi za wakurugenzi kukosa vipimo vya ufanisi wa kazi na hivyo uwajibikaji kiujumla hauwezi kupimwa. Kwa hiyo, ninasisitiza kuwa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za

Umma ziongeze kasi katika kufuatilia na kuhakikisha zinaningatia Sheria ya Msajili wa Hazina.

# SURA YA TISA

## HALI YA MADENI YA SERIKALI KWENYE MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

### 9.0 Utangulizi

Tanzania ina Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipatayo sita (6) ambayo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na maendeleo ya wanachama wake. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Pensheni wa PPF, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu wa GEPF. Mifuko hii inasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

Hata hivyo, Mifuko hii imekuwa ikiathiriwa kwa kiasi kikubwa na mikopo ambayo hairejeshwi hasa ile iliyokopeshwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi zake. Baadhi ya mikopo hii haina mikataba ya kisheria wala dhamana ya Serikali. Hali hii inaiweka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika hatari ya kupoteza mikopo hiyo, tozo na riba zake au kutokurejeshwa kwa wakati.

Sura hii inaelezea hali ya madeni ya Serikali katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii na athari zake kwa Mifuko hiyo na Serikali kwa ujumla.

### 9.1 Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hutumia fursa mbalimbali katika kuwekeza fedha za michango ya wanachama kwa malengo ya kupata faida ili kuiwezesha kukua na kuwa na uhakika wa ulipaji mafao kwa wastaafu, kutoa huduma kwa wanachama na kumudu gharama za uendeshaji wa mifuko hiyo. Kwa Tanzania, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekua ikiwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo yenye riba kwa Serikali na Taasisi zake.

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo imekuwa ikiwekeza ni pamoja na Mfuko wa Pensheni wa PPF, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu wa GEPF. Pia, Mifuko ya Hifadhi za Jamii imekuwa ikiwekeza kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa kufuata miongozo iliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

## 9.2 Sera na Mwongozo wa Uwekezaji wa Fedha za Mifuko

Kwa kuzingatia matakwa ya aya ya 3.12 ya sera ya Mifuko ya Jamii ya mwaka 2003, mwongozo wa uwekezaji wa fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2012, uliandaliwa. Mwongozo huu uliandaliwa kwa kuzingatia uhakika wa mapato ya uwekezaji na ukwasi kwa kuwa fedha za mifuko zimekuwa zikielekezwa kwenye maeneo ambayo hayana mwamko wa kiuchumi. Uwekezaji wa fedha za mifuko ni kazi isiyoepukika kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kuendelea kwa mifuko hii na uboreshaji wa mafao ya mifuko kwa wanachama kunategemea sana mapato yanayotokana na uwekezaji.

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekua ikiwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo yenye riba kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, Serikali imekuwa ikidhamini Mashirika ya Umma yanayokopeshwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Serikali imekuwa ikikopa fedha hizi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Hivyo, Serikali inawajibika kulipa mikopo yote ambayo imekopeshwa yenyewe na ile iliyotolewa kwa Taasisi/Mashirika iliyoyadhamini endapo Mashirika hayo yatashindwa kulipa.

## 9.3 Deni la Serikali katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Ukusanyaji wa mikopo, tozo na pato la riba za mikopo ni muhimu kwa mifuko ili kuiwezesha kulipa mafao yanapohitajika, kumudu gharama za uendeshaji wa mifuko, na kutumia fursa za uwekezaji zinazojitokeza ili kuziwekeza tena fedha hizo.

Deni la Serikali kwa mifuko ya Hifadhi ya Jamii limekua likiongezeka kila mwaka bila kurejeshwa au kurejeshwa kwa kiasi kidogo sana. Kwa mujibu wa barua za uthibitisho kutoka kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2014 deni la Serikali kwa Mifuko lilifikia kiasi cha Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.698 ambapo Shilingi za Kitanzania bilioni 975.048 zilipaswa ziwe zimekwishalipwa lakini bado hazijalipwa.

**Jedwali 14: Deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kufikia Tarehe 30 Juni, 2014**

| Mfuko wa Hifadhi ya Jamii | Jumla ya Deni (Sh.) | Kiasi ambacho kilitakiwa kiwe kimeshalipwa (Sh.) |
|---|---|---|
| LAPF | 173,231,417,845.00 | 94,655,371,891.00 |
| PSPF | 460,995,168,878.82 | 251,942,767,372.27 |
| PPF | 221,070,451,951.77 | 27,252,909,658.32 |
| NHIF | 105,792,983,055.76 | 26,325,247,799.96 |
| NSSF | 722,460,946,894.36 | 575,048,756,582.94 |
| GEPF | 14,333,964,512.22 | - |
| **Jumla** | **1,697,884,933,137.93** | **975,048,756,582.94** |

***Chanzo:*** *Barua za uthibitisho za hali halisi za madeni hadi tarehe 30 Juni, 2014 kutoka kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufuatia barua ya CAG ya kuomba taarifa hizo.*

## 9.4 Ripoti ya Kikosi Kazi Juu ya Deni la Serikali katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliguswa na hali ya deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kamati ilikutana na Serikali pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kujadili na kupata maelezo juu ya madeni haya na hatua za kuchukua kuhusiana na namna ya ulipwaji wa madeni haya. Takwimu za madeni haya kati ya Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zilitofautiana kama ilivyoripotiwa katika aya ya 1.1.2 ya ripoti ya madeni ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwenye kikao cha PAC cha tarehe 24 Oktoba, 2014.

Kutokana na tofauti hizo za takwimu, kiliundwa kikosi kazi kilichojumuisha wadau mbalimbali kutoka Serikalini, Taasisi za Serikali/Mashirika ya Umma na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kufanya usuluhisho wa taarifa hizo na kutoa taarifa sahihi za deni la Serikali katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Taarifa ya kikosi kazi hicho iliwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) cha tarehe 24 Oktoba, 2014. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ilikubaliwa na wadau wote kuwa jumla ya deni la Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.875 ambapo kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 937.865 kilitakiwa kiwe kimesharejeshwa katika Mifuko husika. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 7 Machi, 2015, kiasi hicho cha fedha kilikuwa hakijarejeshwa kwenye Mifuko husika.

**Jedwali 15: Deni la Serikali kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii hadi tarehe 30 Septemba, 2014**

| Mfuko wa Hifadhi ya Jamii | Jumla ya Deni (Sh.) * | Kiasi ambacho kilitakiwa kiwe kimeshalipwa (Sh.) * |
|---|---|---|
| LAPF | 173,231,417,845.00 | 94,655,371,891.00 |
| PSPF | 478,564,986,495.99 | 273,422,154,530.03 |
| PPF | 275,682,357,071.87 | 53,269,846,358.40 |
| NHIF | 106,576,578,959.88 | 27,651,457,652.66 |
| NSSF | 827,506,941,339.53 | 488,866,404,953.71 |
| GEPF | 14,333,964,512.22 | - |
| **Jumla** | **1,875,896,246,224.49** | **937,865,235,385.80** |

**Chanzo**: *Taarifa ya kikosi kazi iliyowasilishwa kwenye kikao cha kamati ya bunge ya hesabu za serikali (PAC) cha tarehe 24 oktoba, 2014 na kama inavyoonekana kwenye aya ya 2.7.1 ukurasa wa 34 wa ripoti namba TK/02 JAN.2015 ya PAC kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2014*

** Jumla ya madeni na kiasi kilichopaswa kulipwa vinajumuisha deni lililokopwa, riba pamoja na adhabu.*

Kwa mujibu wa ripoti ya kikosi kazi na ripoti ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali namba TK/02 JAN.2015 ya mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013, deni la Serikali la Shilingi za Kitanzania Trilioni 1.875 halijajumuisha jumla ya Shilingi za Kitanzania Trilioni 7.1 ambalo ni deni la Serikali inalodaiwa na PSPF tangu mwaka 1999 ambapo PSPF iliwalipa mafao waastaafu ambao walikua hawachangii lakini wanatakiwa kulipwa mafao ya kustaafu kwa mujibu wa sheria.

## 9.5 Mikopo Iliyotolewa kwa Serikali na Taasisi zake Bila Kusaini Mikataba

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa baadhi ya mikopo ilitolewa kwa Serikali na Taasisi zake kwa makubaliano ya maongezi wakati mikataba ya kisheria ya mikopo hiyo na dhamana ya Serikali kwa mikopo ya taasisi hizo vikiwa bado havijakamilishwa. Kutokuwepo kwa mikataba ya kisheria na dhamana ya Serikali kwa mikopo hii, kunatia shaka juu ya uhakika wa ulipwaji au mipango ya ulipwaji wa madeni haya hali inayoathiri utendaji wa Mifuko.

Ilibainika kuwa Mfuko wa LAPF ulikikopesha Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 36.185 kabla ya kusaini mkataba au kupata dhamana ya Serikali katika mkopo huo. Hali hii iliulazimu mfuko wa LAPF kufuta mapato ya riba za mkopo huo. Pia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulitoa mkopo wa jumla ya Shilingi za Kitanzania bilioni 43.356 kwa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa

ajili ya ujenzi wa kituo cha utabibu (awamu ya kwanza) kabla ya kuingia mkataba au kupata dhamana ya Serikali kwa mkopo huo. Mikopo hiyo imetolewa miaka mingi iliyopita.

## 9.6 Athari za Kutorejeshwa kwa Mikopo

Ucheleweshwaji wa ulipaji wa mikopo hii unaweza kuwa na madhara makubwa kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kiasi cha kuathiri uendeshaji wa mifuko na uwezo wa Mifuko kumudu kulipa/kukidhi mahitaji ya muda mfupi na mrefu ikiwa ni pamoja na kushindwa kulipa mafao kwa wanachama wanaostaafu. Pia fedha zilizokopeshwa kwa Serikali bila kurejeshwa zinainyima Mifuko ya Hifadhi ya Jamii fursa ya kuwekeza kwenye maeneo yenye faida zaidi na pengine zingeweza kuwekezwa sehemu nyingine ili kupata faida kubwa zaidi. Mikopo hii inakwamisha au kuathiri juhudi na wajibu wa Mifuko kufanya kazi zao ipasavyo.

Kwa upande mwingine, mzigo wa madeni kwa Serikali unazidi kuongezeka kwa kuwa baadhi ya mikopo hii ina riba na tozo za adhabu za ucheleweshaji malipo. Ongezeko la riba na adhabu zinazotokana na mikopo lisingekuwepo laiti kama Serikali ingelipa madeni haya kwa wakati unaotakiwa. Lakini kwa mwenendo na hali hii ya kutolipa au kurejesha kwa kasi ndogo sana, kunaashiria kuwa deni hili litaongezeka huku likiathiri Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

## SURA YA KUMI

## MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU

### 10.0 Utangulizi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa Mamlaka chini ya Kifungu Na. 29 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ya kufanya ukaguzi maalumu au kwa kufuatia maombi ya mtu mwenye mamlaka, Taasisi, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

Kwa mujibu wa kifungu hicho cha sheria, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya jumla ya kaguzi maalumu tatu katika Bodi ya Pamba ya Tanzania (TCB), Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA) na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL).

Matokeo ya kaguzi hizi maalumu, yameanishwa kwa muhtasari katika ripoti hii, na matokeo ya kina yanapatikana katika ripoti husika ambazo hupatikana katika Mamlaka zilizoomba kaguzi hizo. Matokeo ya taarifa za kaguzi maalumu yanaainishwa kwa kifupi kama ifuatavyo:-

### 10.1 Bodi ya Pamba Tanzania (TCB)

Ukaguzi huu maalumu umetokana na maombi yaliyotolewa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia barua yenye Kumb. **Na.CAB 65/138/01** ya tarehe 6 Juni, 2013 ikiniomba nifanye ukaguzi maalumu ili kubaini ukweli kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za ruzuku ya wakulima wa pamba iliyotolewa na Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Matokeo ya ukaguzi maalumu wa Bodi ya Pamba Tanzania yalikuwa kama ifuatavyo:-

**(a)** Kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 166.45 kililipwa kama ruzuku na Bodi ya Pamba kwa baadhi ya makampuni yanayonunua pamba ikiwa ni zaidi ya kiasi kilichostahili kulipwa kwa kampuni hizo. Baadhi ya wanunuzi wa pamba walidai ruzuku zaidi ya kiasi kilichostahili. Malipo hayo yalifanyika bila kuhakikiwa na timu ya wakaguzi wa Bodi ya Pamba kinyume na taratibu. Baadhi ya malipo hayakuwa na saini za walioandaa malipo hayo na pia hayakuwa na saini za ofisa mwandamizi aliyepitia usahihi wake. Hali hii ilithibitisha

kuwepo kwa udhaifu mkubwa katika udhibiti wa ndani wa Bodi ya Pamba.

**(b)** Wakati wa ukaguzi, wakaguzi walitembelea kampuni ya S & C Ginning Company Ltd ili kuhakiki kiasi ambacho mnunuzi (S & C Ginning Company Ltd) aliwalipa wakulima kutokana na ruzuku ya Shilingi za Kitanzania Milioni 237.99 alizopokea toka Bodi ya Pamba kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Hata hivyo, zoezi hili halikuwezekana kwa sababu uongozi wa kampuni ulidai kwamba hati zote za malipo zilichukuliwa na Wakaguzi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Uhakiki wa ziada ulifanyika baada ya ukaguzi huu maalumu na kubaini kwamba kati ya Shilingi za Kitanzania Milioni 237.99, nyaraka zenye jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 169.2 zilionekana kuwa zimelipwa kwa wakulima wa pamba huku nyaraka zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 68.7 hazikupatika kwa ajili ya uhakikiwa. Kutokana na kukosekana kwa hati hizo, wakaguzi walishindwa kujiridhisha kama Kampuni ya S & C Ginning Company Ltd iliwalipa Wakulima wa Pamba kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 68.7.

**(c)** Ukaguzi ulibaini kwamba, makampuni mawili ya Badugu Ginning Company Limited na Vearrian (T) Limited ambayo yalipata ruzuku kutoka Bodi ya Pamba, yalifunga biashara baada ya msimu wa ununuzi wa pamba kwisha. Makampuni hayo yalifunga biashara yakiwa na ruzuku ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 105.8 ambazo hazikulipwa kwa wakulima.

Ukaguzi ulibaini kuwa, wakulima waliopoteza stakabadhi zao za mauzo ya Pamba hawakulipwa fedha za ruzuku kwa kukosa vielelezo vya kuthibitisha mauzo yao ya pamba. Kampuni nne (4) ambazo ni Fresho Investment Co.Ltd, Gaki Investment Co.Ltd, Kahama Cotton Co.Ltd na Roko Investment zilikuwa bado hazijawalipa wakulima kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 104.68 ambao hawakuwa na stakabadhi za mauzo ya pamba. Fedha hizo hazikurudishwa Hazina kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali.

**(d)** Mjumbe mmoja wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Pamba alikuwa ni miongoni mwa wamiliki wa makampuni yanayonunua zao la pamba. Kutokana na umuhimu na majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi katika kusimamia shughuli za Bodi ya Pamba, Mjumbe huyu kujihusisha na makampuni yanayonunua pamba kunaleta mgongano wa kimasilahi kati ya Bodi ya Pamba na kampuni hizo.

**(e)** Bodi ya Pamba ya Kanda ya Mwanza inawajibika moja kwa moja na utunzaji wa takwimu za ununuzi wa pamba toka kwa wanunuzi wa pamba. Baada ya kupitia mawasiliano kati ya Bodi ya Pamba Makao Makuu na Ofisi ya Kanda Mwanza, ilibainika kwamba baadhi ya makabrasha yaliyopelekwa Makao Makuu kwa ajili ya madai ya ruzuku, hayakuwa yamepitiwa vizuri na maofisa waandamizi kwenye Ofisi za Kanda. Hivyo, makabrasha hayo yalikuwa na makosa na kulikuwa na uwezekano wa ubadhirifu wa mali ya Umma.

## 10.2 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA)

Ukaguzi maalumu ulifanyika kutokana na ombi la Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya kupitia barua yenye Kumb.Na.UWSA/MB/C/UM/16/66 ya tarehe 05 Aprili, 2013 ikiomba ufanyike ukaguzi maalumu katika Mamlaka. Katika ukaguzi maalum wa MBEUWSA nilibaini yafuatayo:-

(a) Katika kipindi cha mwaka 2010/11 na 2011/12 Mamlaka ilitumia kiasi cha jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 554.6 kwa ununuzi wa mita na viungio vya kuzifungia. Katika manunuzi haya ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Mamlaka haikuweka kumbukumbu sahihi kuonyesha jumla ya mita zilizonunuliwa, zilizofungwa kwa wateja na zilizokuwepo ghalani. Hali hii ilidhihirisha kuwa Mamlaka ina mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani.

(b) Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa Mamlaka hukusanya mapato yake ya mauzo ya maji kwa kuwapelekea wateja Ankara za kila mwezi. Hata hivyo, wapo wateja 2,399 ambao hawajafungiwa mita lakini wanapata huduma za maji. Wateja hao huwa wanalipa kiwango maalum kwa kila mwezi (flat rate) baada ya kupelekewa Ankara. Katika Ankara hizo ambazo wateja hupelekewa kila mwezi Mamlaka inatoza tozo la huduma (service charge) kwa wateja wake wote.

(c) Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa udhaifu katika udhibiti wa hati za madai ambapo kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2012 hati zenye thamani ya jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 155.3 hazikuingizwa kwenye mfumo wa kompyuta (quickbook accounting) unaotumiwa na Mamlaka. Hii ina maana kuwa Watumishi wasio waaminifu wameweza kufanya malipo yasiyokuwa na manufaa kwa Mamlaka nje ya mfumo wa komputa pasipo kujulikana.

(d) MBEUWSA ilibainika kuwa na mgongano wa kimasilahi katika ununuzi uliyofanyika na Mamlaka ambapo kampuni ya Transportation Agricultural and Milling Services inayomilikiwa na Mkuu wa Kitengo cha Fedha cha Mamlaka, ilipewa zabuni za kutoa huduma kwa

Mamlaka yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 825,200 bila kufuata taratibu na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

(e) Mamlaka ilitoa ajira mpya katika kipindi cha mwaka 2010 na mwaka 2013 bila kufuata kanuni na taratibu za ajira za Mamlaka. Ukaguzi maalumu ulibaini kuwa kati ya ajira mpya 62 ajira za watumishi 30 zilitangazwa kwa mujibu wa sheria lakini ajira za watumishi wengine 32 hazikutangazwa kinyume na matakwa ya sheria za ajira. Kati ya waajiriwa hao wapya, waajiriwa watano (5) ambao ni (Msimamizi wa Mita, Mhasibu wa Mapato, Afisa Mahusiano Msaidizi, Mhasibu na Mkaguzi Mwandamizi wa Ndani) walipewa mishahara mikubwa isiyoendana na nafasi zao za kazi. Pia, kulikuwa na waajiriwa wengine wapya walioajiriwa kwenye nafasi ambazo hazipo kwenye ikama (scheme of service) na katika muundo wa utawala (Organization Structure) wa Mamlaka. Ukaguzi maalumu ulibaini pia kuwa, msimamizi wa kitengo cha ‘‘mitashop’’ aliajiriwa na Mamlaka bila kufanyiwa usaili na akapewa mshahara mkubwa kuliko mshahara uliopo kwenye Ikama (Scheme of service) ya Mamlaka (MBEUWSA).

(f) Ukaguzi ulibaini kuwa wazabuni walikuwa wanaleta mita na kupokelewa na kitengo cha ‘mita shop’ kabla ya kupokelewa kwanza ghalani ndipo zipelekwe ‘mita shop’. Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka haifanyi zoezi la kuhesabu mita (stock taking) jambo ambalo limesababisha kutokuwepo na taarifa sahihi za mita.

(g) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEUWSA) ilionekana kutokuzingatia kanuni za fedha za Mamlaka. Malipo yafuatayo yalifanyika yakiwa na mapungufu:

Hati za malipo zenye thamani ya jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 71.25 ziliandaliwa na Mamlaka pasipo kuonyesha kasma husika za malipo. Aidha, wakaguzi walibaini malipo yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 18.94 ambayo hayakuidhinishwa na Wakuu wa Idara kinyume na kifungu Na.8.3.5 (e) cha Kanuni za Fedha za Mamlaka. Ilionekana pia kuwepo kwa malipo yaliyoidhinishwa na mlipwaji mwenyewe kinyume na kifungu Na.4.1.10 na 4.2.3(b) yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 10.5.

Wakaguzi walibaini uwepo wa malipo ya umeme kwa TANESCO yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 28.25 yaliyolipwa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka kinyume na kanuni za fedha za Mamlaka. Hata hivyo, wakaguzi hawakupewa stakabadhi ya malipo kutoka TANESCO ya kukiri kupokea fedha hizo.

Kulikuwepo na baadhi ya hati za malipo zisizogongwa mhuri wenye neno 'PAID' kinyume na kifungu Na.8.3.12 cha Kanuni ya Fedha za Mamlaka na kiasi kilicholipwa kupitia hati hizo ni Shilingi za Kitanzania Milioni 382.7. Hali hiyo inaweza kupelekea malipo kufanyanyika zaidi ya mara moja kama hati hizo zitawasilishwa tena kwa malipo. Wakaguzi walibaini kuwa fedha zilizokuwa zinachukuliwa benki kwa ajili ya matumizi ya ofisi zilikuwa zinaandikwa jina la mfanyakazi wa Mamlaka badala ya kuandikwa jina la mlipwaji ambaye ni Mamlaka. Hii inaweza kusababisha Mamlaka kupoteza fedha zake kama mfanyakazi huyo hatakuwa mwaminifu. Malipo yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania Milioni 110.1 yalichukuliwa kutoka benki kwa utaratibu huo.

Wakaguzi walibaini kuwa Mamlaka ililipa fidia ya jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 62.7 kwa wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa na Mamlaka kupitisha bomba kwa ajili ya Mradi wa Maji wa awamu ya pili. Baadhi ya malipo hayo ya Shilingi za Kitanzania Milioni 32.1 yalifanyika kwa njia ya fedha taslimu badala ya hundi kinyume na taratibu za Mamlaka. Tathmini ya maeneo yaliyoathirika kwa ajili ya mradi wa maji ilifanywa na kitengo cha Mahusiano ya Umma na Idara ya Ufundi ambavyo havina utaalam wa kufanya tathmini. Kwa hiyo, hakuna ushahidi kuwa fidia iliyolipwa ilikuwa sahihi.

Pia, Mamlaka ilifanya malipo ya kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 70.1 bila ya kuwepo kwa ankara za madai ili kuhakiki kama malipo hayo yalikuwa sahihi.

## 10.3 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

Ukaguzi maalumu wa TTCL ulifanyika kufuatia ombi la Wakurugenzi wa Bodi ya TTCL kutokana na tuhuma mbali mbali zilizotolewa juu ya kampuni hiyo. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi huo maalum:-

(a) Ukaguzi uligundua kwamba watumishi wa TTCL na Menejimenti ya TTCL walitegemea wakati wote kupata taarifa za fedha kutoka kwenye ''MS Excel'' badala ya kutumia mfumo wa kutoa taarifa za fedha wa SunSystem uliowekwa na kampuni. Hali hii inaleta ugumu kuziamini taarifa za kampuni kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zinaweza kuwa na makosa ambayo hayawezi kuonenakana na kurekebishwa kwa mara moja.

(b) Menejimenti ya TTCL hupitia na kuhakiki mifumo na taratibu mbalimbali katika idara za kampuni hiyo. Hata hivyo, iligundulika kuwa zoezi hili lilikuwa halifanyiki kwa ufanisi na ripoti zilikuwa

haziandaliwi kwa ukamilimilifu. Wakaguzi walibaini kuwa mameneja wa idara waligundua vihatarishi (risks) vikubwa kwenye biashara ya kampuni lakini hawakuweka mifumo madhubuti ya ndani ili kuweza kuzuia vihatarishi hivyo hata pale ambapo palikuwa na mifumo ya udhibiti wa ndani ufanisi wake haukusimamiwa ipasavyo.

(c) Menejimenti ya TTCL haikutoa taarifa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni kwenye masuala muhimu yaliyotakiwa kupelekwa kwenye Bodi hiyo kwa ushauri kwa ajili ya kupata kibali au kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya utekelezaji. Kwa mfano, wakati wa uboreshaji wa mfumo wa taarifa wa SunSystem Bodi haikupewa taarifa kuwa mfumo huo ulisimama na kushindwa kufanya kazi kwa kipindi cha miezi minne.

(d) Menejimenti ya TTCL haikuwa makini katika kusimamia kazi na shughuli muhimu za kampuni kama vile kuendeleza mifumo ya mitandao kulisababisha kuwepo kwa kazi ambazo hazijakidhi viwango na kutopokelewa kwa huduma na vifaa mbalimbali.

Kutokuwa makini na kukosekana kwa uangalizi mzuri wa Menejimenti ya TTCL kwenye shughuli za kampuni kulipelekea kuwepo kwa udanganyifu kwenye maandalizi ya mishahara (payroll processing) ambapo mtumishi mmoja alikuwa anaanzisha maandalizi ya mishahara na kumaliza mchakato mzima wa kuandaa mishahara hadi kufikia hatua ya malipo bila kuwepo uangalizi na usimamizi wa kutosha.

Mhasibu aliyekuwa anashughulikia mishahara toka mwezi Agosti 2007 hadi mwezi Januari 2011 alipangiwa kazi nyingine kama Kaimu Meneja wa Uhasibu lakini aliendelea na kazi ya kuandaa mishahara kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kuulizwa na menejimenti ya TTCL akiwepo Mtendaji Mkuu na Mkuu wa Idara ya Fedha (Chief Finance Officer) ambao walikuwa na jukumu la kusaini malipo ya mishahara ya watumishi wa TTCL.

Katika kuandaa malipo ya mishahara, mtumishi huyo aliweza kujiongezea mshahara wake kupitia kwenye mfumo wa mishahara wa TTCL. Kutokana na nyaraka zilizokaguliwa zilidhihirisha kuwa jumla ya kiasi cha jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 71.8 kililipwa kwenye akaunti zake binafsi za benki kukiwa na kiasi kilicholipwa zaidi ya mishahara yake ya kawaida. Udanganyifu huo wa kujiongezea mshahara uliwezekana kwa sababu mfumo wa kompyuta wa kuandaa mishahara haukuwa unahitaji kuidhinishwa na afisa mwingine kabla ya kulipa mishahara. Ilibainika pia, hakukuwa na uhakiki wa mara kwa mara katika mfumo huo wa mishahara ambapo ni kiashiria tosha kuwa

miamala yenye shaka inaweza kupita bila kubainika mapema na kirahisi.

(e) Ukaguzi maalumu wa TTCL ulibaini kuwepo kwa ankara ya malipo namba INB80029 ya Shilingi za Kitanzania Milioni 99.48, ambayo yalilipwa mara mbili na TTCL kwa kampuni ya Adwest. Kampuni hii iliingia mkataba na TTCL wa kutoa huduma ya kusambaza nyaya (Optical fibre) na vifaa vyake (accessories) kwa ajili ya kuunganisha matawi mengine ya benki ya NMB na mtandao wa nyuzi ''fibre''. Malipo ya mwanzo ya Shilingi za Kitanzania Milioni 99.48 ya ankara hiyo yalilipwa na TTCL tarehe 13 Aprili, 2012, na malipo ya pili ya kiasi hicho hicho yalifanyika kwa kampuni hiyo tarehe 7 Septemba, 2012. Malipo hayo yaliyofanyika mara mbili yalifidiwa na Ankara zilizofuatia za kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni 93.02 kutoka kampuni ya Adwest. Fidia hiyo ilifanyika miezi sita baada ya malipo ya mara ya pili kufanyika. Menejimenti ya TTCL haikuijulisha kampuni ya Adwest baada ya kubaini kosa hilo la malipo mara mbili kwa ankara moja. Hali hii inaashiria wazi kuwa kulikuwa na dalili ya udanganyifu kwa kulipa malipo hayo mara mbili.

**(f) Manunuzi ya magari 10 na Bajaji 30**

**(i) Ununuzi wa Bajaji**

Kampuni ya Simu Tanzania Limited (TTCL) ilinunua bajaji 30. Ununuzi huu awali ulipendekezwa ufanyike kwa ushindani wa kimataifa kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Milioni 156 na ikapitishwa na kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wa TTCL cha Disemba 2011 kuwa bajaji hizo zitanunuliwa kwa mchakato wa manunuzi wa ushindani wa kimataifa. Hata hivyo, Bodi ya Zabuni ya TTCL ikatengua uamuzi huo na kutumia zabuni zuifu (restricted tendering) kinyume na maamuzi yaliyofanywa na Bodi ya Wakurugenzi walioidhinisha mchakato wa manunuzi wa ushindani wa kimataifa. Pia, ilibainika kuwa ubatilishwaji wa maamuzi ya Bodi ya Zabuni hayakupata ridhaa ya Bodi ya Wakurugenzi wa TTCL.

Kati ya wazabuni wanne (4) waliopewa makabrasha ya zabuni ni mzabuni mmoja tu alirudisha majibu. Bodi ya zabuni hata hivyo iliamua kuendelea na mchakato huo kwa madai ya uharaka wa kukamilisha zabuni hiyo ya ununuzi wa bajaji. Hali hii ya manunuzi inaweza kuathiri uwezo wa kampuni (TTCL) kutokana na kutofaidika na ushindani wa bei katika manunuzi.

**(ii) Manunuzi ya Magari 10 aina ya Toyota**

TTCL iliingia mkataba na kampuni ya Toyota Tanzania kwa ajili ya ununuzi wa magari matano (pick ups) na mengine matano aina ya

‘Station Wagon’ kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.254. Maamuzi ya kuagiza magari hayo kupitia Toyota Tanzania bila kufanya ushindani na makampuni mengine yalifanywa na Bodi ya Wakurugenzi wa TTCL kwa kufuata mapendekezo kutoka kwa Menejimenti ya Kampuni ya TTCL. Taarifa ya Kamati ya tathimini ilionyesha kwamba baadhi ya vigezo vilivyowekwa havikuwa vimetimizwa na Toyota Tanzania kama vile rangi za magari kuwa ya ‘Lemmon chrome yellow’. Pamoja na hayo, Toyota Tanzania haikukidhi kigezo cha uwezo wa namba ya abiria ndani ya gari na uthibitisho wa kutoka kwa mtengenezaji wa magari hayo. Ijapokuwa zabuni hii ilionekana kuwa na mapungufu yote hayo, Kamati ya Tathimini iliendelea kupendekeza kuwa zabuni hiyo ipewe Toyota Tanzania pamoja na kutokukidhi vigezo vingi vilivyoainishwa katika zabuni hiyo.

**(g) Usimamizi wa Matumizi ya Mafuta Usioridhisha**

Ukaguzi maalumu ulibaini kutokuwepo na umadhubuti katika vipimo vya mafuta kulikopelekea kutumika kwa ‘‘dipstick’’ mbovu katika upimaji wa mafuta kwenye mapipa kulikopelekea upotevu wa lita 1,900 sawa na Shilingi za Kitanzania 3,300,300 katika kituo cha Mwenge. Ukaguzi ulibaini kuwa, kanuni iliyotumika kubadilisha uniti (units) kwenda kwenye lita ilitiwa dosari (iliharibiwa) ili isitoe vipimo halisi vya mafuta yaliyokuwa kwenye mapipa. Vipimo vilionyesha kutokutoa uhalisia wa matumizi ya mafuta na kusababisha hasara ya lita 9,640. Katika kituo cha TTCL Singida kulionekana kuwepo kwa upotevu wa mafuta kiasi cha lita 4,065.40 zenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 8,130,808, Tawi la HBU Zanzibar kulionekana kuwepo kwa hasara ya lita za mafuta 4,008 zilizokadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania 8,418,900.

Mkoa wa Tanga ulianzisha kiwango cha matumizi ya mafuta kwa majenereta ‘‘standby generators’’. Kiwango hicho kilizidishwa sana na kuisababishia kampuni ya TTCL kupata hasara ya lita 26,669.45 sawa na Shilingi za Kitanzania 53,338,900. Vituo vitatu vya kuongeza nishati (Power stations) vilikuwa vinafanya kazi zaidi ya muda wa kawaida na kiwango kilichowekwa cha matumizi ya mafuta hakikuwa cha kawaida hivyo kusababisha upotevu wa lita 1,284.35 za mafuta yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania 2,632,918 kwa mwaka 2011.

Ilibainika pia kuwa, magari mawili ‘‘Ford Ranger’’ na ‘‘Land Cruiser’’ yaliigharimu kampuni fedha nyingi za matengenezo zilizokadiriwa kuwa Shilingi za Kitanzania 9,505,021 kwa Ford Ranger na Shilingi za Kitanzania 7,343,500 kwa Toyota Land Cruiser kwa mwaka 2011. Hali hii ilionyesha kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa ndani wa kusimamia matumizi na safari za magari. Jumla ya lita 3,285 za

mafuta ya dizeli sawa na Shilingi za Kitanzania 6,570,000 yalibainika kutumika kujazwa kwenye magari matano bila taarifa ya Afisa msimamizi wa magari (Motor Transport Officer). Matumizi hayo hayakutolewa taarifa katika ripoti ya usimamizi wa safari na magari za mwaka 2011.

# SURA YA KUMI NA MOJA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 11.0 Mtazamo wa Jumla

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya masuala yaliyojadiliwa katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kutazamwa na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Masuala yote yaliyomo katika ripoti hii ni ya ujumla na ambayo ni muhtasari wa ripoti zilizopelekwa kwenye Menejimenti za Mashirika na mambo mengine muhimu yaliyojitokeza ambayo Umma unapaswa kuyafahamu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa Mamlaka kupitia Kifungu Na. 12 cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kutoa mapendekezo yatakayosaidia kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyo na tija, kuongeza ukusanyaji wa mapato, na kuondoa hasara ambazo zinasababishwa na uzembe, kutojali, wizi, ukosefu wa uaminifu, ubadhirifu na vitendo vya rushwa katika mali za umma ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za fedha za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zimeandaliwa kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2013, 31 Disemba, 2013 na 30 Juni, 2014. Kwa kutumia mamlaka niliyopewa chini ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, napenda kuhitimisha na kutoa mapendekezo kutokana na kaguzi zilizofanyika kama ifuatavyo;

## 11.1 Mapendekezo Maalum

### 11.1.1 Maoni ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokamilika

Nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zipatazo 125 kati ya kaguzi 180 zilizotakiwa kukaguliwa na ambazo zipo chini ya mamlaka yangu ya ukaguzi. Mashirika matatu (3) hayakuwasilisha hesabu zake kwa ajili ya ukaguzi. Kaguzi 52 zilizobaki zilikuwa katika hatua mbalimbali za ukaguzi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi, Mashirika mengine kutoandaa vikao vya Bodi za wakurugenzi kwa wakati na kushindwa kwa baadhi ya wakaguliwa kujibu hoja za wakaguzi kwa wakati hali iliyopelekea pia ukaguzi kutokamilika kwa wakati.

Kwa ujumla, matokeo ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kuzingatia idadi ya hati za ukaguzi zilizotolewa hayakubadilika sana ikilinganishwa na mwaka uliopita, isipokuwa kwa Mashirika manne (4) ambayo ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Chalinze yaliyopata hati zenye shaka ikilinganishwa na shirika moja (1) lililopata hati hiyo mwaka uliopita. Mashirika 105 (96%) yalipata hati inayoridhisha ikilinganishwa na Mashirika 92 (99%) ambayo yalipata hati inayoridhisha kwa mwaka uliopita. Mchanganuo wa misingi na aina za hati za ukaguzi yamejadiliwa kwenye sura ya pili (2) ya ripoti hii.

Ninapendekeza kuwa Mamlaka husika, zihakikishe kwamba Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati pindi muda wake unapokwisha, hatua za kinidhamu zinachukuliwa kwa Maafisa Watendaji Wakuu wote walioshindwa kuwasilisha hesabu kwa wakati na Serikali ichukue hatua za haraka kuyanusuru Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo zina hali mbaya kifedha. Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti kwenye Mashirika husika zinapaswa kuangalia njia mbadala za kuongeza vyanzo vya mapato ili kuziwezesha kujiendesha na kuhakikisha kuwa zinabana matumizi yake.

### 11.1.2 Utekelezaji wa Mapendekezo wa Ripoti Zilizopita

Katika ripoti zangu za miaka iliyopita, nilitoa mapendekezo ambayo yalihitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya utekelezaji. Kuna baadhi ya mapendekezo yamefanyiwa kazi na mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ofisi yangu ina jukumu la kuhakikisha kuwa mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti yanaleta tija katika Taifa. Lakini, jambo muhimu ambalo linaweza kuongeza motisha wa kazi katika ofisi yangu ni iwapo jitihada zinazofanywa na ofisi yangu zitatambulika na hatua za kutekeleza mapendekezo ya taarifa zangu zitachukuliwa. Ni jukumu la Serikali na wadau wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kutambua umuhimu wa mapendekezo ninayoyatoa na kuja na mikakati ya utekelezaji kwa ajili ya kurekebisha mapungufu hayo. Ikumbukwe kwamba, mapendekezo yanayotolewa kwenye ripoti zangu za kila mwaka yanakusudia kuongeza ufanisi na kufuata njia bora na sahihi za kuendesha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Napenda kukiri kupokea majibu ya Serikali ya ripoti yangu iliyopita kupitia barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye Kumb. Na.C/DE.85/229/01/72 ya tarehe 30 Agosti, 2014. Majibu niliyoyapokea kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali hayajitoshelezi kujibu mapendekezo yote niliyoyatoa katika taarifa yangu ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ya mwaka 2012/2013. Kuna mapendekezo mengi ambayo hayajafanyiwa kazi na baadhi yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Naiomba Serikali kuingilia kati hasa kwa yale mapendekezo yanayohusiana na Utawala Bora kwa kuwa yasipotekelezwa, ndiyo chanzo cha matatizo kwani yanasababisha Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kutofikia malengo kutokana na muingiliano wa kimaslahi kati ya watendaji na waliopewa jukumu la usimamizi.

Kuna mapendekezo yanayohusu Shirika husika la Umma na mengine ni ya jumla. Ninaomba Serikali kupitia Wizara Mama za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo, Bunge, Kamati za Hesabu za Bunge, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi kuhakikisha kuwa mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi yanafanyiwa kazi ili kuongeza uwajibikaji na matumizi mazuri ya rasilimali za Taifa katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma.

### 11.1.3 Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka 2012/2013

Nilibaini kuwa kulikuwa na madeni ya muda mrefu yanayodaiwa na Shirika la Posta Tanzania, Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam na Shirika la Nyumba la Taifa ambayo yalikuwa hayajalipwa kwa kipindi kirefu na hivyo kuathiri hali ya kifedha ya Mashirika hayo. Kwa hiyo, napendekeza kwamba menejimenti ya mashirika husika zifanye juhudi za ziada kukusanya madeni ya muda mrefu ili kuzinusuru Taasisi hizo.

Pia, nilibaini ucheleweshwaji katika kuwasilisha michango ya kisheria kama PAYE, SDL na VAT kwa Shirika la Posta Tanzania. Kushindwa kulipa michango ya kisheria kwa wakati kunapelekea adhabu kwa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Hivyo ninapendekeza Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania itekeleze Sheria za Kodi kwa kujaza fomu za malipo ya kodi na kulipa michango ya kisheria kwa wakati kama Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 na Sheria za Hifadhi za Jamii zinavyotaka.

Ili kuepuka malimbikizo ya riba katika maeneo yaliyotengwa na Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA) kwa ajili ya kujenga ukanda wa uwekezaji, napendekeza kwamba Menejimenti ya Mamlaka ikishirikiana na Wadau kuhakikisha malipo ya fidia

yanafanyika kwa wakati. Pia, Mamlaka iangalie athari za kulimbikiza riba na kuja na mikakati ya kuepuka hatari ya kutolipa fidia kwa wakati.

Kwa mikopo iliyodhaminiwa na Serikali kwa asilimia 100 kupitia Wizara ya Fedha iliyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) takribani kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 351.872, Serikali inashauriwa kuhakikisha mikopo hii inarejeshwa. Kutorejeshwa kwa mikopo hii iliyodhaminiwa na Serikali kunauweka Mfuko kuwa katika hatari zaidi ya kupoteza fedha za wanachama na hivyo kuhatarisha uwezo wa kuhudumia wanachama na kuweza kuwekeza zaidi katika miradi mingine.

### 11.1.4 Usimamizi wa Sheria ya Ununuzi na Mikataba

Kuanzishwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 pamoja na Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013 zinatoa miongozo ya kisheria inayoelekeza namna ambavyo ununuzi unavyopaswa kufanyika. Licha ya uwepo wa Sheria, baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma bado hazitekelezi Sheria za Ununuzi ya Umma na Kanuni zake ipasavyo. Kwa hiyo, ninaona kuna uelewa mdogo kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma umebaini kwamba shughuli za ununuzi katika baadhi ya Taasisi hazikufanyika kwa mujibu wa sheria. Ilibainika kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikusimamia vyema mikataba ya ununuzi. Kwa ujumla Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinashauriwa kubadili miendendo juu ya usimamizi wa mikataba wanayoingia na wazabuni kutoka siku ya kwanza ya utekelezaji wake. Kwa kuzingatia muhtasari wa mambo yaliyojitokeza kwenye sura ya tano, Taasisi za Umma zinashauriwa kufanya kazi kwa ukaribu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa mikataba inahakikiwa kabla ya kutiwa saini.

Wakuu wa Taasisi (CEOs), Vitengo vya Ununuzi (PMUs), Bodi za Zabuni, Kamati za Tathmini za Zabuni, na Watumiaji bidhaa au huduma ni vema wahakikishe wanatekeleza kikamilifu matakwa ya Sheria ya ununuzi hususani kwenye eneo la uaandaji na utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (APP). Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma wanapaswa kuhakikisha kuwa Vitengo vya Ununuzi na Bodi za Zabuni zinaundwa ipasavyo na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Kuhusiana na utunzaji wa kumbukumbu za ununuzi, nashauri Vitengo vya Ununuzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zihakikishe kunakuwepo na utunzaji mzuri wa nyaraka na kumbukumbu zinazohusiana na ununuzi.

Kuhusiana na kuchelewa kukamilika kwa mikataba, nashauri Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuzingatia masharti yote yaliyomo kwenye mikataba husika na kuhakikisha adhabu zinatozwa kwa wakandarasi wote ambao hawatatimiza yale waliyokubaliana katika mkataba. Nashauri pia, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zijiepushe na njia zisizo sahihi wakati wa kufanya ununuzi wa Umma, mfano ununuzi wa chanzo kimoja na zabuni zuifu. Ununuzi kwa njia hizi yafanywe tu pale ambapo mazingira yanaruhusu kwa kuzingatia Kanuni Na. 159 ya Kanuni za Sheria za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 na pia thamani ya fedha katika manunuzi izingatiwe.

Mamlaka ya Bandari Tanzania, Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania wanashauriwa kuimarisha vitengo vyao vya ununuzi ili viweze kutimiza wajibu wake wa kisheria wa kusimamia ununuzi kama Sheria ya Ununuzi wa Umma inavyotaka.

### 11.1.5 Usimamizi wa Rasilimali

Baada ya ukaguzi wa usimamizi wa mali za Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma, yafuatayo ni mapendekezo ya ukaguzi;

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zihakikishe zinapanga vizuri na kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza miradi mbalimbali ya maendeleo ili kufahamu iwapo zitamudu gharama za mradi husika hivyo kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati. Pia, Mashirika na Taasisi za Umma zinashauriwa kufanya ununuzi kulingana na uhitaji na kuepuka uhifadhi wa vifaa vingi kwenye maghala. Aidha, Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinapaswa kutumia vyema mali zake ili kuhakikisha zinafanya uzalishaji wenye tija. Kadhalika, mali zote zinazomilikiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinapaswa kujumuishwa kwenye vitabu vya hesabu. Mashirika na Taasisi za Umma pia zinapaswa kuthaminisha mali zake kila baada ya miaka mitatu hadi mitano kama inavyotakiwa na viwango vya kimataifa vya uhasibu. Pia, kwa yale Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zenye kupangisha majengo yake, zihakikishe kuwa kodi ya pango inakusanywa kikamilifu na kwa wakati.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma zinashauriwa kuweka mifumo thabiti katika usimamizi wa mafuta ya magari ili kupunguza gharama. Serikali kupitia Wizara ya Miundo Mbinu inapaswa kupeleka gari inalodaiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji au kurejeshe fedha zilizolipwa.

Kuhusiana na tofauti iliyoonekana ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 1.1 baina ya Mfuko wa Huduma za Mawasiliano na Kampuni ya Mawasiliano Zanzibar, Serikali inapaswa kuingilia kati na kusimamia utatuzi wa tofauti hiyo ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza.

Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma pia zinashauriwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia kwa kutumia njia za kielektroniki katika shughuli zake. Pia, Taasisi hizo zinashauriwa kuboresha sera zake za teknohama.

### 11.1.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Kama ilivyoelezewa kwenye sura ya saba, usimamizi bora wa rasilimali watu unaweza kusaidia Taasisi kufikia malengo ya kiutendaji iliyojiwekea kwa kuamsha ari ya kazi na wafanyakazi kuridhika na utendaji kazi katika ngazi zote.

Ninapendekeza tathmini ya utendaji kazi wa wafanyakazi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ifanyike kwa kuwa inatoa maoni juu ya utendaji wa wafanyakazi na kutambua maeneo ambayo yana udhaifu kwa ajili ya kuyaboresha. Gharama za wafanyakazi zinapaswa kutambuliwa katika kipindi ambacho mfanyakazi anatakiwa kulipwa badala ya kipindi ambacho atalipwa. Majalada ya wafanyakazi ni muhimu yakatunzwa vizuri yakiwa na nyaraka zote muhimu kama ilivyoainishwa kwenye sera na miongozo ya rasilimali watu. Pia, ni muhimu Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kuwasilisha makato ya kisheria ya michango ya wafanyakazi kwa wakati ili kuepuka adhabu na kutozwa riba. Serikali inapaswa kuridhia ajira za wafanyakazi wa ziada kujaza mahitaji yaliyopo kwenye Taasisi husika.

Aidha, Uongozi wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Tanga unapaswa kuandaa mpango kwa kurithisha madaraka mpango ambao unapaswa kujumuishwa katika mpango mkakati wa biashara na mipango. Kanuni za watumishi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ziboreshwe ili watumishi waliohudhuria mafunzo watoe maoni kutokana na mafunzo waliyoyapata.

### 11.1.7 Utawala Bora

